

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Nane – Tarehe 12 Aprili, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba niwape taarifa. Kama mlivyoona leo tumeingia hapa Bungeni kwa utaratibu mpya tofauti na ilivyozoleka. Kanuni ya 20(1)(c) ya Kanuni za Bunge inaeleza kwamba Spika ataingia na kutoka ndani ya ukumbi wa Bunge akiongozana na mpambe wa Bunge lakini haitoi maelezo ya mlango gani utumike wakati wa kuingia au kutoka Bungeni. (*Makofi/Kicheko*)

Katika Mabunge mengi ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Madola (*Commonwealth*) na nchi nyingine, utamaduni uliozoleka ni kwa Spika wa Bunge kuingia ndani ya ukumbi wa Bunge akitokea chumba maalum cha Spika (*Speaker's Lounge*). Baadhi ya nchi zenyе utamaduni huo ambazo mimi na misafara yangu mbalimbali tumewahi kushuhudia ni India na Uingereza, wana utaratibu kama huu tuliotumia leo.

Kwa kuwa tumekuwa tukiboresha taratibu zetu kwa kuiga mifano bora ya wenzetu, kuanzia leo tutaanza kutumia utaratibu huu mpya tuliotumia asubuhi ya leo kwa misafara

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

ya Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kuingia na kutoka Bungeni kwa kutumia mlango wa kuelekea *Speakers Lounge*, ni kuingia na kutoka kwa utaratibu huu hapa.

Waheshimiwa Wabunge, mlango mkuu wa mbele utaendelea kutumiwa na Waheshimiwa Wabunge kama kawaida yenu na Spika na msafara wake watautumia mlango huu mkuu wakati wa matukio maalum ya Kibunge kama vile wakati wa kufunga au kufungua Bunge au tunapokuwa na ugeni wa Kitaifa kama Mheshimiwa Rais akitutembelea tutaingia kwa lango lile kuu, katika siku za kawaida zote tutafuata utaratibu huu mliouona hapa mbele.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, hii ndiyo taarifa ambayo nataka kuitoa na ina faida nydingi. Wakati mwingine mnawenza mkawa na hasira tunapopita hapa mkaturukia hapo katikati ikawa tabu. Kwa hiyo, hata kiusalama hapa ni bora zaidi. (*Makofi/Kicheko*)

Katibu.

NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali, swali la kwanza ni kwa Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba yake Mheshimiwa Mbunge wa Rombo.

Na. 63

**Mgogoro kati ya Wafanyabiashara na
Manispaa ya Mpanda**

MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y RHODA E. KUNCHELA)
aliuliza:-

Kuna mgogoro kati ya Manispaa na wafanyabiashara wanaomiliki vibanda katika masoko ya Buzogwe Soko Kuu

na Mpanda Hoteli ambapo Manispaa inawaongezea kodi wafanyabiashara hao bila makubaliano ya pande zote mbili:-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kumaliza mgogoro huo maana ni muda mrefu sasa na wafanyabiashara wamefunga vibanda vyao wakisubiri muafaka na hivyo Serikali kushindwa kukusanya kodi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashari ya Manispaa ya Mpanda imejenga vibanda vya biashara katika masoko kwa ubia baina ya Halmashauri na wafanyabiashara (wamiliki/wajenzi). Masoko ambayo yaliongezewa ushuru wa pango ni masoko yanayomilikiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda ambayo ni soko kuu la Buzogwe na Azimio.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda iliamua kufanya mabadiliko ya ushuru baada ya kubaini kuwa wamiliki/wajenzi walikuwa wakinijufaisha wenyewe kwa kuwapangisha wafanyabiashara na kuwatoza kodi katika Sh.100,000 hadi Sh.150,000 na kuwasilisha kodi ya Sh.15,000 tu kwa mwezi kwa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya kodi yaliyofanyika kwa wamiliki/wajenzi ni kutoka Sh.15,000 hadi Sh.40,000 kwa mwezi. Wadau wote walishirikishwa na makubaliano yaliridhiwa katika vikao vya kisheria vya Halmashauri. Aidha, hakuna maduka yaliyofungwa, huduma zinaendelea kama kawaida na Halmashauri imeendelea kukusanya mapato.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zinaweza kufanya marekebisho ya kodi wakati wowote. Utaratibu unaotumika katika kuibua na kuongeza kodi/tozo huanzishwa, huchakatwa na kuamuliwa na kikao cha Kamati ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Halmashauri husika.

SPIKA: Mheshimiwa Selasini, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Wafanyabiashara kote nchini hivi sasa wanalalamika biashara zao kuyumba na ukweli uliopo ni kwamba tatizo hili bado linaendelea katika Manispaa hii ya Mpanda. Je, Serikali iko tayari kuiagiza Halmashauri kwa *spirit* ya utawala bora kukaa tena na wafanyabiashara hawa ili kuweza kwa pamoja kujadili kiwango ambacho Halmashauri na wafanyabiashara watanufaika ili sasa pande zote mbili ziweze kufanya kazi bila manung'uniko?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika utendaji bora na ushirikiano na Halmashauri ni kwamba maeneo mengi utendaji unaonekana kukwama kwa sababu wakati mwingine mabavu yanatumika katika kuweka hivi viwango vya kodi na kadhalika. Ni lini Serikali itatoa maagizo ya hakika kabisa ili Halmashauri zisigombane na wateja wao ambao ni hawa wafanyabiashara na sasa hivi tunavyohimiza Halmashauri ziweze kuongeza vyanzo vipyta vya mapato ili mapato ya Serikali kokote katika nchi yetu yasipotee tu kwa sababu ya uhusiano mbaya kati ya Halmashauri pamoja na wafanyabiashara? (*Makofii*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaibana Serikali kwa jambo ambalo ni letu wenyewe. Madiwani ndiyo mnaongeza hizo bei halafu mnaitaka Serikali iingilie kati wakati ninyi wenyewe ndiyo Madiwani mnaongeza bei.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Josephat Kandege, ufanuzi tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa

Spika, nafarijika swalii kama hili kutoka kwa Mheshimiwa Selasini na bahati nzuri yeye ni Mjumbe wa Kamati ya Utawala na TAMISEMI. Katika nafasi niliyopata kushiriki katika vikao vyake amekuwa akihimiza Halmashauri zihakikishe kwamba zinakusanya mapato yake ili ziweze kujiendesha.

Mheshimiwa Spika, umenisaidia. Sisi Waheshimiwa Wabunge ni Madiwani tukiwa kwenye halmashauri zetu. Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda ilishirikisha wafanyabiashara, zimeundwa Tume zisizopungua tatu na katika jibu langu la msingi nimeeleza hawa ambao wamekuwa wanapangishiwa wamekuwa wakilipa Sh.100,000 mpaka Sh.150,000.

Mheshimiwa Spika, sasa halmashauri katika kuona katika vyanzo vyao ambavyo ni vizuri wakavisimamia iko katika kupandisha kutoka Sh.15,000 ambayo imekuwa ikitozwa zaidi ya miaka 30 na kwenda mpaka Sh.40,000 which is very fair.

Mheshimiwa Spika, ameelezea juu ya suala zima la kutokuwa na migongano baina ya wafanyabiashara na halmashauri. Kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, ushirikishwaji umekuwepo na hata ninavyoongea leo hakuna hata kibanda kimoja ambacho kimefungwa katika Manispaa ya Mpanda kwa sababu ushirikishwaji umekuwepo. Zimekuwepo Tume zaidi ya tatu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba maridhiano yanakuwepo na halmashauri inapata chanzo chake cha pesa na kinatumika sahihi.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Mollel.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Siha inafanana na wilaya iliyotajwa hapo lakini kwa tofauti kidogo, Halmashauri ya Siha ina magulio, haina masoko. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano alishatoa maelekezo kwamba akinamama wanaotandaza bidhaa chini na wale ambao ni wa chini kabisa wasidaiwe ushuru.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha kabisa jana katika Wilaya ya Siha wananchi kwenye soko la Sanya Juu wameenda kulazimishwa kulipa ushuru kwa kutumia polisi na wananchi waliposema Rais alishasema sisi tunaotandika chini tusilipe waliambiwa Rais huyo huyo ndiye anasema tukusanye kodi na bado yeye anatuvuruga kwenye kukusanya kodi, lipeni ushuru na polisi wakapelekwa sokoni na wananchi walipata tahiruki sana.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nielezwe kwamba tunawezaje kuwasaidia hawa akinamama ambaao ni vipedhi vya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari alishatoa maelekezo na yamekuwa yakipuuzwa na Halmashauri zetu. (Makof)

SPIKA: Majibu ya swali hilo muhimu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, maelekezo aliyotoa Mheshimiwa Rais kwamba wale akina mama ambaao wanapanga bidhaa zao ikiwa ni pamoja na wale ambaao wanauza ndizi wasibugudhiwe ni msimamo ambaao uko thabiti, hauyumbi hata mara moja. Kama kuna Mkurugenzi ye yote ambaye hataki kutekeleza kauli na maelekezo ya Mheshimiwa Rais tafsiri yake ni kwamba Mkurugenzi huyo hajitaki. (Makof)

Mheshimiwa Spika, naomba nikuhakikishie, leo wakati naingia nilimwambia Mheshimiwa Mollel katika maeneo ambayo nina wajibu wa kwenda kutembelea ni pamoja na Jimbo lake hii ni pamoja na kwenda kutazama eneo la ujenzi wa hospitali mpya ya wilaya. (Makof)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na swali linalofuata la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Viti Maalum Kigoma.

**Uhitaji wa Watumishi wa Afya Katika
Zahanati za Mkoa wa Kigoma**

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE aliuliza:-

Zahanati nyingi za Vijihi vya Mkoa wa Kigoma katika wilaya zote zina upungufu mkubwa sana wa watumishi wa afya na baadhi ya zahanati hazina Waganga hivyo huduma zinatolewa na Manesi Wasaidizi tu:-

Je, ni lini Serikali itapeleka watumishi wa afya wa kutosha katika maeneo hayo ili kuimarisha utoaji wa huduma za afya vijijini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Josephat Kandege, majibu ya swali hilo, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kigoma una jumla ya vituo vya kutolea huduma za afya 278, hospitali sita (6), vituo vya afya 32 na zahanati 240. Kati ya vituo hivyo, vituo vya Serikali ni 224 sawa na asilimia 80%, hospitali tatu (3), vituo vya afya 23 na zahanati 198. Idadi hii inajumuisha vituo vya mashirika ya dini, kambi za wakimbizi, binafsi na taasisi za umma kama Magereza, Polisi, Jeshi na *TRL*.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya watumishi wa sekta ya afya kwa mujibu wa ikama mpya ya mwaka 2014 katika vituo vya umma kimkoa ni 5,007, watumishi waliopo ni 1,663 sawa na asilimia 33.2 ya mahitaji na upungufu ni 3,344 sawa

na asilimia 66.8. Mkoa pamoja na halmashauri zimeendelea kukabiliana na changamoto hii kwa kushawishi wadau wa sekta ya afya wakiwemo *THTS, East African Public Health Lab Net, Engender Health* na *UNICEF* kusaidia kuajiri watumishi muhimu kwa muda/mkataba, pamoja na kuweka katika bajeti kwa ajili ya kuajiri watumishi wapya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Mkoa wa Kigoma umepatiwa watumishi wa afya 95 wakiwemo Madaktari watano (5), Matabibu 24, Wauguzi 33, Wafamasia 17 na Wataalam wa Maabara 16. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, mkoa umeomba kutengewa nafasi za ajira 1,667 kwa kada mbalimbali za afya.

SPIKA: Mheshimiwa Genzabuke, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Hospitali ya Wilaya ya Kasulu kuna upungufu mkubwa wa Madaktari na Wauguzi, Muuguzi mmoja anahudumia wodi moja akiwa peke yake hali inayosababisha azidiwe na shughuli. Wagonjwa wanawalalamikia Wauguzi kwamba hawawahudumii lakini ni kutokana na kuzidiwa na kazi nydingi. Je, ni lini Serikali itapeleka Waganga na Wauguzi ili kumaliza tatizo liliko katika Wilaya ya Kasulu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, katika Mkoa wa Kigoma kuna kambi tatu za wakimbizi. Wilaya ya Kasulu kuna Kambi ya Nyarugusu, Wilaya ya Kakonko kuna Kambi ya Mtendeli na Wilaya ya Kibondo kuna Kambi ya Nduta. Wagonjwa wanapozidiwa katika kambi mbili ya Mtendeli na Nduta katika Wilaya ya Kibondo na Kakonko, wale wa Nduta hupelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Kibondo na wale wa Mtendeli hupelekwa katika Kituo cha Afya cha Kakonko. Je, ni lini Serikali, kwanza, itapeleka pesa za kumalizia Hospitali ya Wilaya katika Wilaya ya Kakonko na kupeleka Wauguzi na Madaktari? Pili, katika Wilaya ya Kakonko ni lini nao

watapelekewa Waganga na Wauguzi wa kutosha ili kumaliza matatizo yaliyopo katika hospitali hiyo? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Kandege tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) : Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nimekiri upungufu wa waganga pamoja na watumishi wa afya kwa ujumla wake. Pia nimeeleza jinsi ambavyo katika bajeti ya 2018/2019 walivyoomba kupatiwa Waganga 1,667.

Mheshimiwa Spika, lakini ni nia njema ya Serikali ya kuhakikisha kwamba huduma ya afya inatolewa. Nimepata nafasi ya kwenda Kasulu na tatizo ambalo nimekutana nalo pale Kasulu ni pamoja na kutokuwepo vituo vya afya vya jirani ili hospitali ya wilaya iwe na sehemu ya kupumulia. Katika utaratibu mzima wa Serikali wa kuhakikisha kwamba huduma ya afya inapatikana ya kutosha. Miongoni mwa wilaya 67 ambazo zinaenda kupata hospitali za wilaya, Wilaya za Kigoma zitakuwepo ikiwa ni pamoja Uvinza, Buhigwe pamoja na Kasulu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, Kakonko kuna Kituo cha Afya kinaitwa Gwamanumbu na Lusesa nao wanaenda kupata kituo cha afya ambacho kina hadhi ya kuweza kufanya operesheni. Hii yote kwa ujumla wake unaona jinsi ambavyo Serikali ina nia njema ya kuhakikisha kwamba afya kama jambo la msingi linaenda kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Waziri wa Utumishi na Utawala bajeti yake imesomwa jana na sisi TAMISEMI pamoja na uhitaji wetu kibali cha ajira tunapata kutoka kwao. Naamini katika maombi haya ya wahudumu pamoja na Waganga 1,667 tutapata wa kutosha na tutaenda kupunguza huo uhaba wa watumishi.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, ye ye mwenyewe ni shuhuda kwamba kuna mashirika ambayo yamekuwa yakishirikiana na Serikali kwa sababu suala la wakimbizi huwezi uka-predict kwamba watakuja wangapi. Naamini kwa ushirikiano ambao umekuwa ukioneshwa hakika huduma ya afya itaenda kuboreshwa na tatizo hili litapungua.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa Mbunge wa Manyoni mtauliza maswali ya nyongeza kwa kuanzia halafu tutaendelea na wengine.

MHE. SUSAN A.J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Katika Kamati yetu ya huduma za jamii ni wazi kwamba tuna upungufu wa watumishi wa afya takribani 48%. Katika zoezi hili la uhakiki vituo vingi vya afya vimefungwa, hali inayosababisha akinamama wengi wajawazito kuendelea kufariki na hata takwimu zinaonesha kwamba wanaokufa ilikuwa 400 na zaidi kati ya vizazi 100,000 leo tunaongelea zaidi ya wanawake 500 na zaidi katika vizazi 100,000.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini sasa Serikali haiajiri wakati Madaktari wako kibao na watumishi hao wako nje ya ajira? Ni kwa nini Serikali haiajiri wakati watu wetu wanaendelea kufariki? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) : Mheshimiwa Spika, tumekiri juu ya upungufu wa wataalam wa afya lakini pia ni ukweli usiopingika kwamba unapoajiri *implication* yake ni suala la bajeti. Naamini kabisa kwa upungufu huu tulionao na idadi ya watumishi katika kibali ambacho kimetoka wanaoenda kuajiriwa ni pamoja na Madaktari. Naomba tuvute subira tupitishe bajeti hii wengi wa wale wanaoenda kuajiriwa itakuwa ni Madaktari ili kupunguza tatizo hili kubwa tulilonalo.

SPIKA: Mheshimiwa Massare.

MHE. YAHYA O. MASSARE: Mheshimiwa Spika, naomba nimuulize swali dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, matatizo yaliyopo huko Mkoani Kigoma yapo pia katika Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, kuna uhaba mkubwa wa watumishi, vituo vya afya na zahanati wakati mwingine vina mtumishi mmoja. Je, Serikali iko tayari sasa baada ya kuajiri kuleta watumishi katika Halmashauri ya Itigi? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo la nyongeza kutoka kwa Mbunge wa Manyoni Magharibi, Mheshimiwa Yahaya Massare, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, katika wale watumishi watakaokwenda kuajiriwa hakika tuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba sehemu ambayo kuna upungufu mkubwa ikiwa ni pamoja na jimbo lake tunawapeleka.

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Susan anaongea, aliongelea kuhusiana na baadhi ya vituo kufungwa na sisi Wabunge ni mashuhuda Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora alitoa tamko tukiwa humu ndani ya Bunge kwamba kama kuna eneo lolote Mbunge anajua kwamba kituo kimefungwa kwa sababu ya kukosekana watu wa kutoa huduma pale apeleke maombili ili isitokee hata sehemu moja eti tumefunga kituo kwa sababu hakuna mtu wa kutoa huduma ya afya kwa eneo husika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niendelee kuwasihii Waheshimiwa Wabunge kama kuna maeneo ambayo tumejenga na Mheshimiwa Bobali alisema jana, ni fursa hii tuhakikishe kwamba hakuna kituo cha afya hata kimoja au zahanati yetu hata moja ambayo inajengwa ikakamilika ikaacha kutumika eti kwa sababu hakuna watu wa kutoa huduma.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Rukia upande wa *CUF* nilikuona na Mheshimiwa Mlinga utakuwa wa mwisho kwenye eneo hili.

MHE. RUKIA AHMED KASSIM: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swalii la nyongeza. Kwa kuwa Hospitali ya Benjamin Mkapa ni kubwa, nzuri na ya kisasa ambayo inatumika kuwahudumia wananchi wa Dodoma, wanafunzi wa *UDOM* pamoja na sisi Wabunge, lakini ina tatizo kubwa sana la Madaktari pamoja na watumishi wengine. Je, ni lini Serikali itatatua tatizo hili? (*Makofii/Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Rukia unasema ina tatizo kubwa la Madaktari, wamefanyaje hao Madaktari, watoro kazini au? (*Makofii/Kicheko*)

MHE. RUKIA AHMED KASSIM: Mheshimiwa Spika, Madaktari ni kidogo sana.

SPIKA: Anazungumzia upungufu wa watenda kazi katika Hospitali ya Benjamin Mkapa.

Mheshimiwa Naibu Waziri Afya, Dokta Ndugulile, majibu, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambayo ndiyo mamlaka ya kusimamia Hospitali ya Benjamin Mkapa, inatambua kwamba tuna changamoto ya Madaktari Bingwa.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tumeweka mikakati ya kuainisha mahitaji ya Hospitali ya Benjamin Mkapa pamoja na Hospitali zote za Rufaa za Mikoa na tutafanya mgawanyo kwa kuangalia yale maeneo ambayo yana Madaktari wa ziada na kuwapeleka katika Hospitali zote za Rufaa za Mikoa, ikiwa pamoja na Hospitali ya Benjamin Mkapa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, katika mwaka huu wa fedha tumefadhili masomo ya Madaktari Bingwa 125 katika fani ambazo hatuna katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, ikiwa ni pamoja na Hospitali ya Benjamin Mkapa. Pindi Madaktari hao watakapomaliza watakuwa *posted* katika hospitali hizi.

SPIKA: Mheshimiwa Mlinga.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza naomba niishukuru Serikali kwa kuitupia sekta ya afya jicho la pekee katika Jimbo langu la Ulanga. Kituo cha Afya cha Lupilo karibu kinakwisha, sasa wananchi wa Ulanga wategemee nini katika huo mgawo? Siyo kwamba Madaktari ni wachache tu lakini ni pamoja na kuwa na watumishi wa afya wasio na sifa. Ulanga inakusikiliza sasa hivi Mheshimiwa Waziri.

SPIKA: Sidhani kama umeeleweka Mheshimiwa Mlinga, jaribu kuliweka sawa.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, Jimbo la Ulanga limepewa kipaumbele sana kwenye sekta ya afya, hilo naishukuru Serikali, hicho ndiyo kipaumbele cha Mbunge wao, kipaumbele cha kwanza afya, cha pili afya, cha tatu afya. Shida kubwa iliyopo ni watumishi wachache, Mheshimiwa Waziri katika majibu yake haya ya kugawa watumishi wa afya wananchi wa Ulanga wanamsikiliza sasa hivi anawaambia nini?

SPIKA: Alisimama Mheshimiwa Naibu Waziri, tuendelee Mheshimiwa Kandege, majibu tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nitangulie kupokea shukrani anazozitoa, lakini naomba nimhakikishie nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba vituo vyatya afya na zahanati zetu zote zinafanya kazi iliyokusudiwa kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi wetu.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, litakuwa ni jambo la ajabu tukamilishe kituo cha afya kizuri halafu kisiwe na watenda kazi. Katika wilaya ambazo zitapata watendaji kwa maana ya wahudumu wa afya pamoja na Waganga, nimhakikishie kwamba wale wenye sifa ndiyo ambao watapelekwa kwake, kwa hiyo, wananchi wategemee mambo mazuri kuhusiana na suala zima la afya.

SPIKA: Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, bado tuko TAMISEMI hapo hapo lakini swali la Mheshimiwa Mbunge wa Rungwe, Mheshimiwa Saul Henry Amon.

Na. 65

Barabara ya Pakati Hadi Mpakani

MHE. SAUL H. AMON aliuliza:-

Barabara ya Pakati – Njugilo – Masukulu – Matwebe hadi mpakani ni barabara kubwa na inapita katika Kata nne ambazo ni Masoko, Bujela, Masukulu na Matwebe, barabara hii ilishapandishwa daraja na kuwa ya *TANROADS*:

Je, ni lini barabara hii itaanza kujengwa ili kuondoa adha kwa wananchi kwa kupoteza kipato kwa mazao kuharibika njiani?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saul Henry Amon, Mbunge wa Jimbo la Rungwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Pakati – Njugilo – Masukulu hadi Mpakani mwa Wilaya ya Rungwe na Kyela yenye urefu wa kilometra 24.5 ni barabara ya wilaya. Katika kikao cha Bodi ya Barabara ya Mkoza Muhtasari Na.2016/2017/01 cha tarehe 6/12/2016, kilipendekeza ipandishwe hadhi na kuwa barabara ya mkoza. Baada ya mapendekezo kupelekwa

Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, barabara hiyo iliihdinishwa na kupandishwa hadhi kwa urefu wa kilometa 4.4 kutoka Njugilo hadi Masukulu katika Wilaya ya Kyela.

Mheshimiwa Spika, matengenezo ya barabara hii yanatarajia kuanza Agosti 2018, kufuatia kuwekwa kwenye Mpango wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Barabara za Vijijini kupitia ufadhilli wa watu wa Marekani (*USAID*), chini ya programu ya *Irrigation and Rural Roads Infrastructure Project – IRRIP II* ambapo kwa sasa zipo kwenye hatua ya usanifu.

SPIKA: Mheshimiwa Saul Amon, Mbunge wa Rungwe, swali la nyongeza tafadhali.

MHE. SAUL H. AMON: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Naomba kama Naibu Waziri ana nafasi aone hali ilivyo mbaya, kile kipande cha kata nne hata kwenda kuwasalimia tunaogopa kwa sababu tunatoa ahadi lakini haitimizwi. Je, yuko tayari kuongozana na mimi akaangalie hali ilivyo mbaya ya hicho kipande cha kutoka Njiapanda mpaka Mpakani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, vilevile barabara hii iko sawa kabisa na barabara ya Igogwe – Mchangani - Mbeye One. Mazao ni mengi lakini wananchi wa eneo hilo wanauzu mazao kwa bei ya chini sana kwa sababu hakuna usafiri. Naomba Waziri atakapokuja Rungwe aangalie vipande hivyo viwili na aone ukweli na hali halisi ilivyo kwa wananchi wa Rungwe. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, kubwa ambalo Mheshimiwa Mbunge analitaka kwangu mimi ni suala la kupata fursa ya kwenda kutembelea ili njionee kwa macho hali halisi ikoje. Mimi niko tayari baada ya kwamba tumehitimisha shughuli za Bunge la Bajeti,

nikiamini kwamba bajeti yetu itakuwa imepita salama ili nikajionee na tushauriane.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwa kupitia chombo chetu cha TARURA ambacho tumekianzisha tutahakikisha tunawaelekeza maeneo yote ambayo ni korofi yaweze kutengenezwa ili yapitike vipindi vyote.

SPIKA: Ahsante sana. Niliwaona Mheshimiwa Deo Sanga, Mheshimiwa Gekul na Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Barabara ya kutoka Ilunda - Igongolo yenye kilometra tisa ni ya *TANROADS*na imetengenezwa lakini mbele inaendelea kwenda Kivitu – Kifumbe – Makambako urefu wa kilometra 19 na tuliomba ipandishwe hadhi. Ni lini Serikali itaipandisha hadhi barabara hii kuwa ya *TANROADS* ili itengenezwe iweze kuzunguka kama ambavyo imefanyika kwa zile kilometra 9?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, sisi sote ni mashuhuda tukiwa katika Bunge lako Tukufu Wabunge wengi walikuwa wakiomba barabara zao zipandishwe hadhi na zichukuliwe na *TANROADS*. Mawazo hayo Bunge lako Tukufu likachukua na kulifanya kazi kwa nini Wabunge wengi tumekuwa tukiomba barabara zichukuliwe na *TANROADS*?

Mheshimiwa Spika, jibu ni jepesi kabisa kwamba kwa sababu barabara ambazo ziko chini ya *TANROADS* zimekuwa zikitengenezwa kwa kiwango kizuri. Ndiyo maana tukasema tuanzishe chombo ambacho kitakuwa kinafanya kazi nzuri kama *TANROADS* wanavyofanya na ndiyo *essence* ya kuanzishwa kwa TARURA.

Mheshimiwa Spika, naomba tutoe fursa kwa chombo hiki ambacho tumekianzisha ndani ya Bunge lako kifanye kazi. Naamini kinafanya kazi nzuri kwa sababu tumeanza kupata taarifa kutoka kwa baadhi ya Wabunge, wengi wana-appreciate jinsi ambavyo *TARURA* imeanza kufanya kazi. Naamini hata Mheshimiwa Mbunge kilio chake si barabara kuchukuliwa na *TANROADS* bali barabara itengenezwe ipitike kwa vipindi vyote.

SPIKA: Mheshimiwa Gekul nilikuona na Mheshimiwa Magdalena Sakaya jiandae.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swalii moja la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri mapema mwaka huu alifanya ziara katika Halmashauri yetu ya Mji wa Babati nasi tukakueleza juu ya ahadi ya Mheshimiwa Rais kuhusu ujenzi wa barabara za lami kilometra 20 alizoaohidi wakati wa kampeni. Wananchi wa Babati wanaauliza ni lini ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kilometra 20 za lami katika Mji wao wa Babati utaanza?

SPIKA: Loh jamani, Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali, kama unaweza ukalikumbuka hilo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, ni kweli nilipata fursa ya kutembelea Babati, lakini pia katika ziara yangu sikumbuki kama Mheshimiwa Gekul alisema hilo. Hata hivyo, kwa sababu ni ahadi ya Mheshimiwa Rais na ahadi zake ni mkataba baina yake yeye na wapiga kura na mkataba huu ni ndani ya miaka mitano, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, yale yote ambayo yameahidiwa na Mheshimiwa Rais yanaratibiwa na ndani ya miaka mitano yataweza kutekelezwa.

SPIKA: Mheshimiwa Magdalena Sakaya, tafadhali.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii muhimu sana. Kutokana

na mvua ambazo zinaendelea kunyesha barabara nyingi za Jimbo la Kaliuwa zimekatika na hazipitiki kabisa, zikiwemo barabara ambazo zinatoa magari Kahama kwenda Kaliuwa na kwenda vijiji mbalimbali. Barabara ya Kahama kwenda Ugaza imekatika, Kahama kwenda Usinge imekatika, Usinge kwenda Lugange Mtoni imekatika na Kahama kwenda Mpanda Mloka imekatika.

Mheshimiwa Spika, *TARURA* waliomba bajeti ya dharura ili waweze kufungua barabara hizi ambazo sasa hivi hazipitiki kabisa, wananchi wametengeneza mitumbwi ya kupita. Naomba Serikali ituambie mpango wa haraka wa kuweza kuwapa fedha kwa *TARURA*, Wilaya ya Kaliuwa ili waweze kutengeneza barabara hizi ziweze kupitika kwa sababu ni barabara kubwa za uchumi?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo. Vumilia Mheshimiwa, ukishakuwa TAMISEMI basi ujue moja ya kazi kubwa uliyonayo ni kujibu maswali Bungeni. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kuhusu suala la barabara nyingi kukatika kwa sababu ya mvua zinazonesha, naomba nimhakikishie na itakuwa vizuri mimi nikishatoka baada ya hapa tukafanya mawasiliano ili tuhakikishe haraka kabisa barabara hizo zinatengenezwa ili ziweze kupitika. Kwa sababu ni lengo la Serikali kuhakikisha kwamba barabara zote zinapitika kwa vipindi vyote.

Mheshimiwa Spika, ametaja barabara nyingi, itapendeza kama tutawasiliana halafu tuone jambo gani la haraka linaweza likafanyika ili wananchi wasije wakakwama katika shughuli zao.

SPIKA: Swali la mwisho kwenye eneo hilo, nilikuona Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro.

MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Tatizo la barabara katika Jimbo la Songea Mjini hususan barabara itokayo Songea Mjini kupita Kata ya Ruvuma na Kata ya Subira ni kubwa sana kiasi kwamba haipitiki na hata mimi Februari hii nilikwama wakati natumia barabara hiyo. Je, Mheshimiwa Waziri ni lini barabara hiyo itaweza kutengenezwa kwa kiwango cha lami ili kuwahudumia wananchi wa Jimbo la Songea Mjini? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Kandege, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, ni lini barabara hiyo itaweza kutengenezwa kwa kiwango cha lami, najua kiu yake kubwa angetamani hata kesho barabara ikakamilika, lakini ni ukwelli usiopingika kwamba kutengeneza barabara kwa kiwango cha lami inahitaji pesa za kutosha.

Mheshimiwa Spika, hivyo, ni vizuri katika vipaumbele vya halmashauri yake na katika vyanzo vya mapato walivyonyavyo wakaweka kama ni kipaumbele. Pia ni vizuri nkipata fursa wakati nikiwa katika ziara kwenda Ruvuma nitapita ili tushauriane na Mheshimiwa Mbunge tukiwa *site* ili tuone umuhimu wa barabara hii.

SPIKA: Ahsante. Sasa tuvuke twende Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, swali linaulizwa na Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, Mbunge wa Wingwi.

Na. 66

Nafasi ya Zanzibar katika Jumuiya za Kimataifa

MHE. JUMA KOMBO HAMAD aliuliza:-

Je, Zanzibar ina nafasi gani katika Jumuiya za Kimataifa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO
WA AFRIKA MASHARIKI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, Mbunge wa Wingwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na mabadiliko yake, masuala ya Mambo ya Nje yapo chini ya mamlaka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikihakikisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inashiriki kikamilifu kwenye masuala yote ya kimataifa. Masuala hayo ni pamoja na ziara za viongozi na mashirika mbalimbali ya kimataifa zinazofanyika nchini, ziara zinazofanywa na viongozi wa Kitaifa kwenye nchi mbalimbali, mikutano ya mashirika na Taasisi za Kimataifa na Kikanda na mikutano ya pande mbili (*bilateral*) na Zanzibar kuwa mwenyeji wa mikutano na makongamano ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, aidha, viongozi mbalimbali wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wamekuwa wakiongoza ujumbe wa nchi kwenye mikutano mbalimbali ya kimataifa. Kwa mfano kwa mwaka 2017/2018, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshiriki katika mikutano ipatayo 11 ya mashirika na taasisi mbalimbali za kimataifa; imeshiriki katika ziara nne za viongozi mbalimbali wa mashirika na taasisi waliofanya ziara hapa nchini; imekuwa mwenyeji wa mikutano na warsha zilizosimamiwa na mashirika ya Umoja wa Mataifa pamoja na kunufaika na miradi ya miundombinu, afya, kilimo na maji safi inayofadhiliwa na mashirika ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, miradi hiyo ni kama vile ujenzi wa barabara mbalimbali zikiwemo barabara za Mahonda - Mkokotoni Kilomita 31, Fuoni-Kimbeni Kilomita 8.6, Pale - Kiongole Kilomita 4.6 na Matemwe - Muyuni Kilomita 7.6 inayotekelizwa chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya

Afrika. Kadhalika, Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Chakula na Kilimo (*FAO*), linatekeleza miradi mbalimbali ya kilimo na lishe Zanzibar, ukiwemo mradi wa *aquaculture*.

SPIKA: Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, Mbunge wa Wingwi, swali la nyongeza.

MHE. JUMA KOMBO HAMAD: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba sasa nimuulize Mheshimiwa Waziri maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni miaka 20 sasa toka pale ambapo Zanzibar ilitakiwa ijiondoe kwenye Jumuiya hii ya *OIC*. Zanzibar ilijiunga na Jumuiya ya *OIC* kwa maslahi ya kiuchumi na si siasa wala siyo dini kama vile wengine walitafsiri katika kipindi hicho. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, je, sasa kwa sababu Tanzania kwa miaka 20 imeshindwa kujiunga kama ilivyoahidi ipo tayari kutoa ruhusa kwamba Zanzibar ina haki ya kujiunga na taasisi hii? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Waziri ametaja miradi mingi na ameenda mbali lakini nataka kuona tu kwamba kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Tanzania, anionyeshe kwa Ibara kwamba Zanzibar ina nafasi hii ndani ya Jumuiya za Kimataifa lakini ye ye kazungumza masuala mengine ambapo na mimi nitaelekeza nguvu zangu huko huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kataja miradi hapa, miradi hii kwa bahati mbaya au nzuri yote imetekelawa upande mmoja wa Kisiwa cha Unguja, si vibaya yote ni Zanzibar, lakini katika ahadi ambayo imekuwa ikiwekwa kila bajeti ni upanuzi wa uwanja wa ndege wa Pemba pamoja na bandari ya Mkoani Pemba. Naomba Mheshimiwa Waziri anieleze ni lini sasa bandari hii na huu uwanja wa ndege kupitia Jumuiya hizi za Kimataifa utakelezwa na itapanuliwa kama walivyoahidi?

Mheshimiwa Spika, nashukuru. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Hilo la pili nalikataa, haliendani, maana swali lako msingi wake ni ndani ya Katiba, sidhani kama uwanja huo uko kwenye Katiba, kwa hiyo, tujikite huko huko ulikokuwa umeuliza swali lako wewe.

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali la kwanza tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO

WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, anasema kwamba kwa miaka 20 Zanzibar imejiondoa katika kuijunga na ile Jumuiya ya Kiislam na kwamba sisi kama Tanzania iko tayari kuiruhusu Zanzibara kuijunga na taasisi hiyo? Jibu langu nasema bado liko vilevile kama lilivyojadiliwa katika Bunge hili katika siku za nyuma na maamuzi yaliyofanyika siku za nyuma kwamba kama ni faida bado Tanzania ikiwemo Zanzibar inaweza ikafaidika tu kwa mahusiano yaliko baina yetu na nchi ambazo ni wanachama katika Jumuiya hiyo hiyo ya Kiislam.

Mheshimiwa Spika, kama anavyojua kwenye Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania suala la dini tumesema kwamba si suala ambalo tunataka tulijadili au kujihuisha na kuweza kuweka utenganishi kati ya sehemu ya nchi na nchi nyingine. Kwa hiyo, bado msimamo uko pale pale kwamba sisi kama Tanzania hatujakubaliana kwamba Zanzibar ijiunge na taasisi hiyo. Hata hivyo, faida za taasisi hiyo bado tunaweza kufaidika nazo kwa kufanya mikataba baina sisi kama Tanzania au upande wa Zanzibar kushirikiana na nchi hiyo kwa kufanya *bilaterals*. (*Makofii*)

SPIKA: Nimewaona Mheshimiwa Maryam Msabaha na Mheshimiwa Khatib maswali ya nyongeza, tuanze na Mheshimiwa Maryam.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niulize swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri kumekuwa na malalamiko nafasi nyingi za Balozi Wazanzibari wengi wanapelekwa nchi

za Kiarabu. Je, kama malalamiko haya ni kweli hamuoni kama sasa kuna umuhimu wa kufanya uwiano sawa ili Wazanzibari wengi wasipelekwe nchi za Kiarabu nao wapelekwe nchi hizi nyingine kama Marekani, Ulaya na kwingineko?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, Mheshimiwa Dkt. Susan Kolimba.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maryam Msabaha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, anasema kwa siku nyingi sana wamekuwa wakilalamika kwamba Watanzania ambao wanatoka Zanzibar wanapoteuliwa kuwa Mabalozi wanapelekwa kwenye nchi za Kiarabu zaidi. Naomba niweke taarifa hii sawa kwamba tunapowateua Mabalozi tunawateua kwa kigezo cha weledi, ufahamu wao na uwezo wao wa kushika nafasi hiyo ya kiubalozi. Tunapowateua kuwapeleka mahali popote iwe ni kwenye nchi za Kiarabu, Afrika, Ulaya au Latin America wako sawa kabisa kwa *status*.

Mheshimiwa Spika, nimwambie tu siyo tu kwamba katika hizi nchi za Kiarabu wako Watanzania ambao wanatoka Zanzibar yaani Mabolozi ambao wanatoka Zanzibar tu wapo pia wameteuliwa na wamekwenda huko wanatoka pia Tanzania Bara. Naomba hisia hizo za kusema kwamba tunawapeleka Mabalozi kwenye nchi za Kiarabu wale tu ambao wanaotoka Zanzibar zitolewe.

Mheshimiwa Spika, vilevile niseme tu kwamba sisi tunapowapeleka Mabalozi mahali popote iwe nchi za Kiarabu, tunaangalia pia *additional value* ambayo anaweza akaifanya. Sisi tunapowapima wale ambao pengine wanatoka Zanzibar au Bara tunajua kabisa kwamba kwa kufanya kazi kule watasimamia maslahi ya Taifa na maslahi wa nchi hii kwa ujumla wake.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, wako Watanzania Mabalozi ambao wanatoka Tanzania Bara wameteuliwa hivi karibuni na wamekwenda kule. Nafasi hiyo itaendelea kufanya hivyo na wale wanaotoka Zanzibar na wao ikifika wakati tunaweza tukawachukua tukawapeleka sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba hakuna upendeleo wala dharau kwamba wanapopelekwa kwenye nchi za Kiarabu maana yake kwamba tumewaonea na wanafanya kazi nzuri. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Maryam Msabaha hilo lina shida gani mbona huko Uarabuni kuzuri sana huko. Mheshimiwa Khatib. (*Kicheko*)

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki imekuwepo ahadi ya muda mrefu ya upanuzi wa uwanja wa ndege wa Chake Chake Pemba na upanuzi wa Bandari ya Wete Kaskazini Pemba.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge hili jambo hili limekuwa likiahidiwa kupitia bajeti zilizotangulia lakini ni muda mrefu wananchi wa Pemba wamekuwa na hamu ya kuona miradi hii inatekelezwa lakini hakuna kilichoendelea hadi sasa. Je, Mheshimiwa Waziri ni kipi kinachokwamisha kukamilisha miradi hii ambayo wananchi wa Pemba wanaishubiri kwa hamu kubwa?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Hilo swali nilishalikataa tangu mwanzo aliuliza Mheshimiwa Juma Kombo Hamad mtalipeleka Wizara ya Uchukuzi itakapokuja liweze kujibiwa.

Mheshimiwa Jaku nilikuona kwa swali la mwisho eneo hili.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Spika, nami nikushukuru kwa kuniona. Mheshimiwa Naibu Waziri

alipokuwa akijibu swalii la msingi hapa alitaja Balozi, sasa nataka kujua Balozi zote za Tanzania duniani ziko ngapi na Zanzibar wamegaiwa ngapi?

SPIKA: Mheshimiwa Jaku maswali ya nyongeza yanapokuwa ya takwimu ya ghafla lakini Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, Balozi za Tanzania ziko 40 na Mabalozi wanaotoka Zanzibar wako tisa na hiyo ni asilimia 22.5 ya Mabalozi wote walioopo. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa tuhamie Wizara ya Kilimo, swalii linaulizwa na Mbunge wa Urambo, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta.

Na. 67

Matatizo yanayowakibili Wakulima wa Tumbaku

MHE. MARGARET S. SITTA aliuliza:-

Pamoja na kuishukuru Serikali kwa hatua mbalimbali zilizochukuliwa katika kumwondolea mkulima matatizo ya zao la tumbaku:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua zipo katika kuimarisha utendaji kazi wa Bodii mpya ya Tumbaku ili ifanye kazi kikamilifu?

(b) Je, Serikali inawahakikishiaje wakulima wa tumbaku upatikanaji wa mbolea kwa wakati?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Jimbo la Urambo, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(a) Mheshimiwa Spika, Bodi ya Wakurugenzi wa Bodi ya Tumbaku Tanzania ilizinduliwa rasmi tarehe Mosi Disemba, 2017. Ili kuimarisha utendaji kazi wake kikamilifu, Serikali imeagiza kuwa tumbaku iendelee kuwa miongozi mwa mazao mkuu yanayowanufaisha wakulima ili kuliingizia Taifa fedha za kigeni kwa kuhakikisha kuwa ubora wa tumbaku unaongezeka kwa asilimia 15 ifikapo mwaka 2021 na uzalishaji wake kufikia tani laki moja na ishirini kutoka tani elfu sitini na tatu za sasa.

Mheshimiwa Spika, tumbaku inazalishwa kwa mujibu wa sheria na taratibu na wakulima wanazalisha kwa mkataba ili kuwa na soko la uhakika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tumbaku ni moja ya zao la kimkakati, Bodi imelekezwa kuyataka makampuni ya ununuzi kufanga mikataba na Bodi ya Tumbaku Tanzania na kisha kuyapangia maeneo ya kwenda kununua badala ya utaratibu wa sasa ambapo makampuni hujichagulia maeneo ya kwenda kununua.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ni kutafiti na kubaini aina nzuri za tumbaku zinazopendwa na wanunuzi ili zilimwe na kuwauzia wanunuzi wa aina hizo za tumbaku; kuwachukulia hatua za kinidhani watendaji wasiowajibika kikamilifu na kufuata vizuri kalenda ya uzalishaji wa tumbaku.

(b) Mheshimiwa Spika, katika msimu wa mwaka wa 2017/2018, mbolea ya tumbaku ilichelewa kutokana na kuchelewa kwa maafikiano ya bei ya kununulia tumbaku ambayo ni kigezo kwa kila kampuni kuahidi kiasi cha tumbaku itakachonunua na hivyo kubaini kiasi cha mbolea itakayotumika kuzalisha kiasi hicho cha tumbaku.

Mheshimiwa Spika, ili mbolea ianze kuagizwa maafikiano ya bei yanatakiwa kukamilika kati ya Machi na Mei kila mwaka. Katika msimu wa kilimo wa 2018/2019, Bodi ya Tumbaku Tanzania inaendelea kuratibu majadiliano ya bei kati ya wanunuzi na wakulima ili uagizaji wa mbolea ufanyike mapema. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta swalii la nyongeza.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niulize maswali ya nyongeza, lakini kabla sijafanya hivyo, kwa ruhusa yako, kwanza naomba nichukue nafasi kwa niaba ya wananchi wa Urambo kuishukuru Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa kupitia Ofisi yake ya Rais, Manejimenti ya Utumishi kwa kauli aliyoitoa hivi karibuni, Mheshimiwa George Mkuchika, Waziri Mhusika, ya kuwarudisha kazini Watendaji wa Vijiji na Madereva waliokuwa wameachishwa kazi kutokana na elimu yao ya darasa la saba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuwarudisha kazini na kuamrisha walipwe mishahara yao yote ambayo wameikosa katika kipindi walichokuwa wamesimamishwa ni ishara na ushahidi tosha kwamba Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi ni sikivu. Tunaiomba Serikali yetu iendelee kuwasikiliza wanyonge na kuwatengenezea yale ambayo wanaona hayakwenda sawa. Ahsante sana Serikali ya Awamu ya Tano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyotoa lakini pia kuishukuru Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na Waziri Mkuu mwenyewe kwa kuunda Bodi ya Tumbaku mpya ambayo imeanza kazi vizuri. Ombi langu tu kwa Serikali ni kuiwezesha kwa kuipa vifaa zaidi kama komputa na kadhalika, lakini pia ateuliwe Mwenyekiti ambaye naamini atakuwa ana uzoefu na zao la tumbaku.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swalii la kwanza, kwa muda mrefu Serikali imekuwa ikiombwa na wakulima wa tumbaku kutafuta wanunuzi zaidi wa tumbaku ili walime tumbaku zaidi lakini pia ilete ushindani wa bei ili mkulima wa tumbaku anufaiki na zao lake, nataka kujua suala hili limefikia wapi?

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Serikali haiwezi kuagiza mbolea kwa wingi hasa *NPK* ili mbolea hiyo iwafikie wakulima mapema kuliko kama ilivyokuwa kipindi kilichopita?

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajiandaa kutoa majibu ya swali hilo, Waheshimiwa Wabunge niwape taarifa kwamba kwa wakati huu, tulishawatangazieni kwamba Bunge la Afrika Mashariki (*EALA*) - *East African Legislative Assembly* litakuwa likiendesha mikutano yake hapa katika Ukumbi wa Msekwa katika kipindi hiki cha karibuni, ambapo tutawaomba Waheshimiwa Wabunge wakati kwa wakati tuweze kufika hapo na watakuwa na sheria mbili watakazokuwa wanashughulika nazo tuweze kuona Bunge hilo linafanyaje kazi na pia wawakilishi wetu wanafanyaje kazi. (*Makofi*)

Kwa vile wao nao wanashughuli zao na zinaenda kwa muda, leo ni wageni wetu hapa naomba niwatambulische ili tuisiwazuie hapa waende wakaendelee na shughuli zao na baada ya hapo tutaendelea na maswali kama ilivyo. Kwa jinsi hiyo ningependa kuwatambulisha wageni hao ambaa wapo Jukwaa la Spika, kama ifuatavyo:-

Ni Wabunge wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki wakiwemo Mawaziri pamoja na Sekretarieti ya Bunge hilo wakiongozwa na Mheshimiwa Ngoga Martin, Spika wa Bunge la Jumuiya Afrika Mashariki. Karibu sana Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki, huyu Spika anatoka nchi ya Rwanda lakini ni mzaliwa wa hapa hapa Tanzania. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika ameambatana na Wabunge wa Bunge hilo ambaa ni Wabunge wa kutoka nchi ya Burundi. Naomba Wabunge wa Burundi wote msimame. Karibuni sana Wabunge kutoka Burundi tunatumaini Bujumbura hawajambo. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Niwatambulisse Wabunge kutoka nchi ya Kenya, wote kwa wakati mmoja msimame. Ahsanteni sana majirani wetu wa Kenya. (*Makofi*)

Tunao Wabunge kutoka nchi ya Rwanda. Naomba wote msimame. Ahsanteni sana. Tunatumaini Kigali ni kwema. (*Makofi*)

Pia tuna Wabunge kutoka Sudani ya Kusini (*South Sudan*). Hawa ndio wamejunga kwenye shughuli hizi hivi karibuni, kwa hiyo, tunawakaribisheni sana katika mchakato huu wa Afrika Mashariki. Karibuni sana Wabunge wetu kutoka Juba. (*Makofi*)

Tuna Wabunge majirani kutoka kule Uganda, naomba msimame. Karibuni sana Wabunge wote kutoka Uganda, karibuni sana toka Kampala kule. (*Makofi*)

Mwisho siyo kwa umuhimu, tuna Wabunge wenyeji wa kutoka Tanzania. Ahsanteni sana Wabunge wetu kutoka Tanzania. Tunayo matumaini makubwa sana kupitia kwenu na kama nilivyosema Wabunge wetu watakuja kuangalia mnafanyaje mambo yenu huko. (*Makofi*)

Kwa upande wa Baraza la Mawaziri la Bunge hilo, tunaye Mheshimiwa Dkt. Susan Kolimba ambaye yuko humu ndani, naye ni sehemu ya chombo hicho. (*Makofi*)

Wageni wengine ni Sekretarieti ya *EALA* wakiongozwa na Kenneth Madele ambaye ni Katibu wa Bunge. Ahsante sana. (*Makofi*)

Ahsanteni na karibuni sana, tutakuwa pamoja katika siku ambazo mtakuwa hapa na tunajivuna sana kwamba kwa mara ya kwanza Bunge la Afrika Mashariki litafanya vikao vyake hapa Dodoma na katika eneo letu la Bunge. Tutawapa kila ushirikiano na kama mnahitaji jambo lolote tafadhalii tuweze kuwasiliana na kwa pamoja tutahakikisha shughuli yenu inaenda vizuri na inakwisha salama kabisa, ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, karibu Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa kutoa majibu ya maswali ya Mheshimiwa Margaret Sitta.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mama yangu Mwalimu Margaret Simwanza Sitta kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia suala hili la zao la tumbaku kule Tabora na Tanzania nzima kwa muda mrefu kuhakikisha kwamba zao hili linakuwa na tija. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nikija katika maswali yake mawili ya nyongeza ni kweli kabisa Bodi ya Tumbaku haina Bodi ya Wakurugenzi lakini imezinduliwa Disemba, 2017 na sasa hivi tunakaimu Mwenyekiti, ni miezi mitatu tu tangu imezinduliwa. Kwa hiyo, tunaamini kabisa Mheshimiwa Rais akiridhia kuteua Mwenyekiti basi na Bodi hii itaongeza tija katika utendaji wake wa kazi.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye swali lake hilohilo la nyongeza kuhusu *ku-monopolize* hii biashara ya tumbaku ni kwamba kama Serikali sasa hivi tuna makampuni manne tu ambayo yananunua tumbaku lakini tuko kwenye majadiliano na Zimbabwe, Misri, China na Vietnam. Vilevile Serikali ya Indonesia kupitia Kampuni ya *Star International* wao wameshakubali pia kununua tumbaku yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nikija katika swali lake la pili kuhusu ununuzi wa mbolea kwa pamoja, sisi kama Serikali tuna mbolea ya *DAP* pamoja na *UREA* ambayo yenye we ndiyo iko katika mfumo ule wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja, *NPK* haiko katika mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naomba niliarifu Bunge lako Tukufu na Mheshimiwa Mbunge kwamba mbolea hii ya *NPK* ambayo inatumika sana katika zao la tumbaku pia tunalichukua suala lake tutalifanyia kazi na hasa ukizingatia kwamba mbolea ya *NPK* mwaka jana ilitumika tu asilimia 21 ukilinganisha na ile ya *UREA* ambayo ilitumika

asilimia 46. Kwa hiyo, wazo lako Mheshimiwa Mbunge ni zuri tunalipokea ili kuhakikisha kwamba mbolea inafika kwa wakulima kwa msimu.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawaona kwa wingi huu, lakini mkiangalia muda wetu kule mtaona kwamba muda wa maswali umeisha tuvumiliane tuweze kuendelea na shughuli zetu.

Waheshimiwa Wabunge, nina mambo muhimu naomba tusikilizane vizuri, tupunguze sauti kidogo. Kwanza mliona leo ilikuwa tuwe na kipindi cha maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu lakini hakikuwepo, nieleze tu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu amesafiri, jana alikuwa Lindi na Dar es Salaam na leo atakuwa Arusha. Kwa hiyo, shughuli za Serikali hapa Bungeni zitaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, Waziri wa Ulinzi ambaye yuko pale. Mheshimiwa Dkt. Hussein tunakutakia kila la heri na tuko pamoja, ahsante sana. (*Makofi*)

Nimalizie matangazo ili twende kwenye mambo mengine. Kuna wageni wanne wa Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) kutoka Kanisa la Baptist Tanzania ni Askofu Anord Manase, Askofu Mkuu wa Dhehebu la *Baptist* Tanzania. Karibu sana Baba Askofu, msisahau kutuombea.

Ameantuana na Askofu Michael Nhonya, Askofu Mkuu Msaidizi wa dhehebu hilo la Baptist. Ahsante sana Michael Nhonya, wewe kwa jina lako hilo kwa vyovyote vile unatoka Dodoma hapa hapa.

Wengine ni Mchungaji Mperi James na Mchungaji Anthony Saimon Mlyashimba. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Ally Keissy amba ni rafiki zake kutoka

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Ngorongoro, Mkoani Manyara. Karibuni sana, huu ndiyo umoja wa kitaifa huu kutoka Namanyere hadi Ngorongoro. (*Makofi/Kicheko*)

Wageni tisa wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu kutoka Chuo cha Ualimu Mpwapwa wakiongozwa na Ndugu Kasanda Japitati. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Maria Kangoye ambaao ni wanachama wa CCM Tawi la *UDOM* wakiongozwa na Ndugu Simon Malando. Karibuni sana popote pale mlipo. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Shaabani Shekilindi ambaao ni ndugu zake kutoka Dar es Salaam. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni 35 wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambaao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Kilolo, Mkoani Iringa. Karibuni sana wajomba na mashangazi. (*Makofi*)

Wageni 22 wa Mheshimiwa Mwita Waitara ambaao ni Wanakwaya wa Vijana Parokia ya Ukonga Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Happines Mkaanga. Karibuni sana Wanakwaya. Baadaye huko nje tutataka mpige *tune* kidogo tuwasikie. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Pascal Haonga ambaao ni wapiga kura wake kutoka Mlowo, Wilayani Mbozi, Mkoani Mbeya. Ahsante. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Esther Matiko ambaao ni viongozi wa Jukwaa la Mwanamke kutoka Dar es Salaam na Tarime. Jukwaa hilo limeandaa kongamano la wanawake Kanda ya Afrika Mashariki na Kati litakalofanyika Tarime Mkoani Mara ambalo litahusu kupambana na ukatili wa kijinsia. Pia jukwaa hilo litapambana na ukeketaji na mambo yanayofanana na hayo. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Wageni 57 wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Iringa wakiongozwa na Ndugu Gildaph Kissi. Karibuni sana wageni kutoka Iringa. (*Makofii*)

Waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 80 na Walimu 10 kutoka Shule ya Msingi Mayamaya iliyoko Mkoa wa Dodoma. Watoto wa Mayamaya hao, karibuni sana. Msiojua Mayamaya ilipo ni barabara ya kuelekea Arusha kutokea Dodoma kabla ya kufika Kondoa. Karibuni sana watoto, mnapendeza kwelikweli. (*Makofii*)

Wanafunzi 30 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wanaosoma Sayansi Asilia na Hisabati (*Natural Sciences and Mathematics*). Karibuni sana. (*Makofii*)

Wanafunzi wengine wote wa Chuo Kikuu cha Dodoma mliopo simameni, ahsante na karibuni sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo ya wageni nina yafuatayo ambayo ningependa kuyaeleza. Kama nilivyo sema, naomba tusikilizane na hasa upande wa chama tawala. Tusikilizane Waheshimiwa, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi tusikilizane, najua jana Yanga walishindwa kuifunga *Singida United* lakini tusikilizane kidogo. Walifikiri tatizo ni Kocha lakini kumbe siyo jamani, Yanga wana shida kweli. (*Makofii/Kicheko*)

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kuna mwongozo ambao uliombwa na Mheshimiwa Goodluck Mlinga kuhusu Gazeti la Raia Mwema, Toleo la 556 la tarehe 9 na 10 Aprili, 2018, kuingilia haki, kinga na madaraka ya Bunge.

Kama mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mlinga aliomba mwongozo wa Spika tarehe 9

Aprilii, kuhusu makala iliyochapishwa katika gazeti la Raia Mwema. Alieleza kuwa makala hiyo ina maelezo yanayokashifu na kushusha hadhi ya Bunge na kwamba gazeti hilo linachonganisha Serikali na Bunge, pia linachonganisha Wabunge na wananchi.

Gazeti hilo la Raia Mwema Na./ISSN:1821-6250, Toleo la 556 la tarehe la tarehe 9 na 10 Aprili, 2018 lilichapisha kichwa cha habari kwa wino mzito kilichosomeka Bunge linajipendekeza? Habari hiyo iliandikwa kwa kirefu katika makala iliyoandikwa na Ndugu Pascal Mayala katika safu yake ya kwa maslahi ya Taifa yenye kichwa cha habari kifuatacho:- "Bunge linajipendekeza kwa Serikali?"

Katika makala hiyo, Mwandishi amekosoa hatua ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kukabidhi Serikalini Taarifa ya Mapendekezo ya Kamati Teule zilizoundwa na Spika kwa hoja ya kwamba matokeo ya kazi ya Kamati hizo ilitakiwa zipelekwe Bungeni zijadiliwe kisha Bunge litoe Azimio ambalo linapaswa kupelekwa Serikalini kwa hatua ya utekelezaji.

Alisema maneno mengi huyu Ndugu Pascal Mayala, pamoja na maneno aliyojasema alisema maneno haya:

"Kwa kweli wengi wa Wabunge wetu au baadhi ya Wabunge wetu ni Wabunge wa ajabu wasiojielewa au wasioelewa majukumu yao kwamba wameenda kufanya nini kule Bungeni. Baadhi ya hawa ni Wabunge wa posho, ulaji na wengine wako kule Bungeni kutoa tu huduma za kibinadamu, yaani hapo anaposema kutoa huduma za kibinadamu mnawenza mkaelewa na siyo kufanya kazi za Kibunge za kuwakilisha wananchi na kusimamia Serikali'.

Ndugu Pascal Mayala anaendelea, "kwa Bunge la kujipendekeza kama hili litakuwa na uwezo kweli wa kusimamia Serikali na kuiambia hapa mmekosea au itakapotokea Rais amevunja Katiba, Bunge la aina hii

litakuwa na uwezo wa kumuadhibu Rais na kumwondoa madarakani?" na mengine mengi ambayo sitakuwa na muda wa kuyafafanua sana au kuyaelezea.

Kwa bahati mbaya sana huyu mtu ni mtu ambaye hajui atendalo, anafikiri Spika ni mtu wa kucheza naye tu kirahisi hivi. Sijui kwa nini katika nchi yetu, yaani wewe mtu mmoja unajiona una akili sana, unaona watu wengine wote *as a group* ni *a bunch of fools*. Wewe Pascal Mayala wewe! Yaani, yaani, Watanzania hawa bwana ukisoma ka-degree kako hako unaona watu wote wajinga, hapa kuna watu wasomi kweli kweli hapa, kuna watu wazoefu kweli kweli, kuna watu wenye heshima zao hata kama unatofautiana iko namna ya kutofautiana na hii ndiyo shida kubwa. (*Makofi*)

Kwa maoni yangu hata kwenye mahusiano ya *opposition* na *ruling party*, hata kama wewe uko *opposition* kuna namna hata ukipanda jukwaa unaweza uka-*oppose* lakini ukianza kutukana wenzako, kuwafanya wenzako kama ni wanyamapori halafu ukaji-*cocoon* kwamba kwa sababu wewe ni mpinzani kwa hiyo una uhuru wa kubomoka tu, hatuwezi kuwa hivyo. Hata huko duniani siyo mantiki ya mfumo huo wala siyo uhuru wa vyombo vyaya habari kwa utaratibu huo. (*Makofi*)

Kwa hiyo huyu kwa kifupi nampeleka kwenye Kamati ya Maadili na Wahariri wa Gazeti hili la Raia Mwema pia. Niwaambie Wahariri wa magazeti mengine kuwa makini sana na kucheza Bunge, huu ni mhimili. Naiagiza Kamati ya Maadili kukaa kwa haraka sana kuwaita hawa niliyosema na tuweze kupata mrejesho wa nini kinaendelea. Hili halikubaliki kabisa. Ahsante sana. (*Makofi*)

Lingine, Mheshimiwa Saed Kubenea ameleta taarifa ofisini kwetu ya kusudio la kuwasilisha Hoja Binafsi Bungeni akitaka Bunge lifanye marekebisho ya masuala yanayohusiana na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (*NEC*) ili ikidhi matakwa ya mazingira ya mfumo wa vyama vingi hapa nchini. (*Makofi*)

Kwa kuwa Tume hiyo ya Taifa ya Uchaguzi imeanzishwa na Katiba katika Ibara ya 74 marekebisho yoyote dhidi ya Tume hiyo yanapaswa kuletwa kwa kupitia Muswada wa Marekebisho ya Katiba na siyo Hoja Binafsi ya Mbunge. Nafikiri naeleweka katika nachokisema. Unapoleta jambo ambalo linahusu Katiba basi uko utaratibu wake wa kufuata ili iendane na marekebisho yanayoendana na marekebisho ya Katiba na siyo tu hoja binafsi ya Mbunge *simply like that.*

Kwa hiyo, kwa kuwa Kanuni ya 55(1) ya Kanuni za Bunge imenipa madaraka ya kukataa hoja inayovunja Katiba, Sheria na Kanuni za Bunge, taarifa yako Mheshimiwa Kubenea naikataa. Kwa hiyo, ukajipange tena kama bado una nia hiyo ili uje katika utaratibu unaotakiwa. Kama hatukukuelewa, basi tafuta muda tuweze kuonana utueleweshe vizuri zaidi, sisi tumeelewa hivyo. (*Makofii*)

Pia tumekuwa na shida kidogo kwenye jambo hili la taarifa za Wabunge kutuletea taarifa ofisini ya kwamba wanakusudia kuleta Hoja Binafsi halafu baadhi yao hata hiyo taarifa haijafika ofisini wameshaweka kwenye mtandao, hata Spika anaanza kuisoma kwenye mitandao na wanawachanganya wananchi, kwa sababu hatua ni mbili.

Hatua ya kwanza unaleta taarifa kwa Katibu wa Bunge, taarifa tu ya kusudio lako la kuleta Hoja Binafsi. Sasa ukileta taarifa una-publicize ya nini yaani unawaambia wananchi ili iweje? Sababu ile ni taarifa tu. Sawa tumepokea taarifa na tumewahi kupokea taarifa za Wabunge wengi.

Inatakiwa baada ya hiyo taarifa baadaye utuletee hoja yenewe sasa, maana ile taarifa ni barua tu ya kawaida ya ukurasa mmoja kwamba nataka kuleta taarifa yenye mambo moja, mbili, tatu, haina shida sawa tumepokea, sasa hoja yenewe iko wapi?

Kwa hiyo, wengi wamefanya hivyo wengi Mheshimiwa Bashe na wengine inaweza kuwa ni mjadala wa kitaifa na hivi na wananchi wengi wanaamini kwamba huyu amepeleka hoja Bungeni kumbe hakuna hoja, hoja iko wapi? Ndio ninyi mnafanya hawa wengine wanaandika Bunge hili wanafikiri kwamba labda kuna hoja imekaliwa, imekaliwa na nani, wapi hakuna hoja? (*Makofi*)

Sasa pamoja na kutaka umaarufu kidogo na nini lakini muwe mnasubiri kidogo, lete taarifa yako baadaye lete hoja yako halafu ukishaleta hoja yako utatangaza tu, mitandao si ipo, utatangaza tu hoja yako kwamba hili jambo lipo hivi. Kwa hiyo, mnatuweka mahali kidogo tunakuwa tunaeleweka na sisi hatupendi kila wakati kumjibu Mbunge kila wakati kwa kufanya kama huelewi unachokifanya lakini mnatuweka katika wakati mgumu. Ningombwa twende vizuri taratibu tutafika safari yetu.

La pili, mkumbuke kuna kanuni tatu zinazotumika hapa Bungeni, kuna kanuni ile ya uendeshaji wa Bunge au mambo ya Bunge ila ya ujumla lakini wapinzani mna kanuni yenu pia ya namna ya kufanya mambo yenu, CCM mna kanuni yenu pia kama kambi ya chama tawala. Kwa hiyo, unapoleta hoja binafsi angalia na kanuni ile ya kwenye kambi yako inasemaje. (*Makofi*)

Kwa Wabunge wa CCM kanuni yenu inasema lazima upeleke jambo lako hilo kwenye chama chako, kwa Katibu wa Wabunge wa CCM watajadili kama *caucus* ya hiyo hoja yako, halafu baadaye itakuja kwa Spika, itafika tu kama ni ya kufika, kama ni ya kufia huko itafia huko. hizo ni kanuni zenu hamjatungiwa na mtu mmejitungia ninyi wenyewe na sisi tunazitambua.

Pia upinzani hivyo hivyo, sio kwa maana hiyo ya CCM hapana lakini unapoleta hoja binafsi kwa ujumla ushauri wangu, ile hoja jina lake inaitwa hoja binafsi lakini haina maana kwamba wewe ubebe jambo lako binafsi, unakuja hapa Bungeni na jambo lako binafsi unategemea hilo binafsi litapita hapa. Bungeni ni lazima ufanye *lobbying* kubwa, kwa

hiyo, utaanza na *caucus* ya Wabunge wako, kama ni mpinzani angalau ukae na wenzio wote uwaeleze jamani mimi nina jambo hili nalionna ni zito, wenzako wakuunge mkono kwa sababu Bungeni lazima uungwe mkono na wengi ili jambo lako liende, ukienda tu binafsi utafika? Huwezi kufika, kwa hiyo, lazima ufanye *lobbying* kubwa, kabla hata ya kuleta hoja binafsi kama unajitakia mema, lazima uwe umefanya *lobbying* ya kutosha ukajiridhisha kwamba hapa sasa nimefika mahali pazuri, lakini binafsi tu itakuja hapa binafsi itapigwa chini. (*Makofi*)

Bungeni kote duniani wanafanya hivyo, unaanza na *lobbying*, uko *canteen* huko unakaa nao, unapokuwa na jambo lako binafsi halikufanyi binafsi, unakwenda kwa Wabunge wa chama tawala, Wabunge wa upinzani kwa sababu unataka jambo lako lipite Bungeni mwisho wa siku ili Spika atakapohoji uungwe mkono.

Waheshimiwa Wabunge, hivyo ndivyo Wabunge wanavyofanya kazi, hata kama jambo lenyewe ni binafsi lakini fanya kazi kubwa sana ya *lobbying*. Ukiona limeiva umepata *support* kubwa, ndio unalileta. (*Makofi*)

Nashukuru sana, kwa hatua hiyo Wahesimiwa Wabunge, naomba nimwite Mheshimiwa Andrew Chenge ili tuweze kuendelea na shughuli nyingine, Mheshimiwa Chenge tafadhali. (*Makofi*)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alikalia kitii

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wa Spika.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Haya.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Mniruhusu nikae vizuri, unataja jina lako, naanza upande huu. Asante tunao sita hawa, naanza na Mheshimiwa Shangazi.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Nimesimama kwa kanuni ya 68(7) na kwa faida ya muda naomba nisisome. Kanuni hii kama wenzangu wote wana vitabu wanaweza wakaisoma na inaeleweka vizuri lakini mara zote kanuni hii imekuwa inatumika vibaya kiasi kwamba Bunge linakuwa linapoteza muda mwingi kwa kujadili mambo ambayo sio yanayolingana na maudhui ya kanuni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wangu nilikuwa nataka kiti chako kituelekeze, hatuoni kwamba kanuni hii sisi wenyewe ambao tumeitunga na tunashindwa kuvisimamia na kufanya kwamba hatuna uendeshaji bora wa shughuli za Bunge? Naomba nipate mwongozo wa kiti chako.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Amina Mollel.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nasimama kwa kanuni hiyo hiyo ya 68(7), nazungumzia jambo ambalo limetokea leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel alipoulima swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusiana na baadhi ya Wakurugenzi ambao wanatumia nafasi zao vibaya kwa kuwabugudhi akinamama ambao tayari Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefuta ushuru kwao kwa bidhaa zile ndogo ndogo wanazofanya sokoni ambazo zinawawezesha kupata kipato na kuendesha maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Rais alishalizungumza hilo na mara nyingi amekuwa akilirudia na Wakurugenzi hawa baadhi yao bado wanaendeleza. Kwa

mfano tu, hapo jana Wilayani Siha katika Jimbo la Siha ambapo wengi pia kwa sababu tulikuwepo katika kampeni za uchaguzi wametupigia simu na kueleza jinsi ambavyo mtafaruku ulivyotokea katika soko la Siha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kauli kutoka kwa Serikali kwa kuwa jambo hili limekuwa likiendelea mara kwa mara. Kauli toka kwa Serikali ili na wale wengine ambao wamekuwa wakiendeleza tabia hiyo. Ni nini sasa kauli ya Serikali kwa Wakurugenzi hawa ambao baadhi ya kodii/ ushuru katika maeneo mengi hasa magulio na masoko umepigwa marufuku na Mheshimiwa Rais amekuwa akirudia mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako na hasa kwa Serikali.

MWENYEKITI: Ahsante. Naanza upande huu Mheshimiwa Haonga.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa kanuni ya 68(7), lakini kwa sababu ya muda sitawenza kuisoma. Kuna jambo limejitokeza leo mapema hapa Bungeni na naomba mwongozo wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maagizo yaliyotolewa hapa muda sio mrefu na kiti cha Spika kwa maana ya Spika kuhusu gazeti la Raia Mwema juu ya makala aliyokuwa ameandika Paschal Mayala la kuudhalilisha mhimili wa Bunge na uchochezi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako, yapo magazeti mengine ambayo yamekuwa yakifanya kazi ya uchochezi. Kwa mfano kuna gazeti linaitwa Jamvi, gazeti hili linatukana viongozi, mara nyingi limekuwa likichochea, hili gazeti hata mara moja hatujawahi kusikia hapa Bungeni likilalamikiwa na kupelekwa huko ambapo gazeti hili la Raia Mwema tumesikia linapelekwa kwenye Kamati ya Maadili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na gazeti hili lakini kuna gazeti linaitwa *Tanzanite*, *Tanzanite* pia linafanya kazi ya kutukana viongozi na Wabunge, lakini pia haya magazeti hasa hili la kwanza la Jamvi limefika mahali, kuna bwana mmoja anaitwa Musiba ambaye anafanya mambo ya ajabu, anaandika kwamba kama mimi ndiye ningekuwa kiongozi mkubwa wa nchi hii ningeweza kuua baadhi ya watu lakini hatujawahi kuona hatua zozote zinachukuliwa juu ya gazeti hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako, je, sasa kitu chako kipo tayari kuondoa *double standard* hii kwa kuita hili gazeti la Jamvi na *Tanzanite* kuweza kuwashughulikia hawa watu kwa sababu tumeona mmeanza na Raia Mwema, sasa hivyo hivyo muweze kushughulikia na Gazeti la Jamvi na *Tanzanite*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kuhusu jambo hili ambalo naamini mtalifanyia kazi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa kanuni ya 68(7). Wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo alipokuwa anajibu swali lake namba 67 na baadaye maswali ya nyongeza aliongea juu ya upatikanaji wa pembejeo lakini hakuliweka vizuri kwa sababu sasa hivi hasa zaidi Mikoa ya Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizingatia mwaka jana Serikali ilikuwa imetoa bure vifungashio kwa maana ya magunia pamoja na viatilifu kwa maana ya *sulphur* kwa ajili ya korosho na mara nyingi tumekuwa tukiona hapa hata Wabunge wengi walivyoongea kutoka maeneo hayo ikiwemo Mheshimiwa Nape pamoja na kubewa wakati ule, tumesema wazi kwamba *sulphur* sasa hivi imeanza kuuzwa tena kwa bei kubwa kabisa, imefikia mpaka Sh.80,000/= kutokana na msimu uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tetesi kwamba Serikali lakini kuna tetesi kwamba Serikali mwaka huu haitawapa tena wakulima *sulphurbure*, watatakiwa wanunue wenyeve lakini ukizingatia mwaka jana tulizalisha kiasi kikubwa cha korosho na wananchi wale walikatwa pesa nyingi kwa maana ya kupata ruzuku kwenye hii mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe mwongozo wako tuitake Serikali iweke wazi masuala haya kwamba kama *sulphur* watatoa bure kama ambavyo walifanya mwaka jana pamoja na magunia ama la ili wakulima waweze kujandaa vizuri kwa sababu karibuni tunategemea kuanza msimu wa kilimo na maandalizi ya mashamba ya mikorosho. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwakajoka.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kutoa mwongozo wangu kwa kanuni ya 68(7). Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ilionesha kabisa kwamba mahitaji ya chakula Tanzania ni tani milioni 13, lakini mavuno yalikuwa milioni 15 na tukabaki na ziada karibuni ya milioni mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016/2017 wakulima wetu wamepata hasara kubwa sana mazao yao hayakuweza kuuzwa kwa sababu mipaka ilikuwa imefungwa na badala yake soko la mazao ambalo lilipatikana Kenya likatekwa na Zambia na Watanzania wakabaki na mazao yao, mpaka leo mazao hayo yapo na sasa tunakwenda kwenye mavuno. Serikali imefanya tathmini gani ya ziada ya chakula katika nchi hii ili kutoa fursa na mipaka hii isifungwe tena ili wakulima wetu waweze kuuza mazao nje kwa muda muafaka ili waweze kupata kipato chao? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waitara.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba mwongozo wako kwa mujibu wa kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa mezani kuna *Order Paper* nafikiri hata mezani kwako hapo ipo kama ambavyo tumepata tangu tumeanza hilii Bunge la Bajeti kuanzia Hotuba ya Waziri Mkuu. Kwenye kanuni ya 14 mpaka 15 inazungumzia Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, hiyo pia ilipelekeea Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa kushirikiana na Ofisi ya Spika ikatengeneza kanuni ambazo zinaongoza Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kama vile muda mfupi uliopita Mheshimiwa Spika amezungumza kwenye hicho kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata tulipokuwa tunapitisha bajeti ya Waziri Mkuu pia kwenye *Vote 42* tuliona fedha zimetengwa zaidi ya milioni 426 kwa ajili ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa sababu tangu tumeanza kujadili hotuba ya Waziri Mkuu na tumeipitisha, sasa tumeingia hotuba ya TAMISEMI na Utawala, leo ni siku ya pili kwenye mjadala huo. Kwenye *Order Paper* zote hizi ambazo zinakuja hapa, hata kuweka hoja mezani, upande wa upinzani hatujaweka hoja zetu mezani na ni kwa sababu Ofisi ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni ambayo inatambuliwa kwa mujibu wa kanuni hizi ambazo amezitaja, tunapozungumza leo hakuna mtumishi hata mmoja ambaye anaweza kuandaa hizi hotuba ili Mawaziri vivuli na Wabunge wa Upinzani tuweze kuchangia katika hoja hizi ambazo zinaendelea. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa sababu kazi ya upinzani, wale watu walikuwa wanasaidia kama wataalam wetu kutoa taarifa mbalimbali na kuziandaa na Wabunge tunapochangia *versus* hoja ya Serikali tunakuwa na hoja zenye mashiko ili na nyie Serikali mzichukue kama sehemu ya ushauri kuweza kuboresha mipango yenu ya kusaidia Taifa hili ili tuweze kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa sababu taarifa zilizopo mtaani ni kwamba Mheshimiwa Mwenyekiti ambaye ni Kiongozi wa Upinzani Bungeni yeze

hata gari alilokuwa anatumia amenyang'anywa pamoja na dereva wake. Vilevile kwenye Ofisi yake hata msaidizi ameondolewa na watendaji wameondolewa katika ile Ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili tusiendelee kuchukua maneno ya mtaani, tulitaka kama Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani humu ndani tupate taarifa rasmi ya Bunge kwamba kwa sasa kuanzia sasa tutarajie nini, Kambi Rasmi imefutwa rasmi au ipo na kama ipo utaratibu wake ukoje. Maana zimetengwa fedha ambazo watumishi tunavyozungumza kule ofisini hawapo, mtueleze pia fedha ambazo zimepitishwa hapa zilikuwepo mwaka uliopita wa 2017/2018, pia tumepitisha mwaka huu 2018/2019 zaidi ya milioni 400 nani anakwenda kulipa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba mwongozo wako kwa sababu hii kambi rasmi maana yake ndio mabunge mengine, bahati nzuri mmetambulisha hapa Rwanda, Kenya na wenyewe wana Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na wenyewe wanahudumiwa kuliko hata Wabunge wa Tanzania wa upande wa upinzani. Sasa tungeomba mwongozo wako ili jambo hili lijilikane kwa Watanzania kama tunajua kwamba sisi watendaji wetu wameondolewa na hiyo fursa haipo, Watanzania wajue na tujipange kivingine namna ya kuweza kufanya kazi humu ndani Bungeni bila kubahatisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo maeneo ya mwongozo ambayo nimeombwa. Nianze na hili la Mheshimiwa Waitara; niseme tu mwongozo wangu kwenye eneo hili nitautoa baadaye. (*Makofi*)

Nije kwa Mheshimiwa Mwambe na Mheshimiwa Frank Mwakajoka; kwa suala zima hili la pembejeo, hasa kwa Mikoa ya Kusini, sio Kusini tu lakini kwa zao zima la korosho. Ushauri wangu na mwongozo kwa suala hili, kwa sababu linahusu

zao muhimu sana nchini na kwa kuwa hatuko mbali sana na Wizara ya Kilimo kuwasilisha bajeti yake, naamini eneo hili Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, tukiwapa nafasi, yaani tusubiri kidogo tu maana hawako mbali katika kuwasilisha bajeti ya Wizara yao, waliseme vizuri na tupate nafasi kama wawakilishi wa wananchi kwenye maeneo hayo na maeneo mengine kuishauri vizuri Serikali.

Niunganishe hapo hapo na mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa Frank Mwakajoka kuhusiana na ziada ya uzalishaji wa chakula mwaka jana na msimu huu, suala la kuzuia wakulima kuuza nje ya nchi jasho lao imekaa vipi. Nadhani Serikali kupitia Wizara ya Kilimo watakuja walitolee maelezo mazuri na ya kutosheleza ili Watanzania wote wajue nini cha kufanya. Huo ndiyo mwongozo wangu kwenye hayo maeneo mawili.

Mheshimiwa Haonga, kwanza nikusihii sana Mheshimiwa Haonga, unapajaribu ku-*challenge* maamuzi ya Kiti cha Spika, Kanuni zetu zinaku-*guide* vizuri tu, kama huridhiki na kilichosemwa na Kiti wewe zingatia tu Kanuni. Mwandikie Katibu kwamba hujaridhika na hiyo, utatoa na sababu zako, wataona namna ya kulishughulikia, lakini hii *defiance* mimi naiona haitusaidii.

Nikujibu sasa kwa hayo unayodai ya Jamvi, *Tanzanite*; hakuna kitu ambacho kinakuzuia wewe, kama alivyoofanya Mheshimiwa Mlinga, aliomba mwongozo vizuri tu na akawa ameyasema hayo aliyokuwa anayaona lakini sio kwa lengo la ku-*challenge* maamuzi na kusema kuna *double standards*. Wewe kama una-*believe* kabisa kuna kitu kinafanyika na magazeti hayo cha kulidhalilisha Bunge kama mhimili, nakusihii sana.

Mwongozo wangu; zingatia taratibu, utaleta unaweza ukamfikishia Katibu wa Bunge, iko hapa, unaweza ukalileta hilo hapa kama uliviyotaka kuomba mwongozo, uombe, lakini sio kusema kwamba Kiti kinakuwa na *double standards*, kinawaita Raia Mwema lakini hatujui waliandika nini unayodai kama wametukana viongozi, ni kitu gani.

Kwa hiyo, mwongozo wangu naanza wa kwanza, tuheshimu maamuzi ya Kiti na kama huridhiki nayo nenda katafute njia. La pili, hayo uliyoyasema mimi siyajui, ndiyo mwongozo wangu wa pili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Amina Mollel, Serikali imelijibu hili na kwa mujibu wa Kanuni zetu aliyeuliza swali la msingi alijibowi vizuri tu, nilikuwa humu ndani ya Ukumbi wa Bunge. Mheshimiwa Mollel aliuliza swali la nyongeza na akajibowi vizuri tu na Serikali, kwamba kama kuna Wakurugenzi wanaendelea na hiyo tabia ya kukaidi wajichukue kwamba nafasi zao hawazitaki na Serikali ipo.

Mwongozo wangu kwa hilo ni kwamba, narudia ni haya majibu ya Serikali yanajitosheleza kwa hayo yaliyojibowi humu Bungeni. Huo ndiyo mwongozo wangu kwa suala zima la agizo la Rais kuhusiana na maeneo ambayo wanaonekana kutozingatia.

Nakuja kwa Mheshimiwa Shangazi, ameuliza swali ambalo, mimi naelewa sisi ni viongozi wote, na juzi Mheshimiwa Naibu Spika alichukua muda mrefu sana kulielezea hili suala au kutoa mwongozo kwa suala hilli. Miongozo hii inapotolewa naamini kwamba tungependa sisi sote tuizingatie, mimi nisingependa ku-*belabor* mwongozo uliotolewa na Mheshimiwa Naibu Spika kwa eneo hili kwa sababu uko wazi kabisa.

Huko nyuma nilikuwa nawaambia, kisingizo cha kusema muda, wewe nisomee ili utupeleke vizuri. Maana Kanuni hii inakueleza kabisa kuomba mwongozo kuhusu nini; kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema na mapema tumeshatoa uamuzi, ni mapema siku hiyo sio jana na wala sio juzi au karibu karibu, ni mapema siku hiyo ili Spika atoe uafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge. Majibu ya Spika anaweza akayatoa hapohapo au baadaye. Kama linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni zetu na taratibu.

Waheshimiwa Wabunge naona tunachukua muda mwinci sana, hata kwa haya ambayo nimeyapokea, unaona kabisa tunachukua muda mwinci ambao tungeweza kuutumia kwa faida ya wananchi wetu wa Tanzania. Hata hivyo, mwongozo wangu kwa hilo ni kwamba tuzingatia Kanuni ya 68(7) kama inavyotaka na tukienda hivyo Waheshimiwa Wabunge wala hakuna tatizo, tutawajibu vizuri tu.

Waheshimiwa Wabunge, nawarejesha, mwongozo wangu kwa Mheshimiwa Shangazi ni ule uliotolewa na Kiti wakati Naibu Spika alikuwa amekalia Kiti hiki; turejee kwenye Kanuni ya 68(7).

Baada ya kusema hayo, nimemaliza mwongozo, nimebakiza kile kiporo ambacho nimesema nitakitolea mwongozo baadaye. Katibu!

MHE. SAED A. KUBNEA: Hoja ya kuahirisha mjadala.

NDG. NENELWA WANKANGA – KATIBU MEZANI:

Hoja za Serikali, kwamba Bunge sasa likubali...

MHE. SAED A. KUBNEA: Hoja ya kuahirisha mjadala.

NDG. NENELWA WANKANGA – KATIBU MEZANI: ...kupitisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, na...

MHE. SAED A. KUBNEA: Hoja ya kuahirisha mjadala.

NDG. NENELWA WANKANGA – KATIBU MEZANI: ...Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019...

MHE. SAED A. KUBNEA: Hoja ya kuahirisha mjadala.

NDG. NENELWA WANKANGA – KATIBU MEZANI: Majadiliano yanaendelea.

MHE. SAED A. KUBNEA: Hoja ya kuahirisha mjadala.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kubenea.

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 47(1), kwamba Bunge liahirishe mjadala wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Tawala za Mikoa ili nijadili jambo muhimu ambalo lipo kwenye jamii kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 19(1) inasema kila mtu anastahili kuwa na uhuru wa mawazo, imani na uchaguzi katika mambo ya dini, pamoja na uhuru wa mtu kubadilisha dini au imani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ibada ya *hijja* ni nguzo ya tano katika Nguzo za Uislamu baada ya *shahadatu laailahaillallah* na nguzo ya tano muhimu kabisa ni ibada ya *hijja*. Hata hivyo, Serikali kuititia Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, tarehe 20, Desemba, 2017 imemuandikia barua Katibu Mtendaji Kamisheni ya Wakfu ya Mali ya Amana, Sanduku la Posta 4092, Zanzibar. Naomba niisome kwa ruhusa yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kubenea, nakuomba ukae chini. Waheshimiwa Wabunge, mimi nawasihi sana, pamoja na nia njema ya Mheshimiwa Kubenea ya kutumia Kanuni ya 47, zisomeni hizi Kanuni. Suala hilo sio la dharura kwetu, nakuomba sana Mheshimiwa Kubenea, umekosea umeanza kutuhutubia. Wewe ulipaswa tu useme kwa kifupi ni nini halafu na mimi nipime, lakini nimkuona huku unakotaka kutupeleka sio suala la dharura, linaweza likashughulikiwa kwa taratibu zingine.

Kama unataka lilete kwa utaratibu mzuri tu, sio kwenye kusitisha shughuli za Bunge tulijadili suala ambalo sisi hatulifahamu.

Katibu!

NDG. NENELWA WANKANGA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha
2018/2019 - Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za
Mitaa na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora**

(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea na wachangiaji tulionao. Ninao wachangiaji, kwa utaratibu tulionao, nianze na Mheshimiwa Ester Mahawe.

MHE. ESTER A. MAHAWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kabla sijaanza naomba nitoe shukrani zangu za dhati kabisa na pongezi za kutosha kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wetu wa Awamu ya Tano kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya hususan katika Mkoa wetu wa Manyara. Napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Rais, alikuja mwaka jana mwezi Julai kuzindua barabara ya lami ambapo kwa mara ya kwanza ndiyo tunaiona lami Mkoa wa Manyara, hususani eneo la Simanjiro Mererani. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kutokana na swali langu nililoliuliza hapa Bungeni tarehe 31, Januari kwamba ni lini Mkoa wa Manyara hususan Kituo cha Afya cha Mererani kitapatiwa *ambulance* na nikajibowi hapa na Mheshimiwa Jafo ya kwamba atalifanyia jambo hilo kazi.

Kwa kuwa Rais ni Waziri wa TAMISEMI pia, alichukua hoja hiyo na juzi alipokuja kufungua ukuta pale Mererani alikuja na

ambulance hiyo, kwa hiyo namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kile alichowatendea watu wa Manyara, hususani eneo la Mererani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimekuwa nikiuliza mara kadhaa hapa Bungeni jinsi gani yale madini ya *Tanzanite* yanayochimbwa pale Mererani yanaweza kuwafaidisha wakazi wa Manyara maana yanachimbwa pale na yanauzwa Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, namshukuru Mungu kwamba tayari sasa tunaelekeea kwenda kufaidika na madini haya ya *Tanzanite* kutokana na kwamba tayari ukuta umejengwa wa kuzuia upoteaji wa madini haya ambayo mara nyingi yamekuwa yakifaidisha mataifa ya nje zaidi kuliko wakazi wa Tanzania na hususani watu wa Simanjiro na Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya kwa ajili ya wananchi wa Tanzania ya kuweza kuzuia upotevu wa madini haya ya *tanzanite* na madini mengine ya dhahabu na kadhalika. Kila mtu ni shahidi hapa ni nini ambacho Rais amekifanya karibuni kwa ajili ya kuhakikisha kwamba yale yote yanayofanyika katika nchi yetu ni kwa manufaa ya wananchi wenyewe.

TAARIFA

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpe taarifa mchangiaji kwamba madini yetu Tanzania hayaibiwi kwa sababu tulikuwa hatuna ukuta na tusione kama ukuta ni suluhisho la kutokuibiwa madini yetu kwa sababu kuna mitobozano, watu wanaweza wakapita chini wakatokea nje ya ukuta. Kinachosababisha madini yaibiwe ni mikataba mibovu, kwa hiyo, turidhie kutengeneza kwanza mikataba yetu ikae vizuri ndipo tuanze kuongea hayo mambo mengine. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mahawe.

MHE. ESTER A. MAHAWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikatae taarifa hiyo. Unajua mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Mtoto hazaliwi akakimbia siku hiyo hiyo. Kazi inayoendelea kufanyika na imekwishafanyika ya jinsi gani ya kuhakikisha madini haya yananufaisha Watanzania hakuna ambaye hajui. Kwa hiyo, wenzetu wanashindwa tu ku-appreciate juhudzi zinazofanywa na Rais pamoja na Serikali kwa ujumla. Naomba niendelee na mchango wangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inajulikana kabisa kwenye ule ukuta unakwenda kuwekwa *CCTV cameras*, unakwenda kuwekwa *electrical fence* juu yake, kwa hiyo kwa namna moja ama nyingine haya madini hayataendelea kupotea, sambamba na kuhakikisha kwamba mikataba hiyo inaendelea kutazamwa kwa ajili ya kuhakikisha madini haya yanaendelea kutunufaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kuititia pia kwa Waziri, Mheshimiwa Jafo pamoja na timu yake ya Naibu Mawaziri kwa yale ambayo wametufanya watu wa Mkoa wa Manyara. Tayari Mkoa wa Manyara tumepokea fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda pale Mbulu tumepokea fedha kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Daudi, Kituo cha Afya cha Dahwi na Dongobesh pia. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kuititia Ofisi ya TAMISEMI kwa kuona changamoto hii na kuifanyia kazi. Natoa shukrani zangu za dhati kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Mbulu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo vivyo ujisogea pale Babati tayari tumepata fedha kwa ajili ya Kituo cha Nkaiti nacho tayari kimejengwa lakini pia tumepata *ambulance* kwa ajili ya kituo hicho. Hizi juhudzi sio za kubezwa, Serikali inafanya kazi na tunaona kwa macho ya nyama na tunaendelea kushuhudia. Hanang tumepata kwa ajili ya Kituo cha Simbai pamoja na *ambulance*, kwa hiyo, niseme tu

naishukuru sana Serikali hii kwa ajili ya kile ambacho inaendelea kutenda kwa ajili ya watu wetu wa Manyara. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisogea kwenye suala zima la elimu, tumepata pia fedha, milioni 215 kwa ajili ya ukarabati wa shule mbalimbali, Shule ya pale Kiteto, tumepata fedha Mbulu, tumepata fedha Hanang, tumepata fedha maeneo mbalimbali kwenye Mkoa wetu wa Manyara kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya shule ikiwemo *hostels*, yakiwemo madarasa na ofisi za Walimu na matundu ya vyoo; kwa hiyo, niishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisemee kidogo mfuko wa asilimia tano za akinamama na asilimia tano za vijana. Nimesoma kwenye hotuba ya Waziri wa TAMISEMI jinsi gani ofisi yake ina mkakati wa kuhakikisha fedha hizi zinatengenezewa mwongozo mzuri wa namna gani ziwafikie walengwa hawa ili kuendelea kupunguza na kuondoa umaskini kwa vijana na akinamama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Jafo, amesema wana mpango wa kuondoa riba katika mikopo wanayopewa akinamama na vijana, hili jambo ni jema sana na naitakia kila la heri ofisi ya Waziri, Mheshimiwa Jafo hili jambo likapate kufanikiwa ili watu wengi wakapate kukopeshwa fedha hizi na hatimaye tuendelee kuondoa umaskini kwa ajili ya watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru pia kwa ajili ya suala zima la miundombinu ya maji katika Mkao wa Manyara, inaenda ikiimarika. Hata hivyo, nina ombi moja, kuna mradi wa maji mkubwa unaoendelea katika Wilaya ya Mwanga karibu na Bwawa la Nyumba ya Mungu, mradi huo unapakana sana na Vijiji vya Ngorika katika Wilaya ya Simanjiro na wale watu wa Ngorika hawana maji kabisa na mradi huo unaondoka kutoka kwenye eneo hilo la Ngorika ama karibu na Bwawa la Nyumba ya Mungu kuelekea Mwanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi lao ni moja tu kuitia Wizara hii ya TAMISEMI, kwamba ikiwezekana na wao waweze kupata *connection* ya maji hayo kwa sababu wako jirani sana, ili kwamba na wenyele waendelee kufaidi matunda ya Serikali hii ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yote niliyojasema changamoto hazikosekani, naomba tu niseme bado tuna changamoto ya miundombinu ya barabara katika Mkoa wa Manyara hususani maeneo ya Kiteto. Kipindi hiki Kiteto wamekuwa kama kisiwa, hawafikiki kwa sababu ya barabara kuvunjika sana kipindi hiki cha mvua. Niombe tu *TARURA*, najua wanafanya kazi kubwa na wanafanya kazi nzuri, kila mtu ameona hapa ya kwamba *TARURA* wanafanya kazi kubwa na barabara zao ni nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ikiwezekana wapate hata asilimia 50 kwa 50, *TANROADS* 50, *TARURA* 50, ili kwamba barabara nyingi zinazotumiwa na wananchi wengi maskini ziweze kutengenezwa na ziweze kuitika, waweze kuza mazao yao, waweze kufanya biashara zao na hatimaye waondokane na umaskini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kila mtu ni shahidi, mvua zimekuwa zikiendelea kunyesha kipindi hiki, barabara nyingi zimevunjika katika maeneo mbalimbali ya nchi hii, kwa hiyo, naomba ile dharura waliyoliomba *TARURA* wapatiwe ili waweze kuboresha baadhi ya maeneo korofi sana na wananchi waweze kuendelea na shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisichukue muda mrefu sana lakini niseme tu kwamba, tunaendelea kuona upungufu mkubwa wa matundu ya vyoo katika shule zetu na hali hi imekuwa ikileta shida kwa wanafunzi wetu especially watoto wa kike. Naomba Ofisi ya Rais, TAMISEMI atakapokuja hapa Mheshimiwa Jafo hapa atuambie ni mkakati na mpango gani Ofisi hii imeandaa wa haraka sana yaani kama *crash program* ya kuhakikisha mwaka kesho hatuji hapa kuzungumzia suala la upungufu wa matundu ya vyoo katika shule za msingi na sekondari nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa tuna zaidi ya upungufu wa matundu ya vyoo 270,000. Ni aibu kuendelea kuzungumza suala la upungufu wa vyoo katika karne hii naomba, Mheshimiwa Jafo atakapokuja nina hakika yeye ni mchapakazi pamoja na Naibu Mawaziri na watu wa kwenye Ofisi yake watuambie ni mkakati gani mahsusuli ulioandaliwa kuondoa tatizo hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nisisahau suala zima la watoto wakike ambao wanabebeshwa mimba wangali bado wako shulenii. Hili suala si suala la kuchukulia mzaha mzaha, hawa watoto wanakatishwa masomo yao bila ridhaa yao, lakini ninaona bado hata ule mfumo uliyowekwa si rasmi wa wao kurudi hatuwatendei haki...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
muda wa mzungumzaji)*

MHE. ESTER A. MAHAWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sasa nitawataja wafuatao wajiandae, lakini atakayefuata sasa hivi ni Mheshimiwa Amina Makilagi ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Papian, Mheshimiwa Ester Midimu na Mheshimiwa Dkt. Kikwembe ajiandae. Mheshimiwa Amina Makilagi.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuungana na wenzangu kuweza kuchangia katika hoja hizi mbili Ofisi ya TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa yote aliyenipa fursa ya kuweza kusimama na kuweza kuchangia katika Bunge lako Tukufu. Nitoe pole sana kwa wananchi wenzetu Afrika Kusini kwa kuondokewa na muasisi wetu mama Winnie Mandela. Naomba niungane nao sisi Chama cha Mapinduzi

tumepeleka mwakilishi na UWT tumepeleka mwakilishi, tunaomba tuungane nao na Mwenyezi Mungu ampoke na amlaze mahala pema peponi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na timu yake yote ya Serikali yake kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya ya kutekeleza llani ya CCM kiasi kwamba hata tukifanya uchaguzi hata hizi ndogo zilizopita Chama cha Mapinduzi kinaibuka na ushindi mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni dalili tosha kwamba hata kura zingepigwa leo za Mheshimiwa Rais na hata kura zingepigwa leo za Wheshimiwa Wabunge na hata kura zingepigwa leo za Serikali za Mitaa na hata Madiwani Chama cha Mapinduzi kingepata ushindi wa asilimia 100 kwa sababu wananchi wana imani nacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumtia moyo Mheshimiwa Rais kuwatia moyo Waheshimiwa Mawaziri wote na hasa TAMISEMI na Utumishi waendelee kuchapa kazi na sisi wanawake wa Tanzania tuko nyuma yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya utangulizi huo, naomba sasa njielekeze katika mambo machache niliyoyachagua kuyatilia mkazo. Hapa nitaanza na kwa kweli kuipongeza Ofisi ya TAMISEMI chini ya kijana wetu shupavu Mheshimiwa Jafo kwa kazi nzuri sana waliofanya ya kudhibiti matumizi ya fedha na mapato yake. Kwa mujibu wa taarifa ya mkaguzi wa hesabu za Serikali inaonesha kwamba kwa halmashauri zilizokaguliwa 166 halmashauri zimepata hati safi zaidi asilimia 90. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mkombozi mkubwa sana kwa sababu nilikuwa mjumbe wa Kamati ya LAAC tulikuwa tukiona madudu mengi katika halmashauri, matumizi ya fedha yalikuwa ni ya ovyo, watu walikuwa hawafuati kanuni za fedha, fedha zilikuwa zinaibiwa, lakini kwa usimamizi

wa Mheshimiwa Waziri na wenzake kuwa makini naona sasa matokeo mazuri yanakuja. Ni matumaini yangu sasa hata fedha zitakazokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 tutapata asilimia 100. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze mpango wa kukusanya mapato ni ukweli usiopingika kiwango kimeongezeka, lakini niseme ukweli bado hakijawa cha kuridhisha. Ni asilimia 50 tu ya mapato yote yaliyokusanywa katika halmashauri, lakini unasikiliza huku Wakurugenzi kilio kingi wanazungumzia sijui mazao, mara tulikosa mvua, mara tulikosa nini, nataka niishauri Serikali hebu Ofisi ya TAMISEMI waweke mkakati na waelekezwe Wakurugenzi waje na mawazo mapya ya kukusanya mapato, wasiendelee kutumia vyanzo vya zamani vya kutegemea kilimo peke yake, wajaribu kuwa wabunifu watafute vyanzo vipya vya mapato na Serikali kuu iwasaidie kuwekeza katika miradhi ya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kwenye uvuvi tuwekeze katika suala zima la uvuvi, kwenye kilimo tuhakikishe mazao yetu yanapata masoko, mazao yetu yananunuliwa , pembejeo zinawahidi ili mapato ya nchi yetu yaweze kuimarika na tuachane na tatizo la Serikali za Mitaa kuwa ni tegemezi kwa Serikali Kuu. Najua Wakurugenzi wakipewa maelekezo kwa Madiwani tulionao na wenyeviti wetu wa halmashauli wakithubutu najua inawezekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie Mfuko wa Wanawake na Vijana. Naomba nichukue nafasi hii kupongeza Serikali kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Wakurugenzi, Madiwani na Wenyeviti wa Halmashauri kwa kweli wameonesha kabisa tulikadiria kutenga bilioni 60, fedha zilizotolewa ni bilioni 15. Hali siyo nzuri, nazungumza kwa sababu nina uhakika nilikuwa kwenye Kamati ya LAAC kila halmashauri wanaokuja wakuja na maneno matupu, fedha haipelekwi, unaona zimepelekwa bilioni 15 peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukienda kwenye uhalisia, hawaji na vikundi ambavyo vinathibitisha kweli

wamepata hizi fedha. Kila siku tukiuliza hapa maswali, Serikali iko kwenye mkakati, tumejjipanga, tutahakikisha tunaelekeza, leo nataka nimwone Mheshimiwa Waziri Jafo, atakapokuja kuhitimisha hotuba yake atuambie sheria hii inaletwa lini katika Bunge hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu jambo hili, sio la leo, taarifa ya Mwenyekiti Mheshimiwa Ngombale kwa awamu zote tangu tumeingia kwenye Kamati ya *LAAC* amekuwa akizungumza na hii taarifa ambayo Mheshimiwa Waziri ametuletea imesema kwamba Serikali ije na sheria, *hansard* zote nimezitafuta tangu 2010, vitabu vyote hivi leo nimevibeba ninavyo, Kamati ya Bunge ya mzee Zungu na wengine na mpaka ameingia Mheshimiwa Rweikiza na hata jana wameendelea kushauri namna ya kuleta hii sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumechoka na kusikia kwamba tuko kwenye mkakati, kutengeneza mipango, tunataka kusika sasa sheria inaletwa lini hapa Bungeni. Leo nitangaze rasmi kabisa hapa, Mheshimiwa Waziri namheshimu sana, ni mwanangu, nimemlea mwenyewe, nimemtengeneza mwenyewe mpaka hapo alipofika na namjua uwezo wake wa kazi. Nataka nimirangazie rasmi kabisa kwamba kama haji na hii sheria hoja yake sikubaliani nayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu Mfuko wa asilimia kumi ya wanawake na vijana ndiyo Mfuko pekee uliowekwa kwa ajili ya kuwakomboa wanawake wanyonge, hawa wanawake walio vijijini hawana fursa ya kufikia mabenki ambayo yana riba kubwa, mashirika mengine hawayawezi kabisa wanawafanya wao kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Mfuko uliwekwa kwa ajili ya kuwakomboa wanyonge. Nimemsikia amekuja na mkakati wa kuwasamehe riba, lakini tunataka kusikia hii sheria inaletwa lini. Kwa kweli nitawaomba na nitawashawishi Waheshimiwa Wabunge, atakapokuja wakati wa kupitisha

vifungu kama haji na majibu kwa kweli mwanangu leo ajiandae kwamba mama yake sasa leo namkwamisha. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niiombe Serikali kuu huu Mfuko wa wanawake na vijana tukitegemea halmashauri peke yake hazitafika popote. Kulikuwa na mfuko ambao Serikali Kuu ilikuwa inatenga, kila mwaka zinapelekwa kwenye halmashauri kuongezea nguvu, lakini miaka mitatu hii mfululizo hakuna kinachotengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunataka leo pia tusikie Serikali ina mkakati gani wa kupeleka hizi fedha kwenye halmashauri kuongezea katika mfuko. Kwa sababu tukitegemea halmashauri zetu na halmashauri zingine ziko hoi kabisa na zingine mapato yake hayatoshi, lakini matumizi yake wakati mwingine yanakuja ya dharura, naomba leo Serikali ituambie huu Mfuko wetu uliokuwepo miaka nenda rudi ukaja ukaondoka katika miaka hii miwili, unarudi lini ili fedha ziende kusaidia wanawake na vijana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie sekta ya afya na hapa nichukue nafasi hii kwa kweli kumpongeza Mheshimiwa Waziri Jafo na timu yake yote, Waziri mwenyewe na Naibu Waziri, Katibu Mkuu lyombe na Naibu Katibu Mkuu mama Chaula, naomba nimtaje kabisa kwa jina huyu mama kwa kweli amenishangaza. Sekta ya afya wanafanya kazi vizuri sana katika kitengo hicho, wamepeleka fedha kwa ajili ya kujenga vituo 48 nchi nzima, wamepeleka fedha za kutosha na nimeshavitembelea hivyo vituo, nimeviona, juzi nilikuwa Makete, nikaenda Nyasa nimekwenda kuangalia mwenyewe kushuhudia kama kweli kazi imepelekwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana kwa hii kazi na wananchi wamenituma wanasema ahsanteni sana kwa sababu sekta ya afya ni ukombozi. Hata hivyo, kwa mujibu wa taarifa ya Waziri tunaona kabisa tuna kata zaidi ya 4000 lakini vituo vilivyopo havifiki hapa 600, lakini nimekwenda mbali zaidi nimekwenda

kufanya *research* katika Ofisi ya TAMISEMI wamenipa kitabu hiki chenye mpango mkakati wa mipango yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaona kabisa sekta ya afya ni eneo muhimu sana, vituo vilivyopo havitoshi kuhudumia wananchi. Kwenye llani ya CCM tumejielekeza kupeleka kituo cha afya kila kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuomba sana na nimeona mipango ya TAMISEMI wamenipa, hapo wanachohitaji TAMISEMI ni fedha, wanahitaji fedha kwa ajili ya kwenda kujenga vituo vya afya, wanahitaji fedha kwa ajili ya kujenga zahanati, wanahitaji fedha kwa ajili ya kujenga hospitali za Wilaya, lakini wanahitaji fedha kwa ajili ya kumalizia maboma, ambayo yalijengwa na wananchi yako zaidi ya 1800. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nguvu za wananchi zimeishia hapa. Nilimsikia juzi Mheshimiwa Ntimizi anasema ye ye amejenga karibu vituo kumi na kitu kwenye kata yake. Nimekwenda juzi Wilaya ya Njombe nimeona. Naomba sasa Serikali na bahati nzuri Ofisi ya TAMISEMI wameshatengeneza mchanganuo kwa kila eneo wanakohitaji fedha wametengeneza wanahitaji fedha katika sekta ya afya kiasi gani, wanahitaji fedha katika hospitali ya Wilaya kiasi gani na katika halmashauri. Tunaomba fedha hizi ziende ili wananchi waweze kupatiwa vituo vya afya na hospitali kwa ajili ya maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie upande wa Utumishi, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana mzee wetu mzee Mkuchika kwa kazi mzuri wanayoifanya ya kuhakikisha sekta ya uchumi inaleta maendeleo katika Taifa letu. Kwa kweli ni ukweli usiopingika wafanyakazi sasa hivi wanafanya kazi tofauti na zamani, watu walikuwa wakiingia Ofisini kuangalia mitandao, kupiga simu, kwenda kunywa chai, lakini sasa hivi kumekuwepo na nidhamu ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwapongeza, lakini ni ukweli usiopingika wafanyakazi wa

nchi hii na wenyewe wanafanya kazi katika mazingira magumu. Kuna posho zao za kujikimu katika masaa ya ziada ya kazi, manesi wetu wanafanya kazi usiku na mchana Madaktari, wafanyakazi wetu katika Taasisi mbalimbali, Walimu wana madai yao huko, lakini wanafanya kazi kwa weledi, wanafanya kwa moyo na wanafanya kazi kwa uzalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba katika bajeti inayokuja hii hebu tuwatengee fedha katika kulipa madeni tulipe na madeni ya wafanyakazi wetu ili waendelee kuwa na hali na kuendelea kuiamini Serikali yao na waendelee kuchapa kazi. Kwa kweli hapa naomba tuangalie sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la upungufu wa wafanyakzi, sekta ya afya peke yake wafanyakazi kwa upande wa TAMISEMI 66,000, upungufu huo kwenye zahanati kwenye vituo vya afya kila mahali na sijakwenda sekta zingine upungufu wa Walimu hasa wa sayansi na wa hesabu, pia Walimu wa shule za awali hawapo. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa hebu atuambie katika hawa wafanyakazi milioni hamsini mnaosema...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Emmanuel Papian, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Midimu na Mheshimiwa Dkt. Pudensiana Kikwembe ajiandae.

MHE. EMMANUEL J. PAPIAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza napongeza Serikali kwa jitihada ambazo imezifanya kutupa huduma pale Kiteto kwa kutujengea kituo cha afya pale Sunya, wanajenga barabara ya zaidi ya bilioni 6.3 kwa kupitia fedha za *USAID*, niipongeze sana Serikali. Naipongeza Serikali kwa jitihada ambazo zimetupa kwa kujenga shule zetu za sekondari zaidi ya milioni

215 imetuletea na shule inaendelea kupauliwa na sasa vijana wetu wataendelea kupata elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali yetu ya Wilaya ya Kiteto ilikuwa ni kituo cha afya na baadaye wakaamua kiwe hospitali ya Wilaya. Sasa nataka kuomba Serikali itusaidie ikiweza kututengea milioni 500 tukaongeza majengo kwenye ile jengo, hospitali yetu ya Wilaya itakuwa imekamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tuna jengo la boma la halmashauri ambalo linaendelea kujengwa na hili jengo tumefikia mahali ambapo sasa tuko kwenye hatua za mwisho. Hata hivyo, kwa mwaka huu haikutengewa pesa zozote kwa mwaka wa 2018/2019, hili jambo limetusikitisha sana, tunaomba Serikali iliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe, kuna maeneo ambayo yametengewa pesa kwa ajili ya majengo halmashauri zao hawajenga, hawana viwanja, wanatafuta maeneo, wako kwenye michakato. Pesa zimekaa zaidi ya miaka miwili, lakini kwa halmashauri ambayo ni kama ya Kiteto jengo liko kwenye *finishing* haliwezi kupata pesa. Niombe Mheshimiwa Waziri Jafo hili suala analifahamu hili jengo amelitembelea afanye jitihada atutenggee pesa tumalizie jengo sisi tuendelee kuchapa kazi pale Kiteto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuomba kuna hili suala la *TARURA*, barabara vijiji. Niishauri Serikali iangalie upya, hawa ma-*engineer* hebu wapeni *training*. Usimamizi wa hizi barabara unatupa mashaka, Mheshimiwa Waziri Jafo ameshiriki kuona ile barabara ya Sunya Namelock na jinsi ambavyo madaraja yamejengwa, tuna Mkandarasi Mshauri Mtanzania amepewa kazi. Madaraja hayawezekani kupitika tu peke yake na hata tu kupitisha maji kwa sababu yale ambayo yamekwishajengwa, *Engineers* wapo, wataalam wapo, *Engineer* wa Wilaya yupo, tumehangaika angalia barabara haiwezi kupitika ambayo *in-a-spend over 6.3 billion*, hivi kweli hawa ma-*engineer* ni Watanzania na wazalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kwenye hili, hii barabara ya Sunya Kiteto Sunya *Namelock* hii barabara isipopitika, imetumia bilioni 6.3, hawa ma-engineer mshauri wa madaraja, hawa watu naomba Serikali iwashughulikie, kabla ya hapo wasipofanya hivyo, hii barabara isipopitika miaka mitatu ijayo mimi Rais akikanyaga Kiteto ni wa kwanza kushika maiki kutaja hii kampuni ya kitapeli iliyo tapeli Wilaya yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora, hebu tusaidieni jamani watu wa utawala bora, hebu kaeni na watendaji wa Serikali wafundisheni zile *ethics* za zamani tulizokuwa nazo, watu wajue namna gani ya kufanya kazi kwenye maeneo yao. Migogoro mingi inayoibuka kwenye maeneo yetu ni kwa sababu watu wameshindwa kui-manage kabisa na hawahangaki nayo. Niombe utawala bora Wizara ya Mheshimiwa Mkuchika isimame iliangalie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili liende sambamba na kutoa watumishi. Leo tunajenga vituo nchi nzima vyta afya watendaji wako wapi, leo Kiteto pale ina zahanati haina mtumishi dawa wananchi watakunywa wapi, niombe nahitaji watumishi wa afya watumishi waliondoka wote na watumishi wamehamishwa, Wizara ya TAMISEMI imesema mtumishi anapoomba uhamisho apewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa watumishi Kiteto wamehama 30, nina *deficit* ya 30, nipe ni watumishi wangu niendelee kubaki na *deficit* lakini nikibaki na walewale wa 30. Mmewaruhusu na hamkunipa wengine, sasa watumishi watafanyaje kazi. Niombe Serikali nahitaji watumishi wa Wizara ya Afya, vituo vimefungwa, vimesimama, hakuna mtu mwenye uwezo wa kutoa dawa, wananchi wanakuja vituoni, lakini hawapati huduma. Sasa naomba Serikali iliangalie hili haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba *ambulance* zaidi ya miaka mitatu tangu nikanyage hapa Bungeni. *Ambulance* inayotumika pale Kiteto ni gari ya CCM ambayo nai-service mimi na naweka mafuta na kadhalika. Sasa

niambieni hii gari inaenda kuchakaa, sasa kwa nini isipewe gari ya *ambulance* wakati mnajua maeneo makubwa *coverage* umasaini pale Makame, Ndedo, Loolera *clinic* sasa akinamama hawawezi kwenda? Kwa nini akinamama hawawezi kwenda *clinic* na Wabunge wa Viti Maalum naomba humu ndani mkinyanyuka wa Manyara, mdai gari ya *ambulace* pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa mpole sana sasa *I am too tired!* Sasa nasema, ifikapo mwezi wa Nane hamjanipa gari nawapa gari ya Ubunge iende kuchapa kazi kule, mimi nitatembea na daladala. Siwezi ku-tolerate this level/kwa sababu wananchi wanajifungulia kwenye magari, wanajifungulia kwenye lori, wanajifungulia barabarani, tunaegesha malori yanashusha kuni wanawake wanajifungua tunawapakia humu, tunaelekeea wapi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiteto *coverage* kwenye zile *rural areas* hatuwezi kutembea watakwenda wapi nimekuwa mpole sana sasa imefika mahali *I am too tired*, nahitaji gari *immediately*. *I am too tired*, nahitaji gari la *ambulance* siyo ya kwangu, nimeomba Ofisi ya Waziri Mkuu, nikamwambia kama kuna gari imeanguka kwake Ofisini wanipe hilo gari nishirikiane na Mkurugenzi tukarabati litembee hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nikamwambia Mheshimiwa Jafo nipeni gari liliangoanguka hapo nishirikiane na Mkurugenzi tutengeneze, hakuna. Sasa nifanye nini? Nataka gari *I am tired*, nataka gari. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mikopo ya vijana, vijana, vijana wamefungua *SACCOS* tumehangai, Mkurugenzi wa Halmashauri amekusanya ile *10 percent*, ameingiza *10 million* amehangaika, tumehangai tumechangishana, vijana wameanza kukopa, nimeomba pesa jamani tusaidieni kwenye hii mifuko ya vijana hii mnayoitaja kila siku, haya mabilioni mnayosema, mbona hatuyaoni kule kwa wananchi? Wameomba *document* tumeleta hapa, *SACCOS* iko *very straight*, vijana wapo,

wanalima, wanafuga, wanahangaika barabarani, kwa nini hamtupi hata fedha kidogo wale vijana wakafanya kazi, kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii mifuko wanayoitaja ni ya nini? *Combine* hii mifuko yote, hii mifuko waliyoitaja ya vijana wakusanye kwenye mfuko mmoja, waweke mahali pamoja, waonyeshe *data* kwamba tumetoa hapa, tumepeleka hapa *otherwise* hakuna kilichofanyika na mwisho wa siku watakuwa wanasoma takwimu ambazo siyo kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe *SACCOS* yangu ya vijana na wanawake wamefungua pale, Mkurugenzi amehangaika nina Mkurugenzi mzuri sana, hizi *10 percent* anahangaika nazo, anatoka Ofisini saa saba, saa nane, anakusanya pesa anaingiza kwenye ile mifuko, vijana wanakopa, naomba Serikali *im-support*, imuunge mkono Mkurugenzi *otherwise* watakuwa wanamsulubu na vijana wetu hawawezi kufanya kazi, mwisho wa siku tutakuwa na vijana wahuni mtaani tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kushauri, ukiwa unajenga majengo mengi, una-*project* kwenda kutoa huduma, nenda sambamba na watumishi. Niombe Serikali iwarudishe wale vijana wa *Rural Medical Aids*, zamani walikuwa wanabeba *kits*, anakwenda hospitali, zahanati, anakaa hapo, anasubiri mgonjwa, anamtibu, anaendelea sasa rudisheni hawa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa vijana mnawalipa mishahara midogo, mshahara kidogo, kesho anakwenda *Medical Assistant*, atakwenda *RMO* eshokutwa atakwenda *degree*, mwisho wa siku unampandisha polepole na Serikali *through the budget* itakuwa inakwenda inapanda polepole kuendelea kuwa-*accommodate* hawa watu, lakini tuwe na watumishi kwenye *rural areas* ili zile zahanati zetu ziweze kufanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hawa watumishi warudisheni ili hivi vyuo virudi kufanya *training* kwa sababu ni

vijana ambao walikuwa wana-rescue situation, sambamba na enzi zile mnakumbuka *UPE*tulikuwa na Walimu wa darasa la saba wanafundisha, leo tumewa-phase out tumemaliza lakini ni *we need Teachers*. Lazima tuwe na alternative as a Government, lazima tuwe na alternative na options kwenda sambamba, tunajenga shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maboma mengi kule Kiteto, mengine siyasemi hapa, siwezi kuyasema hapa ni ya kwangu na kifua changu, siwezi kuyasema hapa, lakini niombe; nipe ni *special funds* kidogo nimalizie yale maboma na nyumba za Walimu. Kuna mahali Kiteto ukipeleka Mwalimu anang'ang'ania suruali ya Mkurugenzi na gari aliyoshuka nayo ni porini, hakubali kukaa na hana nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba moja walimu saba, maboma yameshindikana kukamilika, hatuna nyumba za Walimu, wananchi wamechanga wamefikisha mahali haiwezekani, nipe ni *special funds*. Rural areas kama ya Kiteto ni *special* na watumishi wengi hawakubali kwenda wanaogopa, wengi wameolewa, wameondoka. Sasa tupeni watumishi na tujengeeni yale maboma ya nyumba za Walimu, Walimu wakubali kukaa, inafika mahali wanaogopa, ikifika jioni anaogopa, shule nyingi zipo porini, sasa zile shule zilizopo porini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Esther Midimu, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe na Mheshimiwa Ignas Malocha ajiandae.

Mheshimiwa Midimu.

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Kwanza kabisa namshukuru Rais kwa kazi nzuri anazozifanya kwa kazi nzuri anazozifanya Mwenyezi Mungu ambariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, namshukuru Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Mwenyezi Mungu awabariki sana kwa kazi nzuri wanazozifanya. Pia nampongeza sana Waziri wa TAMISEMI na Naibu Mawaziri wake pamoa na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri wanazozifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara ya Afya kwa kuendelea kuboresha miundombinu ya afya. Katika Mkoa wetu wa Simiyu tuna tatizo la upungufu wa wafanyakazi. Katika vituo vya afya na hospitali hatuna watumishi kabisa. Tunaiomba Serikali yangu sikivu itusaidie ili tuweze kupata watumishi katika hospitali zetu za Mkoa wa Simiyu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kutenga pesa ili tuweze kujenga Wilaya mpya ya Itilima na Busega, wametenga billioni tatu. Naiomba Serikali yangu sikivu hizo pesa zije kwa wakati, tujenge hospitali kwa wakati ili iweze kusaidia Wanabusega na Wanaitilima kwa ujumla. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Wilaya ya Busega wanahangaika sana na wa Itilima, wanafuata matibabu Wilaya ya Bariadi na Wilaya ya Bariadi inategemewa na Wilaya tatu, hivyo, kuna msongamano wa wagonjwa sana. Sasa naiomba Serikali yangu sikivu iweze kukamilisha hizo hospitali haraka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ya Wilaya ya Meatu haina Daktari bingwa kabisa wa magonjwa ya akinamama. Akinamama wa Wilaya Meatu wanahangaika sana, wanafuata matibabu Wilaya ya Bariadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni mtu wa Simiyu, mtu atoke Kata ya Mwabuzo kufuata matibabu Bariadi na hiyo hiyo Wilaya ya Bariadi ina Daktari bingwa mmoja anategemewa na Wilaya nne; Wilaya ya Bariadi, Wilaya ya Meatu, Wilaya ya Busega na Wilaya ya Itilima. Tunaomba katika hospitali ya Meatu mtuletee Daktari Bingwa wa magonjwa ya akinamama. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu, naishukuru Serikali kwa mpango wake wa elimu bure. Katika Wilaya Maswa tuna sekondari 36, maabara zilizokamilika ni saba, maabara 29 bado, zimejengwa na zimeezekwa kwa kuititia Halmashauri na nguvu za wananchi. Naiomba Serikali sasa itusaidie ili maabara ziweze kukamilika na shule bila maabara bado hajakamilika kwa sababu wanafunzi wanatakiwa kusoma masomo ya sayansi yaani *chemistry* na *physics*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni upungufu wa Walimu katika shule za msingi na shule za sekondari. Naiomba Serikali yangu itusaidie Walimu katika shule zetu za Simiyu za sekondari na za shule ya msingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi wa maji wa Ziwa Victoria, kwanza niishukuru sana Serikali mwaka jana kwa kutenga pesa za mradi wa maji wa Ziwa Victoria unaokuja Simiyu. Mradi huu mpaka sasa haujaanza na hakuna dalili zozote zinazoonekana kwamba mradi unaweza ukaanza. Mheshimiwa Waziri wa Maji niilumuuliza swali kuhusu mradi huu, Waziri akanijibu vizuri sana kwamba mradi huo unaweza ukaanza mara moja. Huo mradi utaanza na Wilaya ya Busega, Bariadi pamoja na Itlima kwa awamu ya kwanza ambao ujenzi wake utachukua miaka miwili. Akasema awamu ya pili atamalizia na Maswa na Meatu, lakini mpaka sasa hakuna kinachoendelea kule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni mtu wa Simiyu unajua akinamama wanavyohangaika kutafuta maji, hivyo, mradi huu utawasaidia sana akinamama ambao wanahangaika kutafuta maji kuliko kufanya kazi za maendeleo. Pia utasaidia kwenye taasisi za Serikali kama shule, zahanati na vituo vya afya. Vilevile tutalima na kilimo cha umwagiliaji, sisi ni wachapakazi njaa kwetu itakuwa ni ndoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi mwengine wa Maswa wa chujio, yaani huu mradi umekuwa ni kizungumkuti. Mradi huu una miaka mingi wananchi wa Maswa

wanakunywa maji siyo safi na salama. Nilishawahi kuuliza swali humu, Mheshimiwa Waziri akanipa moyo akasema baada ya miezi mitatu huo mradi utakamilika, huu mradi unasuua sua. Mkandarasi huyu kila akiongezewa muda hamalizi, miaka nenda rudi anaongezewa muda huu mradi hauishi, wananchi wetu wanaendelea kuhangaika. Serikali ina kigugumizi gani kuvunja huo mkataba na mwekezaji huyu, ikafunga mkataba na mwekezaji mwngine? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuishukuru Serikali yangu sana ya Chama cha Mapinduzi ikiongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, mchapakazi, Mwenyezi Mungu ambariki, naendelea kuishukuru sana kwa Wilaya ya Itilima inaendelea kutuletea fedha za kujenga miundombinu. Sasa hivi tumejenga jengo la utawala, zahanati zinaendelea na vituo vya afya vinaendelea, Mwenyezi Mungu ambariki sana. (*Makofii*)

WABUNGE FULANI: Amen!

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kunisemea na mimi maana niko mezani hapa. (*Makofii*)

Tunaendelea nimitaje Mheshimiwa Kikwembe atafuatiwa na Mheshimiwa Malocha halafu na Mheshimiwa Rashid Shangazi ajiandae halafu nitaanza utaratibu mwngine.

MHE. DKT. PUDENCIA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza kabisa napenda kuishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Dkt. John Pombe Magufuli kwa namna ambavyo amekuwa akitakeliza majukumu ambayo yamekuwa yakinatua shida mbalimbali zinazowagusa wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili napenda niishukuru Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa namna ya kipekee ambayo imekuwa ikifanya kazi kwa karibu na mimi Mbunge wa Jimbo la Kavuu kwa namna ambavyo wamekuwa wakijaribu kutatua matatizo ya wananchi wangu. Napenda kabisa niishukuru Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya TAMISEMI kwa kuweza kunipatia *ambulance* ambayo inaweza ikafanya *shunting* kati ya vituo viwili vyaa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua jiografia ya Jimbo langu bado siyo nzuri, kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI uniongezee *ambulance* itakayofanana na miundombinu ambayo nimepata. Hata hivyo, nashukuru sana kwa kile nilichokipata ambacho ni *ambulance* ambayo itanisaidia kutoka kituo cha afya cha Kibaoni kwenda kituo cha afya cha Mamba. (*Makofi*)

Mheshimiwa wenyekiti, napenda niendelee kushukuru kwa kuwa wameweza kuniwezesha kituo changu cha afya cha Kibaoni ambacho sasa kinalekeea kwisha lakini niwaombe katika Jimbo langu la Kavuu nina vituo vyaa afya vitatu; nina kituo cha afya cha Mamba na kingine cha Mwamapuli ambacho wananchi wameanza kujitolea namna ambavyo ya kuweza kutatua matatizo ya afya kutokana na jiografia ilivyokaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri atuongezee nguvu katika vituo hivi. Nimshukuru kwa namna ya pekee Dkt. Zainab ambaye aliweza kutupa mawazo akishirikiana na Katibu Mkuu *Engineer lyombe* namna ambavyo tunaweza tukaanzisha hospitali ya Halmashauri ya Wilaya katika Jimbo la Kavuu na niwashukuru Wizara hii wametupatia kibali na sasa tunakwenda kujenga hospitali ya Wilaya. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee lingine limekuwa likiongelewa sana na limeongeleta na baadhi ya Wabunge hata jana kuhusu mchango wa chakula mashulenii. Ni kweli kwamba chakula mashulenii kinapunguza utoro, ni

kweli kwamba chakula mashulenii kinasaidia wanafunzi kuwepo mashulenii na kinaongeza kiwango cha ufaulu. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge tuendeleee kuwaomba wananchi wetu waendeleee kuchangia kwa maana ya kwamba ni jambo lenye tija katika kizazi chetu kijacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano tu; Mbunge wao wananchi wangu wa Jimbo la kavuu nimeweza kuchangia karibu hekari 30 kwa maana kwamba kila shule inapata hekari moja ya chakula na sasa tumeanza kuvuna. Kwa hiyo ni mchango wangu kwa chakula kwa maana naelewa umuhimu wa chakula mashulenii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru Serikali na niishukuru halmashauri yangu, Halmashauri ya Mpingwe imekuwa ni halmashauri ya pilli katika halmashauri 185 ambayo imekuwa ikifanya vizuri katika kutenga asilimia 10 kwa maana kwamba asilimia tano ya akinamama na asilimia tano ya vijana. Kwa hiyo, niwaombe, niko vizuri na Mkurugenzi wangu na nafanya naye kazi vizuri sana na anasimamia miradi vizuri mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba, kama watafanya *resuffle* mimi Mkurugenzi wangu waniachie pale, yuko vizuri. Kama kuna Wakurugenzi wengine hawako vizuri mimi wa kwangu yuko vizuri, anasimamia miradi vizuri, milioni 400 walizonipa kituo cha Kibaoni pale cha afya zimesimamiwa vizuri, pesa za Jimbo zinasimamiwa vizuri. Kwa hiyo, kazi inakwenda na maendeleo tunayaona na Jimbo la Kavuu sasa linaonesha mabadiliko chini ya Dkt. Pudenciana Kikwembe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishukuru Serikali kwa namna ya pekee ilivyoondoa riba katika ule mkopo wa asilimia 10 kwa akinamama na vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudi kwa *TARURA*. *TARURA* ni chombo ambacho kwa malengo yake ni mazuri sana, lakini naomba kiongezewe pesa, kiongezewe

watalaan. Kutoakana na mvua hizi zinazonyesha nilikwenda ofisini kwa Mheshimiwa Waziri na nikapeleka maombi yangu binafsi, maombi rasmi, maombi *special*/kwa namna ambavyo sasa Jimboni kwango hakuna hata njia moja inayopitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwomba pesa ya kutengeneza *box culvert* ya Mwamapuli-Majimoto ambayo inagharimu karibu milioni 160, nimeomba Majimoto daraja jipya la Msadya ambalo kwa wale wanaongalia vyombo vya habari waliniona nikienda kulitembelea. Sasa hivi kwa hela waliyotupatia nashukuru limeanza kupitika angalau wagonjwa wanawenza kwenda kutibiwa kituo cha afya kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pesa takribani bilioni 1.7 kwa ajili ya kujenga daraja lingine, kwa sababu daraja lile llinahudumla karibu Kata tano kwa ajili ya akinamama na watoto wanaokwenda hospitali. Kwa hiyo, ni maombi rasmi, naomba niyalete kwako hapa na kwa sababu nilishayaleta kwa maandishi naomba mnisaidie kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba *drift* mbili kat i ya Ntibili na Kikonko ambako kumepata mafuriko na hivi ninavyoongea mvua bado zinaendelea, zimenyesha karibu siku nne mfululizo. Naomba pia *box culvert* kat i ya Kata ya Mamba na Makuyugu ambayo inaweza kugharimu pia milioni 160.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia *culvert* ya Kibaoni-Chamalendi ambako pia barabara imekatika ambayo ni barabara moja hiyo hiyo inayoungnisha kwenda kwenye kituo cha afya cha Kibaoni. Naomba pia *culvert* lingine la Mabambasi kupitia Mwamapuli ambalo pia linaunganisha barabara hiyo hiyo kwenda kwenye Kata ya Kibaoni ambayo inakwenda kwenye kituo cha afya ambacho watu wanatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la watumishi, watumishi wamekuwa wengi wakistaafu hawapati

haki zao, kwa mfano, tuna wastaaafu wa Magereza na Mahakama wapatao karibu 200 waliostaafu tarehe 1 Julai, mpaka leo hawjaalipwa haki zao kwa hiyo tulikuwa tunaomba walipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwa watumishi Walimu; Walimu wamekuwa kama ni wanyanyaswaji kwa sababu hawapandishwi vyeo vyao, hawalipwi pesa zao wanapokwenda likizo, hawalipwi pesa zao wanapohamishwa. Kwa hiyo, naomba malipo yao kwa kweli kwa mwaka huu yatiliwe mkazo. Walimu wetu ni wachache katika vituo vyetu, sasa tunapozidi kuwadidimiza, tunawapunguzia *morally* ya kazi kwa kweli naomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee lingine; Mwalimu anapotaka kuhama tunasema atafute nafasi eneo mbadala ili aweze kuhamishwa. Sasa unakuta kuna mwingine kaolewa ama mwingine kaoa kule mnakompeleka hana mume, hana mke, mnachotarajia nini? Kwa hiyo, niwaombe kama mume anataka kumfuata mkewe au mke anataka kumfuata mume wake basi waruhusiwe kwa sababu tunajua maambukizi mapya ya UKIMWI sasa hivi ni mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapowaachanisha vile inakuwa ni rahisi kuwaweka kwenye mitego ambayo wanaweza wakapata maambukizi. Kwa hiyo, tunaomba muwalipe malipo yao ya uhamisho na mambo yao mengine ambayo wamekuwa wakidai hasa wanapokuwa pia wanakwenda kwenye matibabu ambayo yako nje ya utaratibu wa bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana suala la Walimu, kwa kweli ni tatizo. Mimi ni Mwalimu pamoja na kwamba ni Mbunge, lakini ninapokwenda Jimboni kwangu mimi naingia darasani kufundisha. Nafundisha kwa sababu ya uhaba wa Walimu. Kwa hiyo niwaombe sana, katika kasma ijayo ya waajiriwa mtupatие watumishi wa sekta ya afya pamoja na sekta ya ualimu, ni vitu ambavyo tunavihitaji sana hasa katika kuhudumia wagonjwa wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nahitaji zaidi Madaktari badala ya Makatibu wa Vituo vya Afya. Makatibu wanakaa ofisini na *computer*, nkipata *nurse* pale *clinic* atanisiaidia zaidi kuliko Katibu wa Afya. Kwa hiyo, naomba hata tunapofanya *allocation* ya watumishi, tuangalie; Kituo changu cha Kibaoni kina Makatibu wa Afya watatu wa nini?

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naunga mkono hoja kwa asilimia zote.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Rashid Shangazi na Mheshimiwa Heche ajiandae.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na uzima kwa siku ya leo. Pia nampongeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa utendaji wake wa kazi. Naomba ndoto yake ifike mahali ifikie mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nawashukuru na kuwapongeza Mawaziri wote; ndugu yangu Mheshimiwa Jafo; Naibu Mawaziri, ndugu yangu Mheshimiwa Kandege, Mheshimiwa Kakunda na Mheshimiwa Mkuchika. Nawapongeza kwa sababu kubwa, kwanza kwa hekima zao, busara, uwajibikaji, unyenyekevu, uzalendo na usikivu. Tunachowea kuomba kwa Mwenyezi Mungu, aendelee kuwapa afya njema ili waendelee kulitumikia Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na utawala bora. Utawala bora ni pamoja na kusogeza huduma karibu na wananchi. Ili wananchi waweze kupata huduma bora, ni lazima wawe karibu na huduma. Nazungumza jambo hili

kutokana na mazingira ya Jimbo langu. Jimbo langu lina jiografia mbaya na ni kubwa na limekaa vibaya na linawatesa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimchukua mwananchi aliyeo kule llambo ili afike Makao Makuu apate huduma, anatumia karibu nauli ya Sh.50,000/=; kwenda na kurudi Sh.100,000/=, nauli ya kutoka Sumbawanga mpaka hapa Dodoma. Sasa akiwa na mgonjwa, kukodi gari, lazima awe na shilingi milioni moja; au akiwa na kesi, anahitaji mashahidi watano, lazima awe na Sh.500,000. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linawatesa wananchi na sijajua ni kwa nini? Kwa sababau tumepeleka maombi mara kadhaa. Bahati nzuri wapo mashuhuda mbalimbali ambao wameshuhudia jambo hili na ukubwa wake, ambao nataka niwataje leo hii. Shuhuda wa kwanza ni yeye mwenyewe Mheshimiwa Mkuchika, alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, anayafahamu mazingira vizuri mno. (*Makof*)

MBUNGE FULANI: Kabisa.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, shuhuda wa pili ni Mheshimiwa Ole Njoolay, alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa. Shuhuda wa tatu ni ndugu yangu Mheshimiwa Stella Manyanya, alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa na jitihada alizianza yeye mwenyewe japokuwa hazijafanikiwa. Shuhuda wa nne alikuwa Zolote Stephen Zolote. Shuhuda wa tano ni Waziri Mkuu, ndugu yangu Mheshimiwa Majaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana, juzi alifika mpaka Mto Wisa mahali ambapo kuna changamoto kubwa sana. Shuhuda wa sita ni Katibu Mkuu Ndugu Abdulrahman Kinana; yeye tena alitamka kabisa kwamba Jimbo hili lazima ligawanyike, Wilaya lazima ipatikane na Halmashauri lazima zipatikane. Huyo ni shuhuda wa sita. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shuhuda wa saba ni Waziri wa Uchukuzi, ndugu yangu Mbalawa, juzi amepita kule ameliona Jimbo jinsi ilivyo. Shuhuda wa name ni Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu, alifika kule wakati wa kampeni, akashangaa kwamba hivi kweli eneo kama hili linakuwa na changamoto namna hii, linatengwa kiasi hiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, shuhuda wa tisa ni Waziri wa Mambo ya Ndani, ndugu yangu Mheshimiwa Mwigulu, wakati wa kampeni alikuja kule akashangaa eneo jinsi ilivyo. Shuhuda wa kumi ni Waziri wa TAMISEMI ndugu yangu Mheshimiwa Jafo. Alikuja akakaa na Mkuu wa Mkoa mpaka akaanza kumpa jiografia, bahati mbaya hakuzunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shuhuda wa 11 ni Naibu Waziri, ndugu yangu Mheshimiwa Kandege, anajua hali halisi jinsi ilivyo. Shuhuda wa 12 ni Wabunge wote wa Mkoa wa Rukwa na Wabunge majirani wa Mkoa wa Songwe na Mkoa wa Mbeya na baadhi ya Madiwani ambao wamefika katika maeneo yale. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shuhuda mwingine wa 13 ni Naibu Katibu Mkuu wa Elimu, ndugu yangu Zunda, alikuwa Afisa Tawala juzi juzi kwetu. Shuhuda wa 14 ni ndugu yangu Katibu Mkuu Iyombe, alikuwa Meneja wa *TANROAD* Mkoa wa Rukwa. Anayafahamu mazingira vizuri mno. Shuhuda wa 15 ni Waziri Mkuu Mstaifu, Mheshimiwa Warioba, alishawahidi kufika maeneo yale. Alishangaa sana maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shuhuda wa 16 ni Waziri Mstaifu, ndugu yangu Pinda na alitamka hata hapa Bungeni kwamba kwa kweli Jimbo lile ni kubwa na jiografia ni mbaya. Shuhuda wa 17 ni wengine wengi Watendaji wa Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jamani, hata kama Serikali imesimamisha matumizi, wakati mwingine Rais wetu hamumwelezi hali halisi. Mheshimiwa Rais huyu ana huruma kubwa mno. Tunaona maeneo mengi anavyofika anatetea wanyonge. Angepata hali halisi, nami naomba Mwenyezi

Mungu, huyu mtu siku moja afike kwenye Jimbo langu, atatamka pale pale kwa jinsi ninavyomfahamu Mheshimiwa Rais huyu kwa huruma yake, atatamka siku ile ile. Ila wana-*by pass* hawampii *information* hali halisi ya mateso ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli jambo hili linaumiza wananchi na bahati nzuri walio wengi najua wengi wanalijua Jimbo langu. Inaumiza sana hasa wananchi wangu wanashindwa kupata huduma sahihi. Hii maana yake nini? Naomba Mheshimiwa Jafo jambo hili alitolee ufanuzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuzungumza ni suala la afya. Kwanza naishukuru Serikali, juzi juzi wametuambia wametutengea Sh.1,500,000,000/= kwa ajili ya kujenga Hospitali ya Wilaya, tunashukuru sana, lakini vilevile walitupa Sh.400,000,000/= kwa ajili ya kupanua Kituo cha Afya cha Milepa, tunashukuru na kinaenda vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba upanuzi wa vituo vingine vya afya kama Kituo cha pale Nkuhi; Naibu Waziri, ndugu yangu Mheshimiwa Kandege alienda pale akakutana na Watendaji na wananchi wa pale Nkuhi na akasema atalishughulikia. Naomba sasa jambo hili ndugu yangu Mheshimiwa Kandege, wananchi wa Nkuhi wanasubiri awasaidie, kile kituo kiingie kwenye upanuzi na vilevile Kituo cha llemba. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vingine ambavyo vinaendelea katika kumalizika katika hatua mbalimbali ni Muze, Kahoze, Kipeta na Kalambazito. Vilevile tunazo zahanati ambazo zilishafika katika hatua mbalimbali. Zahanati 21 zinahitaji tu kupewa fedha ili ziweze kumalizika na zianze kutoa huduma kwa wananchi. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kuzungumzia ni utaratibu wa upatikanaji watumishi katika

Vituo vya Afya wa kada ya ulinzi, dobi na wapishi. Bado na lenyewe hili ni changamoto, halijulikani vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nizungumzie kuhusu suala la elimu. Kwanza tunashukuru Serikali yetu kwa elimu bure, lakini vilevile zipo changamoto ukiacha Walimu wa Sayansi; na juzi nimepita Lahela pale wananchi wamelalamikia shule yao ile ya Uchile, hawana Walimu wa masomo ya sayansi, lakini vile vile zipo shule kadhaa ambazo zimeanzishwa na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hilo nataka nilzungumze, hizi shule mpya ambazo zinaanzishwa na wananchi, wanazianzisha kwa mahitaji ya watoto wao ambao wakati mwininge shule nyingine ziko mbali au kuna changamoto ya daraja wanaogopa watoto wao wasije wakapata madhara? Wanaamua wao wenyewe kujichangisha nguvu kazi kujenga shule mpaka wanafikia kujenga madarasa manne, ofisi, madawati, lakini changamoto ni namna ya kujisajili. Sijajua hapa kuna jambo gani? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawa wamejitelea wenyewe na sheria inasema shule mpya ya wananchi waliojitelea wenyewe; japokuwa tunapasha kuliangalia upya. Wananchi hawa wengi watoto wao watakosa elimu kwa sababu ni wachache wanaoweza kujitoa. Lenyewe hili nilitaka mliangalie vizuri. Pia shule yangu ya pale Kirando ambayo wananchi walishajitelea wakajenga, iko vizuri; na Shule ya kule Nhungwe, shule ya kule Nkuhi na Shule ya Mahenje kule Milepa Kinamo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naiomba Serikali ijaribu kuangalia fedha za ujenzi wa madaraja, nyumba za Walimu na Vyuo ambavyo zinasimamiwa na elimu. Nashauri fedha hizi ziende TAMISEMI. Wale wabaki na shughuli ya kusimamia taaluma. Ziende TAMISEMI waweze kusimamia fedha hizi. Kwa hiyo, naishauri Serikali iweze kuliangalia jambo hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la barabara. Kwanza naishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi, namshukuru Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Magufuli, alipokuwa Waziri ni mara kadhaa nilikuwa nikimwomba juu ya fedha za kujenga daraja la Mto Mombasa na alikuwa akiniahidi. Nashukuru kwamba baada ya kuwa Rais, katika jambo ambalo alikuwa na kumbukumbu nalo ni kutoa fedha za ujenzi wa daraja la Mto Mombasa, ametupa shilingi bilioni 17.8 na daraja limeshaanza kujengwa, tunatarajia mwezi wa Saba litamalizika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba baada ya kumalizika daraja hilo, Serikali ianze sasa hatua nyingine za upembizi yakinifu ya kuunganisha barabara kwa ajili ya lami kwa maana ya kutoka Kibaoni kuja Kilyamatundu kuungana na wenzetu wa Songwe kwa maana ya kutokea Mloo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ile bado ina changamoto kubwa, ina madaraja mengi na ni eneo ambalo lina uzalishaji wa hali ya juu; mpunga, mahindi, karanga, mtama na kadhalika. Ile barabara ikikamilika, ndilo eneo ambalo tumetarajia hata viwanda vyenyewe vinaweza vikapatikana katika eneo lile kwa sababu mpunga unalimwa kwa wingi. Tunakosa kutangaza...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Rashid Shangazi.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika hoja ambayo iko mbele ya Bunge lako Tukufu. Nami nianze kuwapongeza kwa kazi nzuri sana ambayo Mawaziri wote wawili pamoja na Naibu Mawaziri wamekuwa wakifanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nitoe salamu za pole kwa mtani wangu Mheshimiwa Kakunda kwa shida aliyoiopata ya ajali, lakini Mwenyezi Mungu ameendelea kumsimamia na kumuimarisha; naamini ni kwa sababu ya mambo mema anayowatendea Watanzania, basi hata Mwenyezi Mungu ataendelea kumlinda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa namna ambavyo anatenda kazi na hasa katika Wizara hii ya TAMISEMI. Hivi karibuni alitoa tangazo la kuzuia pesa za Halmashauri ya Bumbuli kutokana na tatizo kidogo la wapi yajengwe Makao Makuu ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia fursa hii kutoa shukrani kwa sababu jana ye ye mwenyewe amempigia Mbunge wa Bumbuli Mheshimiwa Januari Makamba na kwamba pesa zile zimerudishwa na zitaendeleza ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Halmashauri ya Bumbuli. Tunamshukuru sana kama Wanatanga, hili ni jambo jema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninazo changamoto kadhaa; ya kwanza ni eneo la kiutawala. Lengo la Serikali za Mitaa, madaraka mikoani pamoja na ugatu ni kurahisisha shughuli za maendeleo katika maeneo ya Serikali za Mitaa, lakini bado Mkoa wa Tanga unaonekana ndiyo mkoa wenye Halmashauri nyingi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza, Mkoa wa Tanga una Halmashauri 11, una Majimbo ya Uchaguzi 12. Kwa hiyo, hata kuitendaji, baadhi ya shughuli zinasuasua. Mkoa wa Tanga una Shule za Msingi zaidi ya 1,032. Utaona ni mzigo mkubwa sana kuwa na Afisa Elimu ambaye anasimamia shule hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurudi katika Halmashauri ya Lushoto ina shule 162. Sasa utaona kwamba hii ni idadi kubwa ya shule na tunashindwa kuzisimamia na wakati mwingine hata matokeo yanapotoka mara nyingi unakuta

hatufanyi vizuri. Kwa hiyo, inawezekana hatufanyi vizuri siyo kwa sababu watu hawana uwezo ama hatujaandaa mazingira wezeshi ya wanafunzi kupata elimu, lakini tatizo ni kwamba, ni eneo kubwa la kiutawala kiasi kwamba wanashindwa kusimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua liko zio kwamba sasa hivi hakuna kugawanya mikoa ama Majimbo na kadhalika, lakini ni lazima ukweli tuseme, ieleteke hivyo kwamba Mkoa wa Tanga ndiyo mkoa pekee katika Jamhuri ya Muungano wenye Halmashauri 11 inafuata Morogoro, ina Halmashauri tisa; Mtwara ina Halmashauri tisa; Kagera, Halmashauri name; na Mara Halmashauri tisa. Kote huko ukiangalia kwenye mikoa ambayo ina Halmashauri nyingi kuna matatizo ya kiutawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima tukae na Serikali iweze kuona. Mathalan kuna mikoa ambayo ina chache. Mkoa wa Rukwa una Halmashauri nne, Mkoa wa Songwe una Halmashauri tano, Mkoa wa Iringa una Halmashauri tano, Mkoa wa Shinyanga, Halmashauri sita; Geita, Halmashauri sita. Kwa hiyo, mkoa wenye Halmashauri 11kulinganisha na mkoa wenye Halmashauri tano au nne, maana yake kwa kweli katika ulinganishi hatuwezi tukatenda sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija katika Shule za Msingi, nimesema Mkoa wa Tanga una shule 1,032; Mkoa wa Kagera 955; Mkoa wa Kilimanjaro 973. Kwa hiyo, Tanga bado inaongoza katika Shule za Msingi. Ukija Iringa kuna Shule za Msingi 499; Katavi kuna shule 177 ambazo ni chache kushinda hata zilizopo Wilaya ya Lushoto. Geita kuna shule 603. Sasa hawa Maafisa Elimu watasimamiaje kwa ulinganifu ambao hauko sawa? Kwa hiyo, tunaomba Wizara hii iweze kuliona hili jambo na kututafutia *solution*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye suala la miundombinu ya elimu, tunao uhaba mkubwa wa Walimu katika Halmashauri ya Lushoto. Mahitaji ya Halmashauri ni

Walimu 2,408, waliopo ni 1,547. Kuna upungufu wa Walimu 861. Utaona ni *gap* kubwa sana. Kwa hiyo, tunaomba sana tutoe kipumblebe kwa maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa upande wa Walimu wa Sayansi tunazo sekondari 60 ambazo zina upungufu wa Walimu 123.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa nilizungumzie ni suala la mipango pamoja na TARURA. Sasa hivi mpango wa Serikali ni kufikisha umeme vijiji 2020/2021 ndiyo utakuwa mwisho, lakini yapo maeneo ambayo mpaka sasa hivi hayana barabara. Sasa sioni *connection* kati ya mipango hii ya mwaka mmoja na miaka mitano ya Kitaifa katika Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yangu ni kwamba tunatarajia kwamba TARURA wameanza kuchukua barabara zile ambazo Halmashauri ilikuwa tayari iko nazo, lakini tukumbuke kwamba kuna vijiji vingine viko katika maeneo ya milima kutokana na jiografia, bado havijafikiwa na huduma ya barabara. Ukiwaambia TARURA wanakwambia bado hii hatujaipokea, tumepokea zile ambazo zilikuwa zinahudumiwa na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitoe rai kwamba ili mipango ya Serikali isiwe *double standard* kwamba umeme vijiji mwisho ni 2020/2021, basi iwe sambasamba na utengenezaji wa barabara ili watu wa umeme waweze kufikisha zile nguzo kule. Bila kuwa na barabara, nguzo zifatikaje? Kwa hiyo, nawaomba sana TAMISEMI hili jambo waliangalie kwa kina. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo, nataka nizungumze wazi na kwa sababu tunashauri na kuisimamia Serikali, mimi kwenye Halmashauri yangu, sioni umuhimu wa kuwa na Maafisa Ugani kwa sababu hawaongezi chochote katika kilimo. Hapa juzi nimezungumza suala la kilimo cha kahawa, kila Mbunge ananiuliza kwamba Lushoto kuna

kahawa? Maana yake ni kwamba hata Serikali inawezekana hawajui kwamba milima ya usambara kuna kilimo cha kahawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa una Maafisa Ugani ambao hawawezi hata kutoa taarifa kwenye Serikali. Kwa hiyo, hata katika huu uhaba wa Walimu hata mimi nimuunge mkono Mheshimiwa Dkt. Kikwembe kwamba ukiniambia uondoe Maafisa Ugani uniletee Walimu, nitashukuru, kwa sababu sioni kazi wanayofanya kule. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tumekuwa na idara inayotabiri hali ya hewa, inaeleza kuhusu hali ya hewa kwamba safari hii tutakuwa na mvua chini ya wastani, safari hii tutakuwa na mvua nydingi; unatarajia kwamba Maafisa Kilimo wachukue hizi taarifa za hali ya mvua wazitafsiri kwa wananchi, lakini bado wananchi wanalima kwa mazoea. Hawajui kwamba tukilima mahindi mvua zitakata mapema, hawajui kwamba tukilima labda mahindi sehemu za mabondeni, tumetabiriwa kutakuwa na mvua juu ya wastani, kwa hiyo, kuna mafuriko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika eneo hilo napenda kusema wazi kabisa kwamba Idara ya Kilimo katika Halmashauri yangu ya Lushoto, lakini naamini hili ni katika nchi nzima kwa sababu tumeona hata katika mpango kwamba kilimo kinakua kwa asilimia 3.3, kwa hiyo, hili ni eneo ambalo linatakiwa litizamwe kwa mapana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la utawala bora ambalo tunalizingumza mara kwa mara na kwa bahati Mheshimiwa Mkuchika alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga, anafahamu. Tunao Wenyeviti wa Vijiji na kwa mujibu wa kanuni hapa tunaambiwa kwamba sheria asilimia 20 ya mapato ya Halmashauri inatakiwa iende kulipa hawa Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji. Mpaka sasa wana zaidi ya miaka saba wanadai hawajalipwa chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumza hapa asilimia tano na asilimia kumi, tunazungumza tu kwa ajili ya vijana na akinamama, lakini mbona hatuzungumzii hao Wenyevitii wa Serikali za Vijiji ambao mpaka sasa hivi hawapati hizi posho zao, kiasi kwamba hata kwenda kusimamia shughuli za maendeleo wakati mwingine wanafanya kama hisani, kwa sababu hawapi *motivation* yoyote. Kwa hiyo, nitoe rai kwamba tunapozungumza suala la utawala bora, ni lazima pia tuzingatii maslahi mapana ya hawa watenda kazi katika ngazi za vijiji na ngazi za vitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni miradi ya maji. Tunashukuru kwamba miradi ya maji inaendelea kufanyiwa kazi, lakini kwa changamoto hata Kamati ya LAAC ilivyokwenda katika Mkoa wa Tanga kuna matatizo makubwa ya usimamizi wa miradi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwa utafiti wangu, tatizo liko kwa Mhandisi wa Maji wa Mkoa. Anaonekena aidha kama nilivyozungumza awali kwamba ana Halmashauri nyingi za kuhudumia, kwa hiyo, anashindwa kuwa na ufanisi kiasi kwamba hasimamii vizuri maeneo haya ya miradi, inachukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninao mradi wa kutoka Gorogoro, Manoro hadi Kijiji cha mwisho ambacho ni Madala, eneo la mradi ni kilometra 54, lakini sasa nazungumza hapa ni mwaka wa tatu, bado kasi ile hairidhishi. Nitoe rai sasa kwamba wasimamie kwa kina kwamba tunapo...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzunguzaaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Haya. Mheshimiwa Heche. Mheshimiwa Gekul na Mheshimiwa Rashid Abdallah wajialande.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii ili nami niweze kuchangia kwa mwaka huu wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu wananchi wa Tarime wanichague nimekuwa na miaka mitatu hapa Bungeni. Nimejifunza mambo mengi sana na wakati mwingine fikra nilizokuja nazohapa na kitu ninachokiona kinafanywa hapa ni tofauti kabisa na inasikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1994 Rwanda iliingia kwenye machafuko makubwa sana yaliyosababisha mauaji ya zaidi ya watu milioni moja. Ukiangalia na ukifuatilia mauaji yale, kulikuwa na visasi, kupuuuzwa watu, watu kuonewa, *double standard* na watu wakafika sehemu wakachoka kweli kweli, yakatokea matatizo makubwa kama yale. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hapa Tanzania kule Musoma mwaka 2010 yaliwahi kutokea mauji mabaya ya kulipiza kisasi. Watu zaidi ya 16 kwenye familia moja wakauawa, wengi mnajua. Mbuzi wakauawa, ng'ombe, mpaka kuku na mbwa wakauawa kwa sababu ya visasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nchi hii watu wanapigwa kwa sababu wengine wanafikiri wako salama na kwa sababu wanafikiri wako kwenye madaraka, wanaona ni sawa hawa kufanyiwa hivi. Katibu wetu wa Kata ameuawa, watu wanaona ni sawa. Tundu Lissu amepigwa risasi, watu wanaona ni sawa; watu wanaonewa, mnaona ni sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wengine tunajua tuko kwenye *list* ya kuumizwa. Sisi wengine tumeziambia familia zetu kwamba hata kama ni baada ya miaka 10 kwa watu watakaotufanya ubaya, lazima familia zao ziwjibike. Hili liwe kwenye *record* kabisa. Hatuwezi kuwa kwenye nchi ambayo imejaa upendeleo, *double standard*. Tunazungumza kuhusu utawala bora hapo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza kuhusu utawala bora. Utawala bora tunaouzungumza Mzee Mkuchika ni utawala wa aina gani? Utawala ambaeo leo mnakamata mtu, Polisi wanazungumza kwamba huyu mtu amejiteka, lakini yeze mnamuia kuwaambia Watanzania kwamba yeze hakujiteka au alijiteka. Utawala bora upi? Utawala bora leo tunajua, Serikali leo duniani ni chombo cha mabavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza Bunge ndiyo chombo cha wananchi, dunia nzima ndivyo ilivyo. Leo mtu anatoa *opinion* yake kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 18 anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake. Jambo tunalopaswa kufanya kama Bunge ni kumjibu kwamba hili Bunge haliko hivyo kwa kuandika makala kinzani. Au huyu mtu mnafikiri kwa nini anatuona hivyo? Kwa nini hakuliona hivyo Bunge la Mama Makinda? Kwa nini hakuliona hivyo Bunge la Mzee Sitta? Kwa nini hakuona hivyo katika Mabunge mengine? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili likiwa sehemu ya kutoa hukumu kwa watu wanaotutazama nasi hatuwezi kulazimisha kila mtu atuone kama tunavyojiona. Watu wana haki ya kutuona tofauti. Kila mtu ana macho yake na wewe utaona umevaa suti umependeza, mwingine atakwambia hujapendeza umevaa suti mbaya. Kwa hiyo, huwezi kuanza kumchapa kwamba amekwambia umevaa suti mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri kama Taifa, nasi tunaongea hapa, watu wanafikiri sisi ni walalamikaji. Tumewaambia mambo mengi. Mwaka juzi mligusa hapa sukari, "oh, sukari, watu wanaingiza sukari, sijui sukari, sukari! Tutaishusha bei! Sukari imepanda kutoka Sh.1,800/= aliyoiacha Mheshimiwa Kikwete, leo ni Sh.2,800/=. Mnajifanya kama hamjui, yaani mmejisahaulisha. Eti mmejisahaulisha kwamba sukari haijapanda bei. Yaani mnafikiri Watanzania hawawaoni. Hakuna anayezungumza, yaani mmejisahaulisha tu, hamjui kwamba sukari hii mlitibua bei nyie. Tukiwaambia, ooh, hawa ni watu wabaya. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo miaka 50, maendeleo, maendeleo; na *Maaskofu wamezungumza juzi, mnawatukana na viongozi wa Makanisa*. Tuna Kata 4,220 kwenye nchi hii. Kwa mujibu wa Sera ya Afya ya Taifa hili ambayo imetengenezwa na nyie CCM, sisi hatujawahi kuingia madarakani. Sera yenu nyie hapo inasema, kila Kata iwe na Kituo cha Afya. **[Maneno haya sio sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwenye kitabu, msije mkasema maneno ya Heche; kitabu chenu hiki hapa cha Mheshimiwa Waziri Jafo, cha sasa hivi; Vituo vya Afya tunavyo asilimia 15. Yaani kati ya vituo 4,220, tuna vituo 696. Hapo hatujazungumzia ubora wake, hatujazungumzia vifaa vyake, hatujazungumzia wahudumu, 696 na *viongozi wa dini mliowatukana* kati ya hivyo vituo 600, vya kwao 183. Ooh, maendeleo, ooh *Stieglers Gorge*, ooh reli, sijui *SGR...* (*Makof!*) **[Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Mheshimiwa John Heche, naelewa uko kwenye kasi kali, lakini hebu tusikie taarifa au Mwongozo...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

TAARIFA

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimeona kwamba mchangiaji anawazungumzia wenye hoja kwamba wamewatukana Mababa Askofu. Nataka ufanuzi kama hilo jambo ni la kweli au la.

MWENYEKITI: Waheshimiwa...

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, unasema jambo lisilo sahihi. Kanuni ya 64. Kwa hiyo, natamani tu kujua kwamba kama jambo hilo lina ukweli au la.

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Engineer* Manyanya, nakushukuru sana. Amesema kuhusu utaratibu kwenye kanuni ya 64.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Ah! Ah! Waheshimiwa Wabunge tuwe na staha tu na ndiyo tunaomba kila siku. Kuteleza siyo kuanguka. Amemalizia vizuri sana, Kanuni ya 64 (1) lazima ibebe yote yale.

(Baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Sasa narudia. Nami naendesha kikao hiki na wale ambao mnadhani mna kauli nzuri, si mimi ndio nina orodha hapa. Mimi ndiye mwenye orodha hapa. Mimi ndio nimeshika mpini. Tuelewane hivyo. *(Makof)*

Mheshimiwa Heche, changia kwa ustaarabu tu, twende mbele. Wewe changia unachoona kinafaa kwa hoja zilizo mbele yetu hapa. Usiseme sijui tulifanya Maaskofu wamefanya nini, wewe sema cha kwako.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtemi nakuamini, nakushukuru sana. Naomba niendelee. Mama nafikiri nikimsema itakuwa mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema, Mwalimu Nyerere ambaye ni Muasisi wa Taifa hili kama hamumheshimu, aliwahi kusema maendeleo ya vitu siyo maendeleo ya watu. Maendeleo ya watu ni pamoja na watu kuwa na afya. Mimi nawaambia CCM nyie mnaopiga kelele, Vituo vya Afya tangu uhuru kati ya 4,420 mna Vituo vya Afya 696.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mionganoni mwa hivyo Vituo vya Afya kwa mujibu wa kitabu hiki cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, 183 ni vituo vya Makanisa na madhehebu. *(Makof)*

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Taarifa, taarifa.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema, kama ni kujenga reli, Wakoloni walijenga hata kabla ya uhuru.

MWENYEKITI: Ngoja, ngoja. Taarifa.

(Hapa baadhi wa Wabunge waliongea bila mpangilio)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji anayesema kwamba maendeleo ni mchakato na hii pia ni kauli ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwamba maendeleo ni mchakato. Maendeleo hayatokei siku moja. Kazi ya Serikali yoyote ile inayowekwa madarakani ni kuendesha na kusimamia mchakato wa kuleta maendeleo na mchakato huo hauishi siku moja.

MWENYEKITI: Kwa kifupi tu.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Kwa hiyo, mchakato wa kujenga Vituo vya Afya bado unaendelea, lakini katika Awamu hii ya Tano, napenda kumpa taarifa kwamba wakati Serikali inaingia madarakani kulikuwa kuna vituo 113 tu vyenye uwezo wa kufanya upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni. Leo hii ninavyozungumza hapa, nafarijika na kutembea kwa majivuno kwamba takriban Vituo vya Afya vilivyoongezeka kutoka 400 vilivyokuwepo wakati Awamu ya Tano inaingia madarakani vimefikia takriban 700 na katika hivyo, Vituo vya Afya zaidi ya 600 vinatoa huduma za upasuaji wa kutoa mtoto tumboni.

MWENYEKITI: Unachangia!

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Taarifa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima zote. Sisi tuna muda na Serikali ina nafasi ya kuja kujibu. (*Makof*)

Ni mahali ambapo Mbunge anapotosha makusudi ndio unaweza ukatoa taarifa hiyo. Sasa hivi mnatulia muda mwiningi sana. Taarifa hizi jamani zinakula muda wangu, tunataka wengi wachangie.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Kigwangalla unatutia aibu Waislamu wenzako. (*Kicheko*)

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *You are always firm.* Nasema hivi, miaka 59 vituo vya Serikali 513; ili tujenge vituo 4,422 tunahitaji miaka 600. Mnahitaji mtoke madarakani nyie. Ndicho ninachosema hapa, *a simple logic.* (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunakuja hapa mtu anatuambia *SGR*. Wakoloni walijenga reli hii. Wakati ule ndio ilikuwa *standard gauge* ya sasa hivi, wakati wakoloni wanajenga ile (Wajerumani). Watanzania na Watanganyika walikataa kwa sababu walikuwa wanawa-*oppress*. Kitu ambacho mnafanya nyi, leo mnatu-*oppress*. Sisi tukizungumza kuhusu nyie mnatuweka Polisi, mnatupeleka Mahakamani. Mheshimiwa Rais akizungumza kuhusu sisi, mkitukashifu, nyie hakuna pa kupelekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio tunasema, hata watu wa Afrika Kusini walizungumza na Makaburu wakawaandikia barua, wakafanya nini, lakini ilifika sehemu wakaunda MK kukataa ushenzi uliokuwa unafanywa na Makaburu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachozungumza hapa ni kwamba ni lazima tuheshimiane. Ni lazima tuelewe; leo unamshtaki Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbewe, Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, mimi na Mheshimiwa Ester, eti sisi tulisababisha kifo cha mtu (Akwilina). Yule Mkurugenzi aliyetunyima viapo ambavyo viro kwa mujibu wa sheria, alisababisha nini? Haya mambo ndio tunayozungumza.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Ahsante, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Pauline Gekul atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Abdallah.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niseme machache katika Wizara hii muhimu sana kwa maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme kwamba Mwongozo ulioombwa asubuhi na Mheshimiwa Waitara kuhusu Sekretariet ya KUB kuondolewa Bungeni ni Mwongozo ambao hautakiwi kuendelea kupewa siku. Hili suala linatakiwa lijadiliwe kwa dharura ili haki itendeke katika Bunge hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkiendelea ku-*delay*, mkidhani kwamba...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gekul, yaani unahoji Mwongozo niliota? Unahoji wewe? Hebu changia hoja yako.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa afya ya Bunge hili ni vizuri mkafanya maamuzi mapema ili hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani iwepo Bungeni na Watanzania watendewe haki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nategemea kubomoka sana. Sasa kabla sjabomoka, naomba nishauri machache ambayo nikibomoka baadaye hamtonisikia. Naomba nishauri kuhusu suala la *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba mna barabara nchi hii za kilometra 108,000 vijiji na mijini, lakini *TARURA* hii mpaka leo kwenye

shilingi bilioni 230 mmewapelekea shilingi bilioni 98, wamejenga kilometa 4,000 tu kati ya 34,000. Naomba majibu, ni kwa nini tunatengeneza vitu halafu pesa hampeleki? Kuna uhalali gani wa ninyi kuendelea tu kwamba bajeti nzuri wakati ukweli ni kwamba fedha hazipo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nishauri tu kwa nia njema. Mfuko wa Bima ya Afya sasa hivi mtu mmoja hawezi akapata ile Bima kubwa akatibiwa kwenye Hospitali ya Rufaa kama Muhimbili na maeneo mengine, ni lazima awepo kwenye *group*. Naomba nishauri, ile Bima ya shilingi 76,000 muifanye kwa mtu mmoja mmoja angalau wananchi watibowi, siyo lazima wawe kwenye *group* ili isaidie Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, nishauri kuhusu suala la elimu bure. Mmeanza elimu bure, elimu bila malipo, sijui kitu gani na kitu gani. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku- *wind-up* atuambie fedha za walinzi, maji, umeme wameziweka wapi? Kwa sababu kwa sababu walinzi wameacha shule zetu na madawati yanaibiwa na hata fedha za elimu bure bado hawajazongeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nashauri kuhusu mikopo ya vijana na akinamama. Wamefanya jambo jema kuondoa riba ya asilimia 10, ni jambo jema wala hatukatai. Hata hivyo, ni nani aliywelalalamikia kwamba tatizo ni riba? Tatizo ni Halmashauri kutokontakte fedha. Katika bajeti hii iliyopita, kati ya shilingi bilioni 61 ni shilingi bilioni 15 tu zimepelekwa, 9% ndiyo zimetengwa kwa vijana na akinamama. Tatizo siyo riba, tatizo ni fedha hazipeclekwi na Halmashauri hawana vyanzo. Badala ya *ku-tackle* tatizo, mnakuja na maneno mazuri mazuri ya kufurahisha Watanzania, ham-solve tatizo! Atuambie kwa nini fedha hazipeclekwi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, wazee wamewasahu. Wamewapatia walemau, *it is okay*, nami nawapongeza; lakini akinamama na vijana wamebakiwa na asilimia nne nne. Ushauri wangu ni kwamba wachukue

2% wawapatie wazee ili na wao katika nchi hii waone kwamba wamewakumbuka, maana kipindi cha Awamu iliyopita ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete waliambiwa watapewa hata *token amount* kwa mwezi. Mpaka leo hawapewi, lakini hata kwenye hizi fedha hawakumbukwi. Sasa wawatengee na wao 2%. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nibomoke. Utawala Bora katika nchi hii tunapoongea msituone maadui. Hii Tanzania ni ya kwetu sote. Tunatamani kila Mtanzania mmoja wetu aheshimike kwa nafsi yake, atendewe haki kwa nafasi yake; kila mmoja awajibike kwa mujibu wa taratibu na sheria za nchi hii ambazo tumejiwekea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mbunge mmoja wa Mkoa wa Manyara anasema kifua kinamuumma. Wakati anachangia asubuhi, anasema mimi kifua changu kimejaa, kinauma, naomba tu mengine niya-save kwenye kifua. Naomba nisiumie kifua, leo nibomoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa Wakuu wa Mikoa ambaao mmekuwa mkiwateua bila kuangalia ame-serve kwenye *public service* kwa muda gani mnawatoa kwenye Vyama vyta Siasa, mnawaleta mnawapa nafasi za kuongoza Halmashauri na Wilaya zetu, wamekuwa wakifanya mambo ya ajabu hajjawahi kutokeea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kwa Tunduma, siyo kwa Mkoa wetu wa Manyara, siyo kwa Hanang ambako hata mzee wetu, Mama Nagu anawekwa ndani, lakini ni Wakuu ambaao wamekuja kufanya kazi ya siasa, siyo kazi ya maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lilitokea tatizo kubwa sana katika Mkoa wetu wa Manyara. Stendi ya mabasi ambayo Mheshimiwa Waziri anasema kwamba tukusanye ushuru, ilikabidhiwa CCM mwaka huu. Stendi ya mabasi ambayo Halmashauri tunakusanya ushuru wa zaidi ya shilingi milioni 10, imekabidhiwa CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 13 Januari, 2018 tuliiwa kwenye Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Kamati ya Fedha, Kamati ya Ulinzi na Usalama *DC*, pamoja na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa. Tukaambiwa na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, kuanzia hivi ninavyoongea na ninyi hapa tulipo, tumekaa tangu asubuhi na siku ile Mheshimiwa Lukuvi alikuja, akatuacha pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu asubuhi tumekaa, saa 8.00 anakuja anatuita anasema, nimeagizwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nendeni mkakabidhi Stendi Kuu ya Mabasi ya Babati kwa CCM.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Taarifa.

(Hapa baadhi ya Wabunge wallongea bila mpangilio)

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, tukawa *shocked*. Tukauliza, tunaomba utupe utaratibu.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mama tulia hebu, nichangie mambo ya Babati.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Pauline ni Mbunge kama mimi wa Jimbo la Babati, nami Jimbo la Hanang. Nataka nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, ile stendi ya mabasi ilikuwa ya Chama cha Mapinduzi miaka mingi iliyopita. Chama cha Mapinduzi kikaachia stendi ikatumika kwa miaka mingi, lakini imefika mahali ambapo wametaka stendi irudi kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Waheshimiwa tusipotoshe wananchi kwa sababu, kwa kweli, stendi ile ni ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Mheshimiwa Gekul anasema mimi nimewekwa ndani. Pamoja na kwamba walitaka kuniweka ndani, sikuingia ndani. (*Kicheko/Makof*)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Gekul. Naomba utulivu Bungeni. *Please, order!*

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muda wangu ulindwe. Huyo ni mama yangu, sina sababu ya kumjibu. Naomba niendelee tu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulivoitwa tukatakiwa tukabidhi stendi, labda nimsaidie tu, yeye haingii kwenye Baraza la Madiwani la Mji wa Babati. CCM hawajawahi kuomba kumilikishwa stendi, hata ombi tu, acha kumilikishwa, hawajawahi kuomba. Kwa hiyo, kilichotokea, tukatoka hapo tukarudi kwenye Halmashauri yetu. Terehe 2 Machi, wakati tumeondolewa hapo hatukuruhusiwa hata kuhoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipohoji Barua ya Mheshimiwa Rais iko wapi? Tulijibiwa, Mheshimiwa Mkuu wa MKoa akasema, Mheshimiwa Mbunge, sifanyi masuala ya kitoto. Nikamwambia, Mheshimiwa Rais kama anataka kukabidhi stendi CCM, anaandika kwako. Tuoneshe hata tuone. Akasema atatuletea kwenye Baraza la Madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Baraza la Madiwani, hatukuletewa barua wala Kumbukumbu Namba ya Barua ya Rais ya kukabidhi stendi, mali ya wananchi kwa CCM. Tukakatazwa kujadili kwenye Baraza la Madiwani. Nchi hii hakuna utawala bora. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyekiti wa Halmashauri akaandika barua tarehe 2 kumtaka Mkurugenzi Baraza Maalum, Waziri wa TAMISEMI anijibu, tangu lini Baraza la Madiwani linakatazwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkurugenzi akakimbia akaenda kwa Mkuu wa Mkoaa, akapeleka barua tarehe 5, anaomba mwongozo kwa Mkuu wa Mkoaa kana kwamba hajui kazi yake kama Mkurugenzi. Mkuu wa Mkoaa tarehe 6 akajibu akasema haoni mantiki ya Baraza la Madiwani kujadili amri ya Mheshimiwa Rais. Hivi mna utawala bora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 8 Mwenyekiti akaandika mwezi wa Tatu tunaomba tukae tujadili, hiki ni chanzo kikubwa. Wakasema, *shut up*. Hakuna kujadili. Tukaomba, Mwenyekiti wa Halmashauri na Madiwani waende kwa wananchi kwamba stendi yetu imepokonywa na CCM. Polisi wakakataza wasiende kwa wananchi wawaambie kilichotokea. Kuna utawala bora? (*Makof!*)

WABUNGE FULANI: Hakuna.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kubomoka. Sasa Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora mnijibu yafuatayo:-

Ni kwa nini barua ya Mheshimiwa Rais ninyi Mawaziri hamkupewa nakala? Kwa nini anaandikiwa Mnyeti? *Hierarchyya information* katika nchi hii ninyi ni Mawaziri, kwa nini ninyi hamjaandikiwa, mnijibu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kwa nini mmeshindwa kumshauri Mheshimiwa Rais kwamba CCM; maana sisi tulioitwa kwenye Baraza, mchakato wa muda mrefu, walitunyang'anya kwanza uwanja wa wanafunzi ekari nane tukaurudisha. Tena Katibu Mkuu wa TAMISEMI ananisikia yuko humu ndani. Barua yake ikapuuzwa, Mkuu wa Mkoaa anasema hatambui barua ya Katibu Mkuu kwamba uwanja ni wa wanafunzi. Tulivyozuia uwanja, wakatunyang'anya stendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini ninyi Mawaziri mnaogopa kumshauri Rais? Kama alivyosema Mheshimiwa Malocha hapa, kwa nini mnaogopa kumshauri Mheshimiwa

Rais wakati amelishwa matango pori? Naomba mnijibu, ni kwa nini ninyi mnakubali chanzo kikubwa cha Halmashauri kama hiki kinachukuliwa na ninyi mkiwa mnaangalia? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mnijibu yanayoendelea Babati, kwa sababu kengele imelia. Sasa hivi kinachoendelea, CCM walivyokabidhiwa stendi, wale wafanyabiashara ambao wana mkatiba wa miaka 31 mpaka 2031 na Halmashauri wameambiwa ninyi sio wamiliki, wapangaji ndio wamemilikishwa. Sasa hivi kuna vita Babati kati ya wapangaji na wamiliki wa vibanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, Mawakala wa Halmashauri wanaokusanya ushuru wa Halmashauri walifukuzwa kama mbwa, stendi pale CCM wamepeleka *green guard*. Huu ubabe wa CCM mpaka lini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara wamepeleka *notice* wiki ya pili wanaishtaki Halmashauri. Hiyo fidia ya kuwalipa wafanyabiashara kupoteza vibanda vyao tunatoa wapi? Mawakala wameishtaki Halmashauri wamepeleka *notice* ya mwezi mzima, *according to sheria*. Wiki ya pili sasa, mnategemea tutalipa hizi fidia kutoka kwenye chanzo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba leo vyombo vya habari, usalama wa Taifa, mkamwambie Rais, Mheshimiwa Dkt. John Magufuli kwamba Babati kumechafuka. Kwa sababu ninyi mnaogopa kumshauri Rais, tunamtaka Mheshimiwa Dkt. Magufuli aje ajibu Babati, ni kwa nini anachukua stendi ambayo tumemiliki tangu mwaka 2004 mpaka leo wanakabidhiwa CCM? Mungu alivyo mwema, Ofisi ya Mkoa CCM na Wilaya wameanza kupigana kwa sababu ya shilingi milioni 10. Vita vimehamia ndani sasa hivi wanagawana ruzuku. (*Kicheko/Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Kuhusu Utaratibu.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, hatari iliyoko Babati leo, wamiliki wa vibanda...

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Kuhusu Utaratibu.
KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwelewa sana Mheshimiwa Mbunge. Naomba niombe tu jambo la utaraibu kwa Kanuni ya 68(1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani siyo sahihi sasa Mheshimiwa Mbunge anapoendelea kuzungumzia jambo hili wakati anajua Kanuni ya 64(1)(e), hatakiwi kuhalalisha jambo lake kwa kuzungumzia mwenendo wa Rais kwa kutaka Rais sasa ye ye eti ndiye aende akajibu kule...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, mimi ndiye nitakayetoa *ruling*. Kama tutakuwa na wasiwasi na maneno yaliyotumika, *Hansard* ipo. Eeh.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwa kweli, siyo sahihi kwa mujibu wa kanuni zetu. Nadhani ingetosha tu mchangaiji aendeleee kuchangia hoja yake kwa kuhusisha mchango wake na hotuba iliyoko mbele ya Bunge letu ikiwasilishwa na Waziri mhusika ambaye ndiye mwenye wajibu wa shughuli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tu utaratibu wa kikanuni uendeleee kuchukua nafasi yake ndani ya Bunge letu.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Unampa nani? Mimi?

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kwa Mheshimiwa Waziri.

MWENYEKITI: Ameshakaa. Huwezi kumpa taarifa Mheshimiwa...

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisimama hukuniona.

MWENYEKITI: Mheshimiwa ameshakaa. Mheshimiwa Zitto nawe sasa unaanza kuwaje bwana? Wewe ni mzoefu, twende vizuri tu.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 64(e) ambayo inatutaka lugha zetu tusitumie hayo ya kutaka kutumia jina la Mheshimiwa Rais kama kushawishi kitu. Ili tusilikuze jambo hili, ndio maana nilikuwa namsikiliza sana Mheshimiwa Gekul, ulisema unataka kufunguka, sijui umetumia maneno gani? Kupasuka kifua sijui!

Nakuomba Mheshimiwa uchangie tu umalize hoja yako ili ujumbe ufike kwa Serikali kwa suala ambalo unataka kulisemea. Kama utaliendeleza hilo, narudia, mimi ndio nimeshika mpini. Sipendi sana tuumizane kwa sababu ya kanuni. Tukichangia kwa staha kama tunavyotakiwa na kanuni hizi, tutaenda vizuri na ujumbe utafika, lakini ufike kwa lugha ya Kibunge.

Waheshimiwa Wabunge, ni hicho tu ninachoomba. Malizia muda wako Mheshimiwa Gekul.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru...

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Kuhusu Utaratibu.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(1).

MWENYEKITI: Aah, hiyo, Mheshimiwa.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Ndiyo, nataka kueleza.

MWENYEKITI: Ngoja, ngoja. Kanuni ya 68(1) ni ya kuingia tu, halafu uniambie *straight* ni Kanuni ipi ambayo imevunjwa? Ukipatafanya hivyo, ndiyo nitakupa nafasi. Haya.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge wa Jimbo la Babati MJINI anamwongelea Waziri wa TAMISEMI. Waziri wa TAMISEMI nchi hii ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Waziri aliyesoma hoja hapa ni Waziri wa Nchi na sio Waziri wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mbunge wa Babati MJINI yuko sahihi kumtaka Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aende Babati akaeleze ana mamlaka gani ya kunyang'anya uwanja wa wananchi na kukipa Chama cha Mapinduzi? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zitto Kabwe, kwa ombi lako Kuhusu Utaratibu, kwa tafsiri ya mgawanyo wa majukumu ya Rais ambayo ni yote; Serikali ni yake yeye, ila kwa mujibu wa *Presidential Affairs* anaweza akagawa kwa jinsi anavyoona inafaa. Ukiisoma *instrument* ile amegawa majukumu yanayohusu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, amekasimu kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. (*Makofii*)

Rais yeye ndio ni Waziri wa TAMISEMI. Ndiyo. (*Kicheko/Makofii*)

Hata hivyo, Rais hawezi kwenda kila mahali eti kwa sababu kuna tukio limetokea. Waziri aliyekasimiwa hayo na wasaidizi wake ndio watafanya hayo. Huo ndio uamuzi wangu, tuendelee. (*Makofii*)

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muda wangu ulindwe sana.

MWENYEKITI: Una dakika mbili tu.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimesema wafanyabiashara na wapangaji wamegonganishwa; wamiliki wamenyang'anywa, wapangaji wamekabidhiwa vibanda, moto unafukuta, lakini inawezekana hata mali za wafanyabiashara zikachomwa moto kwa sababu walitolewa wana uchungu na vibanda vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fukuto lingine, CCM wanagawana hiyo ruzuku ya shilingi milioni 10, moto umewaka kati ya mkoa na wilaya, wanapigana vikumbo. Vile vile Halmashauri imeshtakiwa na Mawakala kwa kuvunja mkataba; Halmashauri imeshtakiwa na wananchi kwa stendi yao kukabidhiwa CCM; na Halmashauri imeshtakiwa na wamiliki wa vibanda wenye mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu hii hoja tunaambiwa ni barua ya Rais. Tunaiomba hiyo barua tupewe.

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, *group* la wazee wa CCM na wananchi wa Babati walikuja kumwona Waziri Mkuu mwezi wa Pili...

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Haya, nipe taarifa.

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mchangiaji anayechangia kwamba kinachoendelea Babati, kinaendelea siyo Babati tu, ni nchi nzima. Chama cha Mapinduzi...

MBUNGE FULANI: Kanuni gani?

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, 68(8), taarifa. (*Kicheko*)

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Mapinduzi...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge! Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, hebu waambie wenzako hapo.

Mheshimiwa endelea, toa taarifa kwa kifupi tu.

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa kwamba Chama cha Mapinduzi kimeanza mchakato wa kuhakiki mali zake nchi nzima. Kinahakiki na kurudisha mali *regardless* kama ipo kwenye mikono ya Halmashauri au mtu binafsi. Kwa hiyo, kinachoendelea Babati ni sahihi kabisa. Mali zote zilizochukuliwa za Chama cha Mapinduzi ziko kwa mtu binafsi au Halmashauri zitarudishwa.

MBUNGE FULANI: Taarifa.

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nimpe taarifa mzungumzaji.

MBUNGE FULANI: Taarifa.

MWENYEKITI: Huwezi kutoa taarifa juu ya taarifa.
Please.

MBUNGE FULANI: Kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Nakuomba ukae. Mheshimiwa kaa chini. Nakuomba ukae chini Mheshimiwa.

MBUNGE FULANI: Kwani huyo Mbunge wa wapi anayesema hivyo? (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Tusifanye mizaha kwenye nyumba ya Watanzania. Eeeh! Huwezi kutoa taarifa juu ya taarifa.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naoma unisamehe.

MWENYEKITI: Haya. Mheshimiwa, taarifa hiyo unasemaje?

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, *no research, no right to talk*. Sisi ndio Baraza la Madiwani tunaopokea maombi ya yeoyote anayeomba ardhii awe CHADEMA, awe CCM. Sasa wewe unayeongea huko ulikuwepo kwenye Baraza au kwenye Kamati ya Mipango Miji? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawajawahi kuomba wala hawajawahi kumiliki. Naomba *record* iwe sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuja kumwona Waziri Mkuu, Mwenyekiti wa Halmashauri na Madiwani na wazee; akatukaribisha vizuri miezi miwili iliyopita, akasema atapeleka kwa Mheshimiwa Rais. Mpaka leo hakuna majibu. Maana yake kama inafikia hatua mpaka *level* ya Waziri Mkuu tunakuja hamtupi majibu, halafu tunaambiwa kuna barua ya Mheshimiwa Rais; hivi barua ya Mheshimiwa Rais kwa rasilimali ya nchi ni siri? (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Muda wako ndiyo huo. Mheshimiwa Rashid Abdallah.

MHE. RASHID A. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia leo hii kusimama hapa nikiwa na afya. Pia, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAMISEMI ndiyo roho ya nchi hii na Watanzania wote...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu hapo.

MHE. RASHID A. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wote wamo kwenye TAMISEMI. Nachukua fursa hii, katika uhai wangu wa miaka nane sasa ya Bunge, kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na Naibu Mawaziri wake kwa kazi ambazo wanazifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, natoa ushauri kwamba wale Wakurugenzi wa Halmashauri wapewe nafasi ya kupewa zawadi maalum kwa wale wanaofanya vizuri na kama inawezekana kwa kila bajeti waweze kutangazwa Wakurugenzi ambao wamefanya vizuri katika Halmashauri zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni pongezi tu. Leo nitahamia kwenye utawala bora zaidi. Duniani kote tunahitaji utulivu, amani na demokrasia ya kuendeleza uchumi wa Taifa. Kama hatutaweza kudumisha utawala bora, hatutaweza kabisa kuendesha Taifa hili. Utawala bora kwa tafsiri yake, umeenea kila pembe ya Taifa hili. Kwa umuhimu wa utawala bora, nimeamua leo nijikite kwa makusudi kujadili kwa undani zaidi kuhusu shughuli za Serikali yetu juu ya utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu wa utawala bora ndiyo maana katika Dua yetu tunayoliombea Bunge na Taifa huwa tunasema "Mjalie Rais wetu pamoja na wanaomshauri wadumishe utawala bora." Hii imeingizwa

katika Dua ili wanaomshauri wawe karibu kumwambia Rais ajitahidi kusimamia na kutekeleza utawala bora katika Taifa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, niseme utawala bora ni kusimamia Katiba na Sheria ya nchi. Utawala bora ni kusimamia utawala Sheria; ni kusimamia demokrasia ya kweli; ni kusimamia misingi mikuu ya uchumi ili kuendeleza Taifa hili; na kusimamia haki, usawa na uwajibikaji. Tukifika hapo sote, basi tutakwenda vizuri, wala hakutakuwa na mivutano katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba yetu sasa kuna dalili zote za kuchezewa chezewa. Demokrasia hasa ya vyama vingi inapigwa vita na kushambuliwa kabisa. Yote haya yanaleta athari kwa Taifa letu. Kwa maana hiyo ile kasi ya maendeleo ya haraka inakwama sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu kwa heshima yako nisome maelezo ya aliyekuwa Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora wa 2014 na 2015 Mwenyekiti wangu Mheshimiwa Mkuchika. Alisema hivi, migogoro ya ardhi, mauaji ya *albino* na vikongwe, wananchi kujichukulia sheria mikononi, rushwa pamoja na ujangili, vimesaidia kwa kiasi kikubwa kuporomoka kwa Tanzania katika kiwango cha utawala bora duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliendelea kusema kwamba Tanzania ilikuwa ikishika nafasi ya 10 katika miaka miwili iliyopita na kuongeza kwamba kuperomoka huko kumekithiri kwa ukiukwaji wa haki za binadamu. Aliendelea kusema kwamba duniani tuko katika nafasi ya 102 kat i ya nafasi 176. Hii ni nukuu ya Mheshimiwa Mkuchika alipokuwa Moshi alipokuwa akitoa maelezo yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimenukuu haya nikiwa najielekeza katika kitabu cha Mheshimiwa Mkuchika, kuona ni kiasi gani ameeleza katika kitabu chake hiki kuhusiana na matokeo mbalimbali yaliyotokea nchini mwetu. Jambo la kusikitisha kabisa katika ukurasa wa 112, alieleza mistari miwili

tu tena katika majumuisho. Kwa hiyo, sidhani kama ile Dua tunayosoma, sijui kama inatakabaliwa au kuna wachawi humu ndani au vipi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na makundi yanayofanya utekaji. Makundi haya toka yateke watu sijaona hata siku moja mtu mmoja kufikishwa Mahakamani. Nchi ambayo ina usalama wa uhakika na wa kuaminika kabisa, ni juzi tu vijana wetu kule Mtambwe sita walitekwa wakaenda maeneo yasiyojulika, wamerudi watatu wako taabani, wamepigwa na kuteswa na watatu hadi leo hawajaonekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utesaji na uuaji. Vitendo hivi vingi vinatokea sana katika nchi ambazo zina dalili ya kukosa utawala wa sheria. Vitendo hivi vya kivamizi ni ukiukwaji mkubwa wa sheria, ni uvunjaji wa amani na ni kinyume na haki za binadamu na utawala bora. Watu mbalimbali wanaotekwa hutekwa kwa sababu ya maoni yao au kujieleza kwao; na haki hii imelindwa chini ya Katiba ya Ibara ya 18; lakini haki hii pia imelindwa chini Mikataba ya Kimataifa Ibara ya 19 inayoshughulikia haki za kiraia na haki za kisiasa za mwaka 1986. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia haki hii imelindwa katika Ibara ya (9) ya Mikataba ya Kimataifa kuhusu Haki za Binadamu ya mwaka 1986. Kwa hiyo, sioni sababu yoyote kama kuna watekaji wanaowateka Watanzania, kuna wauaji wanaowaua Watanzania, hakuna hata mmoja aliyejohiwa na kupelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza hapa, hatuzungumzi kwa vyama, tunazungumza kama Wabunge na tunapozungumza hapa, tunaiambia Serikali, wanakoelekeea ni kubaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhuru una mipaka yake, lakini pale anapoonekana mtu amekwenda kinyume na sheria yoyote nyingine, sheria ichukue mkondo wake. (*Makofi*)

Hivi sasa kuna watawala, kuna wanasiasa hasa Wapinzani, kuna Wanahabari, kuna vikundi vyatya dini, kuna wafanyakazi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa. Muda wetu ni mdogo. Tunaendelea, nakushukuru kwa mchango wako. *(Makofii)*

MWONGOZO WA SPIKA

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jenista, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu.

WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 68 (7). Mwongozo wangu, najielekeza kwenye mijadala inayoendelea ndani ya Bunge na hasa tunapoingiza mijadala inayohusu masuala ya imani, viongozi wa dini, nyaraka ambazo zimekuwa zikitolewa na viongozi wa dini, lakini mwelekeo ambao labda viongozi wa dini wamekuwa nao kwa namna moja ama nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 19(1) na Ibara ya 19(2), ukipenda nivisome labda naweza kuvisoma lakini kama unaona muda hautoshi, niviache Waheshimiwa Wabunge wenye Katiba wanaweza kuvipitia. Nadhani kwa maslahi ya Mkutano wako, nivisome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 19(1) kinasema, "Kila mtu anastahili kuwa na uhuru wa mawazo, lakini hapo ndipo ninapokwenda uhuru wa imani na uchaguzi katika mambo ya dini, lakini pia mtu ana uhuru wa kubadilisha dini au imani yake." Pili, "kazi ya kutangaza dini, kufanya ibada na kueneza dini itakuwa ni huru na jambo la hiari la mtu

binafsi na shughuli ya uendeshaji wa Jumuiya za Dini zitakuwa nje ya shughuli za mamlaka ya nchi yetu." (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema, hoja ambayo iko ndani ya Bunge ni hoja ya Serikali ambayo inaongoza nchi hii. Napenda kujua kama ni sahihi sana Bunge lako linapoendelea na hoja hii na Katiba hii imetuelekeza kabisa kwamba suala la dini, ni kwamba Serikali yetu haina dini na wala haijihuishi na dini yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hivyo ndivyo kwa mujibu wa Katiba; na kwa kuwa hivyo ndivyo kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge; ninaomba kupata tu mwongozo wako kama ni sahihi mijadala inayoendelea ndani ya Bunge kuhusisha shughuli za kiimani au za imani tofauti ni sawa sawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa mwongozo na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, kuhusiana na baadhi ya matamshi yetu, hasa yanayogusa imani za dini ambazo watu mbalimbali wanazo na baadhi yetu humu.

Ingawa Mheshimiwa Waziri wa Nchi hakusema moja kwa moja ni matamshi yapi na ni Mbunge yupi aliyeyasema, kwa vile mtiririko wa wachangiaji tunao, mwongozo wangu kwa hilo ni kwamba, acha mchana huu tujiridhishe kuititia Taarifa Rasmi za Bunge, kama kuna Mbunge ambaye ametufikisha kule ambapo Katiba na Kanuni zetu za Bunge zinasema tusifanye hivyo.

Tukifika hapo na nikaridhika kwamba yalitamkwa hayo, kwanza nitaagiza kule kwenye *Hansard* yafutwe, lakini pia kama yalisemwa humu nami nikapitiwa, nitamwombwa Mheshimiwa Mbunge afute kauli yake humu humu Bungeni.

Huo ndio mwongozo wangu kwa hilo. Tupeni muda tutatoa baadaye baada ya kusoma *Hansard za proceedings za leo*. (*Makofii*)

Waheshimiwa tuna dakika kama tisa, napenda tutumie muda huu vizuri. Mheshimiwa Hasna Mwilima. (*Makofii*)

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema, maana ninyi wote ni mashahidi, nimetembelea magongo hapa karibu miezi sita; lakini kwa vile Mheshimiwa Rais aliona kwamba afya yangu inatakiwa iimarieke ili niweze kuwatumikia vyema wananchi wa Jimbo langu la Kigoma Kusini, akanipa kibali cha kwenda tena kupata matibabu nje ya nchi na hatimaye leo namshukuru Mwenyezi Mungu naweza kutembea bila kutumia magongo yoyote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nishukuru hivi kwa sababu mambo yalikuwa mengi, wako waliofikiri sasa nitakufa na Jimbo litabaki wazi.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, anayepanga maradhi ni Mwenyezi Mungu. Unaweza ukamwona leo huyu ni wa kufa kesho na asife na wewe ambaye ni mzima ukafa ukamwacha yule mgonjwa anaendelea kuishi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba pia nimshukuru Mheshimiwa Rais, juzi wote tumeona kuititia Mfuko wa Falme za Kiarabu Mfuko wa *Abu Dhabi* tumepata karibu shilingi bilioni 33 kwa ajili ya ujenzi wa kilometra 51.1 kutoka Uvinza mpaka Malagarasi. Barabara hii siyo tu itakuwa ni faida kwa wananchi wa Jimbo la Kigoma Kusini bali pia itakuwa faida kwa Tanzania nzima kwa sababu malori yanayosafiri kuleta bidhaa kwenda Kongo na Burundi yanatumia barabara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa haraka haraka pia nichangie kuhusu elimu ya msingi na sekondari. Tumepokea shilingi milioni 144 nashukuru sana Wizara ya TAMISEMI kwa kutupatia pesa hizo ambazo zitatusaidia kumalizia majengo yanayojengwa na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna upungufu mkubwa sana wa Walimu. Sisi kwenye mgao tumepokea Walimu 32. Walimu 20 wanaume na Walimu 12 wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo lile ni kubwa, Halmashauri ile ni kubwa sana, ina mita za mraba 10,178 zaidi ya Mkoa wa Kilimanjaro. Mnapofanya mgao kwa Walimu, naomba Serikali iangalie Halmashauri ya Uvinza tofauti na Halmashauri nyingine, kwa sababu jiografia ni mbaya, kuna barabara ambazo hazipitiki. Kwa mfano, sasa hivi tuna mvua nyingi, Walimu hata wanapokuwa na mahitaji muhimu hawawezi kusafiri mpaka msimu huu wa mvua uishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunayo majengo ya maabara kwa muda mrefu yamesimama kwa ukosefu wa pesa. Kwa hiyo, naomba Wizara husika ituangalie kwa jicho la huruma ili tusirudishe nyuma jitihada za wananchi wetu wa Jimbo la Kigoma Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya afya. Naishukuru sana Serikali kwa bajeti hii, tumetengewa shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya uanzishwaji wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Kwa niaba ya wananchi wangu, natoa shukrani za dhati, lakini tunatambua hivi karibuni Serikali mmetuambia mtatuletea ramani ya ujenzi wa hospitali. Tunaomba mharakishe ili basi ujenzi huo tuweze kuanza mara moja baada ya kupitisha bajeti hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina vituo viwili vya afya; Kituo cha Kalya na Buhingu. Leo kumeulizwa swali hapa, Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI akajibu kwamba tulete barua ili waweze kutupatia Madaktari. Sisi tumepeleka barua tangu bajeti ya mwaka 2017/2018 kwamba tuna upungufu

mkubwa wa Watumishi Idara ya Afya na Idara ya Elimu Msingi na Sekondari. Cha kusikitisha, mpaka leo hatuna Daktari kwenye Kituo cha Afya cha Buhingu, hatuna Daktari kwenye cha Kalya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI leo hii naomba, naona anatembelea halmashauri mbalimbali, namkaribisha Halmashauri ya Uvinza. Aje atufungulie rasmi Kituo chetu cha Afya cha Kalya ili yeye mwenyewe ajionee kilometra 250 wananchi wanatembea kutoka Kalya mpaka Kigoma Mjini. Hali ni mbaya kwa kweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tumeona juzi, kwanza tumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Utumishi kwa kutupa ufanuzi kwa wale Watendaji wa Vijiji na Watumishi ambaao wamewekwa pbeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vibali hivi mnavyovitoa, mnatupa vibali kuajiri Watendaji wa Vijiji watano au sita au kumi, wakati tuna upungufu karibu wa Watendaji wa Vijiji 30. Tunaomba Wizara ya Utumishi iliangalie hilo tupate vibali ili tuweze kuajiri Watendaji wa Vijiji, Watendaji wa Kata na watumishi wa kada nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naishauri Serikali. Watendaji wa Vijiji wapo waliofanya kazi zaidi ya miaka 20 mpaka 30, leo wamewasimamisha kazi. Kule vijijini wanaojuu mazingira ya vijiji ni wale wananchi husika wa maeneo husika. Tunapotangaza ajira, wanakuja watu wa kutoka Kagera, Mwanza na kadhalika. Mazingira ya kule ni mabovu, badala yake wanaingia kwenye masuala ya rushwa na hawafanyi kazi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wawaangalie sana wale Watendaji ambaao wamefanya kazi zaidi ya miaka 20 ili wamalizie kazi na hatimaye waweze kustaifu vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie mfuko wa *TARURA*. Ni jambo jema...

TAARIFA

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

WABUNGE FULANI: Simama simama.

MWENYEKITI: Jamani, mnanielewa kuhusu mambo haya. Mheshimiwa taarifa.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba suala analogumza la Watendaji kusimamishwa kazi, Serikali nzuri, Serikali sikuvi ya Chama cha Mapinduzi imesikia kilio cha wananchi na kilio cha Wajumbe na imeshatekeleza na wamesharudi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nalipokea lakini nilikuwa naliangalia kwa mapana zaidi na nilishashukuru kwenye hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusiana na barabara. Jimbo langu hali ya barabara ni mbaya sana. Kwenye bajeti ya mwaka huu tumetengewa shilingi milioni 400. Hivi shilingi milioni 400 tunafanya kazi gani katika mtandao wa barabara wa Halmashauri ya Uvinza? Naomba *TARURA* waongezewe pesa ili tuweze kujenga barabara zetu za Jimbo la Kigoma Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona vile vile kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri amezungumizia namna ambavyo tunaendeleza miji kwa maana ya miji 161 iko kwenye hatua mbalimbali ya kufanywa iwe miji midogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Nguruka kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo, takribani sasa miaka 10 tumeomba mamlaka ya Nguruka iwe Mamlaka ya Mji Mdogo lakini hadi leo utekelezaji unakuwa mgumu kwa sababu Kata ya Nguruka ina vijiji viwili, Kata ya Itebula ina vijiji viwili,

tunawezaje kuunda Mamlaka ya Mji Mdogo wakati kuna wakazi zaidi ya 50,000 kwenye eneo moja? Naiomba sana TAMISEMI iliangularie hili jambo ili ituruhusu tuweze kuongeza kata na vijiji ili Mamlaka ya Mji Mdogo wa Nguruka uweze kuundwa na hatimaye shughuli za wananchi ziweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, nimalizie tu kwa kusema, naishukuru sana Serikali kwa mambo mbalimbali hususan miradi ya maji. Miradi ya maji ya Nguruka, Uvinza, Ilaghala, Kalya na Kandaga inaenda vizuri, watu wanakunywa maji. Mradi wa maji wa Rukoma ndiyo utekelezaji haujulikani, sasa ni zaidi ya miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Kwa asubuhi ya leo ndiyo mwisho wetu. Tutarejea jioni saa 11.00.

Mnajua muda, kanuni hizi ni nzuri tunapoositumia kwa sababu ya malengo yetu tofauti, inakula muda na ndiyo maana baadhi yenu leo hamtaweza kuchangia. Tumeshapoteza nafasi tatu.

Niwataje watakaoanza mchana huu. Mheshimiwa Omary Mgumba, Mheshimiwa Mussa Sima, Mheshimiwa Almasi Maige, Mheshimiwa Jitu Soni na Mheshimiwa Zitto Kabwe. Watano hao wa kwanza.

MBUNGE FULANI: Hakuna wanawake?

MWENYEKITI: Mimi iwe wanaume au wanawake, wote ni Wabunge. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

(Saa 7.00 mchana Bunge lilitishwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Niliwataja wachangiaji wetu watano wa kwanza tunaanza na Mheshimiwa Omary Mgumba atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Sima na Mheshimiwa Almas Maige ajiandae.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi jioni hii nami niwe mchangiaji wa kwanza kutoa mchango wangu katika hoja iliyopo mbele yetu ya Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha uhai na uzima tumeonana jioni hii ya leo. Katika mchango wangu wa kwanza ninaishukuru Serikali kwa utendaji mzuri ambao wanaufanya na wanatutumikia watu wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nichukue nafasi hii kuwapa pole sana wananchi wa Kata ya Matombo, Halmashauri ya Morogoro Vijiji na wanachama wa CCM kwa ujumla kwa kuondokewa na Diwani wetu wa Viti Maalum asubuhi hii ya leo, Mheshimiwa Zuhura Mfaume aliyetangulia mbele ya haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwape pole wananchi wangu wa Kijiji cha Kisanga Stendi, Kata ya Tununguo, Taraifa ya Ngerengere ambao siku mbili zilizopita walivamiwa na majambazi na ndugu Mbaga amefariki dunia kwa kupigwa risasi na watu wengine sita wamepigwa risasi ni majeruhi bado wapo hospitalini. Waliotangulia mbele ya haki Mwenyezi Mungu awape mapumziko mema na wale ambao wako kwenye majeruhi wapate nafuu wapone haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba nilitoa pongezi za awali lakini kuna watu wengine wanaona kwamba labda tuktoa pongezi ni kama kuipendeleza Serikalini au tunataka tuipake mafuta Serikali yetu, lakini mimi

kama mwakilishi wa Morogoro Vijiji na watu wa Morogoro Vijiji tusipoishukuru Serikali hii ya Awamu ya Tano tutakuwa hatujatenda hakli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni mzoefu ni mmoja wa wakongwe nchi hii, unafahamu Morogoro ilikuwa ndiyo mji wa viwanda pamoja na Tanga, ilikuwa ni ndoto za Mwalimu Nyerere na Mwalimu Nyerere ndiye alikuwa Mbunge wetu wa kwanza Mkoa wa Morogoro, wa pili alikuwa Ndugu Kambona, tatu alikuwa Ahmed Jamal, tangu aondoke Ahmed Jamal Morogoro ilirudi nyuma kiviwanda, hapo katikati tuliyumba sana, hata vile vilivyobinafsishwa vilikuwa havifanyi kazi sawasawa.

Sasa Serikali hii ya Awamu ya Tano kwa kuja kuufufua Mkoa wa Morogoro ninyi wenyewe ni mashahidi kila akipita alikuwa akisimama Msamvu ni juhudini kuwahamasisha waliochukua viwanda wavifufue, hasa vile vilivyokuwa vinafugiwa mpaka mbuzi. Pia akatutafutia viwanda vipyatatu, tena hivyo vitatu vimetu kwenye Jimbo langu la Morogoro Vijiji, kwa nini nisimshukuru? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kujipendekeza ni ili kupewa kiwanda kikubwa cha sukari zaidi ya kuzalisha tani laki mbili ambapo kitaajiri watu laki moja acha nijipendekeze. Kama kujipendekeza kuletewa Kiwanda cha Kuchakata Mbaazi katika Jimbo langu acha nijipendekeze, kama kujipendekeza ni kuletewa Kiwanda cha Sigara cha kutengeneza Marlboro ambayo inakwenda kuuzwa Marekani kwenye Jimbo langu acha nijipendekeze, kama kujipendekeza ni kuletewa shilingi milioni 500 Februari mwaka huu kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya elimu katika Jimbo langu acha nijipendekeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kujipendekeza ni kuletewa zaidi ya bilioni nne kwa miradi ya maji katika Kijiji cha Fulwe - Mikese, Kijiji cha Kiziwa milioni 700, Kijiji cha Kibwaya milioni 600, Kijiji cha Nyumbu milioni 600 pamoja na Tulo-Kongwa acha nijipendekeze. Kama kujipendekeza ni kuja kuweka kambi ya ujenzi wa *Standard Gauge* reli ya kisasa

katika Kata yangu ya Ngerengere nyumba zaidi ya 70 zinajengwa kwa ajili ya watumishi wakiondoka, acha nijipendekeze, kama kujipendekeza ni kutengeneza barabara ya kutoka Ngerengere - Maturi - Kwaba - Mkulazi mpaka Kidunda kwa thamani ya *one point eight billion* acha nijipendekeze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema hapa mengi ambayo tumefanyiwa kwenye Jimbo langu sitaki Jimbo la mtu mwingine nitajipendekeza sana kwenye Serikali hii. Kama kujipendekeza barabara ya kwenda Stieglers Gorge ipitie kwenye Jimbo langu kutoka Ubena Zomozi - Ngerengere - Tunungua mpaka Mvua acha nijipendekeze. Kama kujipendekeza ni kuletewa *1.5 billion shillings* kuweka kwenye mpango kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ambayo tulioomba hapa Bunge liliopita acha nijipendekeze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kujipendekeza ni kujengewa kituo cha afya cha milioni 400 kwenye Kata yangu ya Mkuyuni acha nijipendekeze. Nayasema haya wenzetu hata kwenye mitandao wanapotosha sana, wanasesma Wabunge wa CCM kazi yao wakifika ni kuisifia tu Serikali ya CCM kama imefanya nini. Nawaambia kama wale watu haya wanajua ni uwongo waje katika Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, ndani ya Halmashauri ya Morogoro, Mkoani Morogoro waje wayaone haya ambayo yamefanyika, kama hawajipendekeza na wao. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo pamoja na mafanikio ndiyo maana uongozi uko kwa miaka mitano na kila mwaka tunapanga bajeti tunakuja kuwasemea wananchi wetu Serikali inayachukua kwa kufanya maboresho kwa ajili ya kuondoa changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na utekelezaji mzuri wa Ilani ya CCM katika Jimbo langu, katika Halmashauri yangu lakini nina maombi machache ndani ya Serikali yangu.

Kwanza katika yote ni barabara ya Bigwa - Kisaki kujengwa kwa kiwango cha lami, hii barabara iko kwenye

Ilani ya Chama cha Mapinduzi lakini ni ya muda mrefu. Kama mnakumbuka ndiyo barabara mbili tu ambazo zilichaguliwa kujengwa kwa msaada wa Serikali ya Marekani, baada ya Serikali ya Marekani kujiondoa hii barabara Serikali imesema itaichukua na bahati nzuri Mheshimiwa Rais akiwa Waziri wa Ujenzi wakati Rais wa Awamu ya Nne, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, anakuja kutuaga katika Jimbo letu alimkabidhi kiporo hicho na aliahidi kwamba atakitekeleza.

Niwaombe sana, hii barabara uchambuzi yakinifu na usanifu wa kina umemalizika, hii barabara ni muhimu kwetu na sasa hivi umuhimu wake umeongezeka zaidi ukizingatia Serikali kuititia Wizara ya Maliasili inataka kufungua utalii kule Kusini kwenda Selous kuititia barabara hiyo. Niwaombe sana tuitengeneze barabara hii ili utalii wetu uende vizuri, lakini pia ni barabara mbadala kutoka Mjini kwenda huko Kisaki, kwenda Stieglers mpaka Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia barabara hii ndiyo inakwenda Makao Makuu ya Wilaya ambayo Mheshimiwa Rais ametuhamisha kwa fedha zake na kwa amri zake sasa hivi tuko Vijiijini. Ni kweli Morogoro Vijiijini na Makao Makuu yetu yako Morogoro Vijiijini, niwaombe sana barabara hii isiihe angalau ndani ya miaka mitano basi ianze angalau wananchi wale wawe na matumaini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilishukuru kuhusu ujenzi wa kiwanda chetu cha sukari katika Jimbo langu. Hakuna mazuri ambayo hayaji na changamoto, kwa sababu kiwanda hiki kitaajiri watu zaidi ya laki moja, watu wenye ajira rasmi na wasiokuwa rasmi itaongeza mahitaji ya huduma za jamii makubwa kwa muda mfupi. Kwa taarifa kiwanda hiki mashine zake zilishaagizwa, zilishaanza kutengenezwa na kitaanza kujengwa mwishoni mwa mwaka huu na kitaanza kuzalisha mwakani Septemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba sana kwa sababu watakuwa ni watu wengi wanakuja kwa mara moja, tuziangularie Kata hizi za Maturi na Mkulazi kinapojengwa kiwanda kile hasa ujenzi wa kituo cha afya pamoja na shule

ya sekondari ukizingatia ile Kata ya Maturi ni mpya, tumeshaanza wenyewe tumejenga madarasa mawili na tunaendelea lakini kwa ujio wa wakazi hawa wapya hatutoweza kumudu kwa mambo ya shule na vituo vya afya na zahanati kwa wakati mmoja kuwa-*accommodate* watu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili pili; barabara hiyo ambayo imetengenezwa mwaka huu, niwaombe sijaiona kwenye mipango ya *TARURA*, barabara ni ndefu sana ina kilometra zaidi ya 80 ambayo kwa sasa tunasaidiwa na mwekezaji, lakini tukiiacha barabara hii iendelee kuhudumiwa na mwekezaji tutaongeza gharama za uwekezaji na ule uwekezaji utakuwa hauna tija au utakuwa na gharama kubwa kwa mwekezaji wetu.

Niwaombe sana Serikali muichukue barabara hii muiingize kwenye mipango yenu ili muitengeneze kurahisisha kutengeneza mazingira mazuri ya uwekezaji ule na kuwavutia watu wengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni kwenye mkazo wa elimu. Hapa ninataka niongee Kitaifa zaidi, hapa nataka niiongelee *UDOM*. Serikali ipo hapa mimi ni mmoja ambaye nimepitia vyuo hivyo vyote viwili *UDSM* na *UDOM*, nimefika pale kama tunavyofahamu kile Chuo Kilitakiwa kijengwe vitivo saba, vitivo viwili bado havijakamilika na Mheshimiwa Rais alishaahidi anatakiwa kukumbushwa tu, mara nyingi Mheshimiwa Dkt. John Magufuli akiahidi lazima anatekeleza, tuliona alifanya katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kwa hiyo niwaombe sana mpelekeeni salamu ili amalizie atupatie fedha pale *UDOM* waweze kumalizia vile vitivo viwili ili lile lengo lililokusudiwa liweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa sababu *UDOM* kina uwezo wa kuchukua wanafunzi 45,000 lakini mpaka sasa kimedahili wanafunzi 30,000 tu, madarasa yapo, vyumba viro, nyumba zipo kila kitu, tatizo kubwa liko kwa wahadhihi ni wachache. Ninakuomba Waziri wa Utumishi katika mipango yako uje utuambie umewaandalia nini watu wa

UDOM kwa ajili ya kuongeza watumishi (wahadhiri) ili waweze kudahili wanafunzi wengi zaidi na yale majengo yote yaweze kutumika na lengo letu pale *UDOM* liweze kutimia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la elimu niongelee kuhusu ubora wa elimu. Katika ubora wa elimu huu mara nydingi unashuka, matatizo yako mengi katika ngazi mbalimbali, ngazi za msingi, sekondari mpaka chuo lakini leo nataka nijikite kwenye vyuo vikuu. Elimu yetu mara nydingi watu wanasema kwamba wanatoka vyuo vikuu lakini hawaajiriki. Miongoni mwa changamoto nilizoziona ni usimamizi wa wale.....

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mussa Sima, Mheshimiwa Almas Maige na Mheshimiwa Zitto Kabwe wajiandae.

MHE. MUSSA R. SIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kukushukuru sana, pia nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi yake kubwa anayoifanya, ama hakika amepita Singida, amefungua kiwanda kikubwa sana cha alizeti na ni kiwanda kikubwa *East Africa*, niwaombe yale maelekezo aliyotoa sasa yatekelezwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru pia na kumpongeza mzee wangu Mkuchika alivyoweza kuzingatia agizo la kuwarudisha wale watumishi wa darasa la saba, tunakushukuru sana. Nimshukuru kaka yangu Mheshimiwa Selemani Jafo na Naibu Mawaziri ama hakika TAMISEMI imetulia. Yapo mambo mengi sana ambayo

wameyafanya sina sababu ya kuyaelezea, lakini mambo machache niwashukuru tumepesta fedha shilingi milioni 500 kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Sokoine na ujenzi unaendelea vizuri. Kama haitoshi mmekwenda mbali na hata majirani zangu mmewapa pia fedha za kujenga Hospitali za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkalama mmewapa shilingi bilioni 1.5 wanajenga Hospitali ya Wilaya, lakini pia hata *Singida DC* wanajenga Hospitali ya Wilaya kule eneo la Ilongero, nawashukuru sana ndugu zangu mmetupunguzia mzigo mkubwa, ama hakika sasa mmepanua wigo wa watu kupata huduma ya afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili la afya ndugu zangu Singida Mjini tunalo tatizo hatuna hospitali ya Wilaya, tumepewa fedha zaidi ya shilingi bilioni 2.3 za kujenga Hospitali ya Rufaa tayari fedha zile zimeshakwenda na Hospitali ya Rufaa inaendelea vizuri. Ninawaomba, hili nilishaliezea kwenye Wizara ya Afya kwamba majengo ama Hospitali ya Mkoa iliyoko pale sasa hivi itakapohamia kwenda Hospitali ya Rufaa ni vizuri yale majengo tukayatumia kama Hospitali ya Wilaya ikishindikana basi mtupe fedha ya kujenga Hospitali ya Wilaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende eneo lingine, katika hotuba ya Waziri ukurasa wa 58 umezungumzia programu za kujengea uwezo Halmashauri za Miji na tayari Halmashauri ya Manispaa ya Singida tumeshaweka mpango kabambe tunayo *master plan*. Ninaiomba Serikali iende mbali zaidi tunapoweka *master plan* nini malengo yake, malengo yake ni kuelekea kwenye Jiji, sasa mtupe mwongozo wa kupanua ule Mji wa Singida ili tuweze kuwa na Jiji. Mnajua tayari Serikali imeshahamia Dodoma sehemu ya kupumulia ambako ni karibu na Dodoma ni Singida. Tukuombe Mheshimiwa Waziri hili tuliwekee mkakati, Mkoa wa Singida uwe mkoa wa kimkakati kwa ajili ya kuisaidia Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niangalie eneo lingine ambalo ni vizuri pia nikalielezea la asilimia 10; asilimia tano kwa vijana na asilimia tano kwa akina mama. Ninashauri

eneo dogo, nishukuru Serikali imeondoa riba, lakini hapa tatizo kama ambavyo wamesema wenzangu haikuwa kwenye riba, tatizo ilikuwa ni utoaji wa hizi fedha.

Sasa naomba nishauri ni vizuri Serikali ikawa makini mtupe mwongozo na mzielekeze Halmashauri zifungue akaunti maalum ili kuweza kuweka fedha hizo moja kwa moja hili litatusaidia sana, lakini tuweke sheria kali kwa sababu hata marejesho yake, mpango wa kuleta marejesho ya zile fedha haueleweki na hii ndiyo inatupa mazingira magumu ya kuweza kuwapa na wengine fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda haraka kwa sababu yako mambo mengi ya kuzungumza, tunalo soko kubwa la vitunguu. Nilishaomba awali hapa tujengewe soko lile na Serikali iliji-*commit* kujenga lakini mpaka sasa haijajengwa. Umezuka mgogoro, yako maelekezo ambayo wanaelekezwa wafanyabiashara wetu kwamba sasa waende wakafungashe ule mzigو (*packing*) shambani badala ya kwenye soko. Sasa tunataka kujua maana ya soko ni nini? Kama sasa watu wanaamua kwenda kufungasha shambani mwekezaji anatoka Kenya, Uganda aende shambani kwa mkulima, tunachojuu akienda shambani maana yake atamuonea mkulima, tunataka mapato. Tunataka kuona maana ya soko yaani umuhimu wa soko uonekane. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nataka nikuombe Mheshimiwa Waziri uje Singida, tufanye mkutano tuweze kuondoa mgogoro huu wa soko na ikiwezekana soko hili la vitunguu liweze kujengwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko eneo lingine la Waheshimiwa Madiwani kwa kweli ni jambo jema sana na wanafanya kazi kubwa sana, ni vizuri Serikali ikafikiria namna ya kuwaongezea posho yao ili waweze kufanya kazi yao vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kuna eneo moja hapa ni vizuri nikawakumbusha Serikali, miaka

minne, mitano nyuma alitokea Mzee Loliondo tulimwita Babu wa Loliondo, tulikuwa tunaenda kupata kikombe cha babu. Watanzania wote walielekea kwenda Loliondo na Serikali iliamua kuhakikisha inatengeneza miundombinu ya barabara inayoenda huko na kujenga minara ya simu, lakini hatukugundua tatizo nini la Loliondo. Hatukugundua tatizo ni nini Watanzania wameamua kuondoka kwenye hospitali zetu tulizozitegemea wamekwendwa Loliondo. Anamtoa mgonjwa yuko *ICU* anapelekwa Loliondo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitarajia kuiona Serikali inatathimini ni wapi tumefeli mpaka Watanzania wote wameamua kwenda kwenye tiba mbadala. Nataka kusema nini hapa, tumeamua sasa kuhakikisha kila kata iwe na kituo cha afya na kila kijiji kiwe na zahanati na Hospitali za Wilaya. Serikali imejikita kwenye Hospitali za Wilaya naomba ije na mkakati tusirudi kule kwenye tiba mbadala, ije na mkakati wa kuhakikisha kwamba huu utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi ambao tumeuelekeza ili uweze kutekelezeka kwa umakini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajifunza hapa Loliondo ninajifunza pia na utawala bora leo. Nataka nilieleze kidogo eneo hili la utawala bora, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ametoa tamko na ameweza kufanikiwa akina mama wamekwendwa pale zaidi ya 2000, jambo hili nilitaka Serikali itusaidie Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam amefanya Jambo jema sana.

Mimi nataka nimpongeze kwenye eneo hili, lakini nataka nifike mahali nishauri, ninampongeza kwa sababu ameonesha kabisa iko mifumo ya Serikali imeshindwa kufanya kazi yake. Kama tunayo Mabaraza ya Kata, tunalo Dawati la Kijinsia, tunao Ustawi wa Jamii mifumo hii yote imeshindwa kufanya kazi yake, tunazo taasisi za dini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, akatokea mtu mmoja akasema na watu wakafika wakaitikia, hapa tunajifunza jambo, mifumo hii ime-*collapse*. Sasa Serikali inachukua hatua gani? Lakini nataka kujifunza jambo lingine, anapata wapi

legal authority ya kuamua kutekeleza haya ambayo wanayasema leo. Kama ni jambo jema Serikali itusaidie, iamue sasa na Wakuu wa Mikoa wengine waamue kufanya utaratibu huo alioufanya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na kama ni jambo jema tumpe *legal authority* aweze kutekeleza kama ambavyo amefanya, lakini tukiacha hivi akafanya, maana yake tunataka kuwapa mzigo wanafamilia hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo anatoa bima za afya, jambo jema sana lakini tunao watoto yatima hawana baba wala mama, hakuna mtu aliyetoka akasema watoto hawa nao wapewe bima ya afya. Niombbe sana Serikali iliangalie jambo hili, jambo hili litatuletea mgogoro mkubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa pili niwakumbushe pia alitokea mama mmoja wa Tanga, Mheshimiwa Rais aliamua kufanya *natural justice* ya kumsikiliza. Yule mama mjane alisikilizwa na alieleza mambo yake yote pale kwenye ule mkutano, lakini Mheshimiwa Rais hakuamua, alichokiamua ni kupeleka kwenye mifumo rasmi na leo yule mama yupo jela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiki kinachofanyika maana yake umeshawasikiliza watu, ukishawasikiliza warudishe kwenye mifumo rasmi iliyowekwa na Serikali, ikiendelea hivi ilivyo maana yake kila mtu atakuwa naamka leo anafanya jambo tumekaa kimya. Nataka niombbe Serikali kwenye eneo hili tuwe makini sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu ameonesha uwezo mkubwa sana na hata wa kuendelea kusimamia matatizo ya wananchi. Ametambua utawala bora maana yake nini na ameweza kutekeleza. Sasa wasaidizi wake nao watambue utawala bora, ile mifumo hata kama *ime-collapse* na yeye ndiye anayoismamia, arudi kwenye mifumo rasmi, awarudishe kule ifanyike *natural justice* wasikilizwe kwa pamoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mazingira mengine atusaidie pia, likiisha hili la akina mama lakini pia akina baba nao waliachiwa watoto akina mama wameondoka nao pia waitwe waweze kusikilizwa, tutakuwa tumeweza ku-*balance* suala la *equality*, tunazungumzia usawa. Usawa haupo upande mmoja tu, usawa upo pande zote mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niiombe Serikali kwenye eneo hili tusilichukulie mzaha, nchi leo kila mama leo ameelekea kule. Sisi tuliozaliwa na kulelewa kwenye *single mother family* tunajua uchungu wake. Kauli tu ya Mkuu wa Mkoa mama anashangilia hajapewa chochote, kauli tu ya kusikilizwa, maana yake mifumo yetu huku chini haisikilizi, mifumo yetu huku chini yawezekana haiwezeshwi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri.

MHE. MUSSA R. SIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Napenda kuamini ushauri ulioutoa kwa Serikali kwenye eneo hilo watauchukua. Tunaendelea, Mheshimiwa Almas Maige atafuatiwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe. (*Makofi*)

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa fursa hii nichangie hoja iliyopo mezani inayohusu Wizara hizi mbili, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema ukweli siyo kujipendekeza, sitaki kusema najipendekeza, nataka kusema kweli kwamba Serikali hii ya Awamu ya Tano imefanya mambo makubwa sana na kwa vile Wizara hii inayohusika ni Waziri ambaye ni Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli, sifa nyingi zinazokwenda kwenye Wizara hii zinakwenda kwa Mheshimiwa Rais, Mawaziri wote wawili na Naibu Mawaziri wote wawili na watendaji wote wa Wizara hizi mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na afya; Serikali imefanya kazi kubwa sana hasa kwenye Jimbo langu licha ya mambo makubwa kwenye Mkoa mzima lakini Jimbo langu limepata milioni 500 za kusaidia kituo cha afya, *ime-upgrade* vituo vitatu vya afya, lakini vilevile imetoe fedha za kukarabati zahanati zote katika Jimbo langu, kwa nini nisiseme ukweli kwamba wamefanya kazi, siyo kujipendekeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie hata wale ambao wanasema tunajipendekeza wangepata fursa hii ya kupata hivi vitu ambavyo tumepata na roho nzuri kama za kwetu wangeshukuru. Hawa watu wana roho mbaya, wamepewa vitu, wamepelekewa maendeleo katika maeneo yao hawashukuru, wamekalia kusema mabaya. Serikali hii hakuna nafasi ya kuilaumu, iko nafasi ya kuipongeza tu basi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema mambo yanayohusu afya kwamba Serikali wamefanya nzuri sana Serikali, lipo jambo ambalo ndiyo sehemu kubwa ya uchangiaji leo. Suala la elimu; TAMISEMI imefanya kazi kubwa sana, wametoa elimu ya msingi mpaka sekondari bure nchi nzima, haijapata kutokea, kama ilitokea ni katika nchi nyingine siyo hapa kwetu. Sasa huku nako siyo kusema ukweli? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama meli imeenda Zanzibar inafika na mawimbi yapo lakini inafika, sasa kama kuna mawimbi kwenye suala la kusomesha watoto bure, yapo matatizo sjui ya walini, imepungua sjui kufyeka majani, hayo ni mawimbi lakini hatuwezi kutoa meli kwenda Zanzibar kwa sababu tu kuna mawimbi. Iko haja ya kusimamia mfumo huu wa elimu bure katika kiwango ambacho kinatakiwa na mapungufu madogo haya yanaweza kusahihishwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo moja kubwa ambalo nataka kuliongelea kuhusu elimu. Wapo wataalam wa lugha wanaweza kunisahihisha na kunisaidia, nchi yetu

inasomesha watoto wetu kwa lugha ya kiingereza, kutoka shule ya msingi darasa la kwanza mpaka la saba wanasona kiswahili, wakifika darasa la saba watoto wetu hawa wanabadilisha elimu kama mawimbi ya redio kutoka *TBC 1* kwenda *TBC 2*, vilevile wanabadilisha mawimbi kutoka labda *ZBC 1* kwenda *ZBC 2*, kutoka kiswahili kwenda kiingereza. Ulipoanza mfumo huu kulikuwa na kipindi cha watoto wa *form one* kukaa wiki nne shulen, shule ya upili kabla ya kuanza masomo wakisoma lugha ya kiingereza, siku hizi mfumo huo haupo. Kwa hiyo, wanatoka shule ya msingi wanakwenda kusoma kiingereza, hawaelewi! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumewapa watoto hawa mizigo miwili; kwanza wajifunze lugha ya kufundishiwa, vilevile wajifunze masomo yale ambayo wanatakiwa wayasome kwa kiingereza. Tatizo hili limekuwa kubwa sana, lakini bila kujua kwamba tumeingizwa kwenye vita vya ukoloni mambo leo. Wapo watu na zipo nchi ambazo hazitaki tuwfundishe watoto wetu kwa lugha ya kiswahili ambapo wataelewa zaidi kuliko kiingereza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na mfumo miaka iliyopita kwamba tutafundisha watoto wetu kwa lugha ya kiswahili na wataalam wakaandika vitabu. Mimi nilikuwa mmoja kati ya watu walioandika vitabu, niliandika vitabu viwili kwa ajili ya somo la umeme, nina kitabu kinaitwa *Mwandani wa Fundi Umeme (Pocket Book for Electrical)*, nina kitabu kinaitwa *Misingi ya Umeme na Sumaku (Basic Principles of Electronic and Magnetism)*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitabu hivi vipo vya kiswahili, watoto wanapenda kuvitumia, lakini mitihani inakuja kwa kiingereza, matokeo yake vitabu hivi havitumiki. Wapo wataalam walioandika vitabu vya kemia na fizikia lakini vitabu vile watu wanakata tamaa, mimi mpaka nimezeeka nimakata tamaa sasa vitabu vyangu haviwezi kutumika na nimkuwa kama niliota na baadae nikaamka asubuhi hakuna kilichofanyika. Lugha ya kiswahili ni muhimu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa matumizi ya lugha ya kiswahili ni muhimu ili kuendeleza elimu yetu, na kwa kuwa kukandamizwa kwa matumizi ya kiswahili katika shule zetu sasa umefikia mwisho, na kwa kuwa sasa umefika muda nchi yetu itumie kiswahili ili kunyanya elimu yetu, na kwa kuwa tunae Mheshimiwa Rais ambaye amekuwa anatoa maamuzi magumu kwa faida ya nchi yetu na kwa faida ya wananchi wa Tanzania; kwa mfano reli ya *standard gauge* alii sema imeteklezwa, amesema mambo ya ununuzi wa ndege imeteklezwa, amesema mradi wa umeme wa Rufiji, tumeambiwa tuseme Stieglers Gorge tuseme Rufiji limeteklezwa, amesema ujenzi wa ukuta kule Mererani limeteklezwa na amesema tuhamie Dodoma limeteklezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Rais ambaye ndiyo Waziri wa Wizara ya TAMISEMI atolee uamuza suala la kusomesha watoto kwa lugha ya kiswahili. Suala hili linahitahitaji utafiti na utafiti umefanyika, nimesikia kwenye redio wameongea wataalam wa kiswahili kwamba walikuwa tayari lakini kwa vile Serikali haikuonesha nia ya kwenda kwenye lugha ya kiswahili suala hili likawekwa kabatini. Nina hakika mambo yalikuwa madogo kuliko kujenga reli ya kati ya *standard gauge*, kujenga ukuta wa Mererani na kununua ndege *cash*. Mheshimiwa Rais ambaye ni Waziri wa Wizara hii akitamka tutumie kiswahili nina hakika litakuwa jambo dogo kuliko kuhamia Dodoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende upande wa Wizara hii ya Mheshimiwa Mkuchika ya Utumishi na Utawala Bora. Kila mtu akisimama hasa upande wa pili kule kumekuwa na maoni ya kutokuwa na utawala bora hapa nchini, nawashangaa sana. Wamekuwa pia wanaisakama Idara ya Usalama wa Taifa wanasesma Idara ya Usalama wa CCM, jambo hili ni baya sana. Kila mtu anaamka hapa na kufanya kazi vizuri kwa sababu kuna utawala bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lawama hizi zinatokana na watu kujua na Mheshimiwa Mkuchika anielewe vizuri, kujua kazi za Idara ya Usalama wa Taifa. Siku moja amezisema

humu ndani, huenda haitoshi ni bora ifanyike elimu ya semina kwa Wabunge wote juu ya kazi ya Idara ya Usalama wa Taifa, itasaidia kwa sababu tunawakilisha watu wote nchi nzima, watu wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wamewakilishwa humu. Tukipata elimu ya Idara ya Usalama wa Taifa tutaenda kuisema kule na wananchi wote wataelewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Usalama wa Taifa ni kuleta amani hapa nchini, umoja na mshikamano, haya yote tunayoyaona, utulivu huu umeletwa na Idara ya Usalama wa Taifa. Kwa hiyo, ni muhimu sana wale wote wanaolaamu wakauliza vilevile Mheshimiwa George Mkuchika, Waziri wa Utawala Bora ni bora ukaandaa semina, tulifanyiwa wakati wa Bunge la Katiba, tulifanyiwa semina tukaelewa sana na haikutupa taabu kuendeleza, kutunga ile Katiba Inayopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea nilimtaja Mheshimiwa Zitto na Waheshimiwa wafuataao wajiandae. Mheshimiwa Joel Makanyaga, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba na Mheshimiwa Omari Kigua halafu nitabadilisha utaratibu.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba zenye mafungu mbalimbali ya Wizara ya TAMISEMI, mafungu matatu na Wizara ya Ofisi ya Rais, Utawala Bora pamoja na Utumishi, na nitachangia maeneo kama matatu/manne tu kutokana na muda jinsi itakavyokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo nataka kulichangia ni la upande wa Fungu 30, Ofisi ya Rais *Cabinet Secretariat* ambapo ni pamoja na Fungu 20 ambapo ndipo Idara ya Usalama wa Taifa ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tarehe 21 Julai, Rais alifanya ziara Mkoani kwetu Kigoma, siku moja kabla ya Rais kufika katika Wilaya ya Kibondo, Mwenyekiti wa

Halmashauri ya Wilaya Ndugu Simon Kanguye aliiwtwa Ofisini kwa Mkurugenzi akakutana na *District Security Officer (DSO)* wa Kibondo na toka siku hiyo Mwenyekiti huyu wa Halmashauri na Diwani hajulikani alipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, familia imechukua hatua mbalimbali, wamelalamika sehemu mbalimbali, Wajumbe wenzake wa *RCC Kigoma* tumehoji kwenye vikao, Wajumbe wenzake, Mameya na Wenyeviti wamehoji kwenye *ALAT*, hakuna maelezo yoyote kutoka Serikalini kuhusiana na jambo hili.

T A A R I F A

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaka yangu Mheshimiwa Zitto anasema kuwa Mwenyekiti aliiwtwa Ofisi ya Mkurugenzi ambayo tunajua yupo Mkurugenzi, yeye alipata wapi hiyo taarifa ya kujua kule kuna Afisa Usalama wa Taifa wa Wilaya alijuaje na kama alijua kuna Afisa Usalama wa Taifa basi anafahamu yule Mwenyekiti wa Halmashauri alipoenda.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zitto.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama wawakilishi wa wananchi wa Kigoma tunalaumiwa kwa nini hatumtetei mwenzetu, mwenzetu yupo wapi toka Julai, miezi tisa leo. Naomba Serikali, Waziri wa *TAMISEMI* ndio Waziri mwenye Mameya wote, Wenyeviti wote wa *Council*, leo hii wananchi wa Kata ya Simon Kanguye hawana mwakilishi kwenye Baraza la Madiwani la Kibondo kwa sababu hawajui Diwani wao yupo wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyekiti wa *Council* (Diwani) ni Diwani wa Chama cha Mapinduzi, wala siyo

Diwani wa *Opposition*, mnapoteza mwakilishi wa wananchi na hamna maelezo yoyote. Naomba tupate maelezo haya kutoka Ofisi ya Rais, Utawala Bora ambayo ndio wanasi mamia Idara ya Usalama wa Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zote zipo Kibondo ya mtu aliye kwendwa kumchukua tena ameenda kumtoa Ofisi ya Chama cha Mapinduzi, kumpeleka Ofisi ya Mkurugenzi, kumpeleka kwa *DSO* ambaye alikuwepo kwenye Ofisi ya Mkurugenzi na mpaka leo haonekani. Habari ambazo zinasambazwa Kibondo ni kwamba Mheshimiwa Kanguye tayari ameuawa, tunataka maelezo ya mtu wetu huyu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kitu kimoja na wazee kama Mzee Mkuchika wanisikie vizuri. Sisi watu wa Kigoma ni watu wa Kigoma kwanza kabla ya kuwa Watanzania na naomba hili lieleweke kabisa. Haiwezekani tuonekane siyo raia, viongozi wetu na Madiwani wetu wakamatwe, wapatee na hakuna maelezo yoyote hatutakubali, kamwe hatutakubali na hatushindwi vita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kupata maelezo ya Mwenyekiti wa *Council* ya Kibondo, Simon Kanguye, familia yake inalia kila siku mchana huu nimetoka kuongea na mke wake na wadogo zake, hawana taarifa. Naomba Serikali itupe taarifa yupo wapi Mjumbe mwenzetu wa *RCC* Kigoma, kama mmemuua mtuambie watu watoe matanga, hatuwezi kuendelea na hali hii. Na ninarudia, watu wa Kigoma, ni watu wa Kigoma kwanza kabla ya kuwa Watanzania na ninaomba lieleweke hili. Kwenye hili watu wa Kigoma, Kakonko, Kibondo, Uvinza na wapi wote tupo pamoja. Mtueleze Mwenyekiti wa *Council* na Diwani wa Kibondo yupo wapi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo napenda kulichangia, Halmashauri zetu kuna kazi inafanyika na nimesoma hotuba ya Waziri na bahati nzuri Waziri alikuwa Naibu Waziri kwa hiyo alijitahidi, alizunguka maeneo mengi

kwa hiyo anafahamu eneo ambalo analifanya kazi. Tuna tatizo kubwa sana la fedha za maendeleo kutokwenda kwenye Halmashauri zetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwenye taarifa yake aliyoitoa hivi karibuni juzi, ameonesha kwamba asilimia 49 ya fedha zilizotengwa kwenye bajeti ya 2016/2017 hazikufika kwenye Halmashauri zetu. Mwaka jana tumetenga fedha zingine, nimesoma hotuba ya Waziri ukurasa wa saba anaonesha kwamba mpaka Februari fedha ambazo zimefika zote na sasa hivi Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI Selemani itabidi mnisamehe kidogo, mmechakachua hotuba sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote hotuba za Mawaziri zinaonesha fedha za kawaida ngapi zimefika, fedha za maendeleo ngapi zimefika, kwenye hotuba hii ukurasa wa saba mmesema tu kwa ujumla fedha ngapi zimefika, fedha ngapi za maendeleo hazijafika hamjaeleza kwenye hotuba mpaka Februari mwaka huu. Lakini taarifa ya *CAG* inaonyesha *almost 49 percent*, nusu ya fedha zinazotengwa kwa maendeleo hazifiki. Sasa tunatunga bajeti kwa ajili ya nini? Kama *budget credibility* ipo namna hii, kama fedha zinatengwahaziendi tunatunga bajeti kwa ajili ya nini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni muingiliano. Bunge liliopita hapa tulisikia malalamiko ya Tunduma, kwamba Halmashauri haifanyi kazi kabisa Tunduma kwa sababu ya muingiliano kati ya Mkuu wa Wilaya na Madiwani. Pili, kuna muingiliano wa kisiasa vilevile kwenye maeneo kadhaa nchini. Kwa mfano, *CAG* anasema kwamba Halmashauri hazikusanyi mapato, Halmashauri yangu ni moja ya Halmashauri ambazo zina matatizo ya mapato, hayakusanywi, magumu kupatikana. Halmashauri nydingi sana *only 17 percent* ya mapato ndiyo imekusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekaa, tumetunga *by-laws*, tumeiletu Serikalini, Waziri wa TAMISEMI amesaini *by-laws*, ushuru uanze kukusanywa, anakuja Kiongozi wa CCM Taifa

Kigoma anasema kwamba msilipe huo ushuru. Fedha ambayo tumeponga kukusanya ndiyo inalipwa Tabora, ndiyo inalipwa Sumbawanga, ndiyo inalipwa Nzega, ndiyo inalipwa Kasulu, ndiyo inalipwa Kibondo, shilingi 50,000 kwa kizimba, lakini sisi tunakuja kuambiwa msikusanye, hii ni nini hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watendaji nina barua hapa za mawasiliano kati ya TAMISEMI na Meya wa Halmashauri kuhusiana na namna ambavyo watendaji hawasimamii vizuri fedha za Halmashauri. Halmashauri yangu imepata hati chafu mwaka huu kwa sababu mapendekezo yote ambayo Meya ameyaandika na barua kutoka TAMISEMI, Katibu Mkuu Mhandisi Mussa lyombe ameandika barua, Naibu Katibu Mkuu Zainab Chaula ameandika barua kuelekeza hatua za kuchukuliwa, hakuna hatua iliyochukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hatua imechukuliwa baada ya juzi CAG kutoa taarifa na kusema kwamba watu wasimamishwe, ndiyo tumeona hatua imechukuliwa. Lakini toka mwaka 2016 Meya wa Halmashauri anaandika barua na nitaziweka Mezani hapo Waziri azione, hakuna hatua inayochukuliwa. Sasa mambo haya mtakuja kuwaumiza bure wananchi, kwa sababu wananchi siyo wanaoandika taarifa. Kuna hoja kumi hapa za hati chafu ya Manispaa ya Kigoma Ujiji, kumi. Katika hizo hoja, tisa ni za watendaji, tutawajibuje wananchi, tutafanya nini katika mazingira kama haya? Haya ni matatizo ya viongozi wakubwa kuwapa viburi watendaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais alipokuwa Moshi aliwaambia watendaji, Madiwani wasiwaapelekepeleke, wakiwapeleka atavunja Halmashauri. Madiwani wakikaa kwenye Kamati ya Fedha na Uongozi wanatoa maelekezo kwa watendaji hawafanyi, ndiyo barua hizi. Tumeponga hati chafu Mheshimiwa Jafo kwa sababu Mkurugenzi hakuchukua taarifa ambayo imefanyiwa marekebisho kumpelekeea CAG kwa wakati, mpaka leo anayo ofisini, tunafanya nini? Kwa hiyo, ninaomba haya mambo tuyaangalie upya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa ni mapato ya ndani ya Halmashauri. Mapato ya ndani ya Halmashauri yanaathiriwa sana na maamuzi... (*Makof*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Zitto kwa mchango wako.

Mheshimiwa Joel Makanya, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Omari Kigua, Mheshimiwa Cosato Chumi na Mheshimiwa Esther Matiko wajandae.

MHE. JOEL M. MAKANYAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hotuba mbili za Mawaziri wa Wizara ya TAMISEMI pamoja na Utawala Bora ambazo zimewasilishwa hapa jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninampongeza Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, kwa utendaji wake mzuri. Tunashuhudia sasa tuna miaka miwili na nusu tangu ameingia madarakani na tuliona mwanzo kabisa alipoanza watu tulifika mahali tukafikiri kwamba hii ni nguvu ya soda, lakini tunadhihirisha muda unavyokwenda nguvu hii inazidi kuwa kubwa zaidi. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili nichukue fursa hii kuwapongeza Mawaziri husika wa Wizara ya TAMISEMI pamoja na Utawala Bora, Mheshimiwa Jafo pamoja na Naibu Mawaziri wako, pia kwa Mheshimiwa Kepteni Mkuchika, mmedhihirisha kwamba ninyi ni hodari na kwamba Mheshimiwa Rais hakukosea kuwateua katika nafasi hizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia kwanza kabisa suala la utawala bora, wachangiaji walio wengi wamejaribu kuchangia, nami nataka niguse sehemu ambayo

naona kama haijapewa uzito unaostahili. Katika suala la utawala bora vipo vigezo vingi vinavyotumika kusema hapa kuna utawala bora wengi wamevizungumza hivyo, lakini mimi nizungumzie suala la kuwa msikivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuwa kiongozi bora kama wewe siyo msikivu, lazima uwasikilize wenzako, lazima uwasikilize walio chini yako wanasema nini ili utoke hapo ujue namna gani ya kuifanya kazi yako iende vizuri. Katika hili niwe wa kushuhudia katika hili pamoja na Wabunge mliomo ndani humu, kwamba Serikali hii ya Awamu ya Tano ni sikivu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nipo kwenye Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, tulikuwa watu wa kwanza wakati tumeanza kujadili hizi bajeti kwenye Kamati zetu, tarehe 19 Machi ndipo tulianza kujadili hizi bajeti na siku hiyo tulikuwa tunajadili bajeti ya Utawala Bora. Wajumbe wa Kamati walilizungumzia kwa kina sana na kwa uchungu sana suala la watumishi walioachishwa kazi kutokana na kigezo cha kutokuwa na elimu ya kidato cha nne na tunashukuru Mheshimiwa Waziri Alilichukua na akasema atalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama vile haitoshi, tarehe 4 Aprili tulianza vikao vya Bajeti hapa ndani na Wabunge humu ndani wamechangia kwa nguvu sana, kwa uchungu sana, suala hili la watumishi walioachishwa kazi kwa kutokuwa na elimu ya kidato cha nne. Tarehe 9 Aprili nataka muone jinsi gani Serikali yetu ni sikivu Mheshimiwa Waziri, Kepteni Mkuchika, amesimama hapo mbele na kutoa tamko ambalo tunalijua sisi sote. Tuseme nini sasa kama siyo usikivu wa Serikali. (*Makof*)

TAARIFA

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa msemaji anayeendelea kuongea sasa hivi kwamba hata hao watu ambao walifukuzwa kwenye kazi walifukuzwa na Serikali ile ile ambayo imewarudisha. Kwa hiyo, hakuna usikivu wowote kwa sababu wangetaka

kusikia wasingewafukuza toka mwanzo, siyo wanasubiri waondoke halafu wawarudishe tena. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Makanyaga.

MHE. JOEL M. MAKANYAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sina haja ya kusikiliza ushauri huo kwa sababu unaposema mtu msikivu ni baada ya kupewa ushauri. Bunge tunafanya kazi gani humu ndani, kazi yetu ni kuishauri Serikali. Baada ya kuwa yametendeka mambo ambayo hayako vizuri tumefanya kazi yetu ya kuishauri Serikali na Serikali imesikia, imetekeleza, tuseme nini sasa? (*Makofi*)

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa, mtalaumiana wenyewe baadae.

T A A R I F A

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninaomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba hata hawa ambao tumesema warudi kazini ni wale tu wenye sifa za kurudi kazini ndiyo wamerudi, wale ambao hawana sifa hawarudi kazini. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Makanyaga.

MHE. JOEL M. MAKANYAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa yake lakini kwa angalizo, naipokea. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee upande wa TAMISEMI, katika kuzichambua bajeti za Wizara hizi mbili, jambo lililojitekeza la wazi ni kwamba upelekaji wa fedha za maendeleo kwenye Halmashauri zetu ni mdogo sana unasuasua, jambo hili linafanya miradi yetu ya maendeleo kwenye Halmashauri haiendi katika kasi tunayoitarajia. Sambamba na hilo, ilijidhihirisha pia suala zima la ukusanyaji

wa mapato ya ndani kwenye Halmashauri zetu pia linasuasua, haya mambo yote yanachangia kufanya miradi yetu ya maendeleo kusucasua katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili naomba nizungumze suala moja, ninaiomba sana TAMISEMI, pale Halmashauri zinapokuja zinahitaji ushauri basi maamuzi yawe yanatoka mapema ili kama kunahitajika kuchukua *plan B* Halmashauri ziweze kuchukua na kusonga mbele na masuala ya maendeleo. Katika hili nitoe mfano mmoja kwa Mheshimiwa Jafo, Waziri wa TAMISEMI, Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino imekuwa na matatizo ya ulipaji fidia kwa viwanja viliwyopimwa katika maeneo ya Buigiri na maeneo ya Aneti, pesa imekosekana ya kulipa fidia, Halmashauri imekuwa ikijaribu kupata hela kutoka sehemu mbalimbali bila mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya mwisho tumeandika barua kama Halmashauri, imekuwa ofisini TAMISEMI kwa maana ya kwamba watusaidie tupate mkopo ili tuweze kulipa fidia kwa wananchi na viwanja vile viweze kugaiwa. Viwanja hivi vikigaiwa ni chanzo cha kuleta maendeleo, watu watajenga na kodi zitakusanywa, mapato ya ndani yataongezeka na miradi ya maendeleo itatekelezeka. Ninaomba sana katika hili Mheshimiwa Waziri uliangalie kwa karibu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ninapenda nizungumizie ni suala zima la elimu. Tunalia sana na masuala ya elimu na hasa tunalia ukosefu wa walimu, sehemu kubwa tunalia walimu wa sayansi mashulenii. Jambo hili pia liko mezani kwako Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI. Kuna walimu wa sayansi ambaao walikuwa *form six*, lakini wamesoma wamemaliza wamepata *degrees* zao mpaka sasa wana miaka mitatu wanafanya kazi hawajarekebishiwa mishahara yao, wanateseka sana lakini pia wanavunjwa moyo katika utekelezaji wao wa kazi. Tunaomba haya mambo yafanyike kwa haraka ile watu waweze kufanya kazi kwa moyo mmoja. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuishukuru sana TAMISEMI, walitupatia kama Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino shilingi milioni 500 kwa ajili ya kukarabati kituo cha afya pale Chamwino, pia walitupatia shilingi milioni 400 zilienda kwa Ndugu yangu Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde kule Jimbo la Mtera kukarabati zahanati. Kama vile hiyo haitoshi pia wametupatia shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Chamwino, tunasema ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Omari Kigua ajiandae.

MHE. LOLESTIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia bajeti ya siku ya leo ambayo iliwasilishwa siku ya jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kipekee kabisa kutoa pongezi, hasa kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kwa kazi kubwa ambazo wanazifanya, kwa kweli wanastahili kupongezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niwapongeze hata watumishi wa Serikali ambao ni Katibu Mkuu pamoja na wenzake wote na wafanyakazi wote kwa ujumla. Nikiangalia kwa kipindi cha miaka miwili na nusu sasa katika Serikali ya Awamu ya Tano nimeona jinsi ambavyo Ofisi ya Rais, TAMISEMI imefanya kazi kubwa sana, hasa Mheshimiwa Waziri kuweza kuititia sehemu mbalimbali kwenye Majimbo yetu, kwenye Halmashauri mbalimbali kwa ajili ya kuangalia changamoto mbalimbali ambazo zimekuwepo kwa muda mrefu na hatimaye kuweza kuzifanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo, nikianza na suala ambalo limezungumzwa na Wabunge walio wengi, nami lazima nilisemee suala la kuwarudisha Watendaji wa Vijiji na Kata ambao walikuwa ni darasa la saba ilikuwa ni

kilio kikubwa sana ambacho kimekuwepo na binafsi pia katika Halmashauri yetu takribani Watendaji 83 walikuwa wameondolewa kazini. Jambo hili wiki iliyopita nilimuona Mheshimiwa Waziri, Kepteni Mkuchika, nikamuelezea changamoto hii na akanihakikishia kwamba Serikali inaangalia namna ya kulifanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kipekee kabisa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla kwa jinsi ambavyo suala hili wameweza kulitendea haki. Niwaombe tu hao Watendaji wafanye kazi kwa bidii ili kuweza kuleta maendeleo katika Halmashauri pamoja na wananchi wote kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika sekta ya afya katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kipekee kabisa niishukuru Serikali kwa jinsi ambavyo imeweza kufanya jitihada kubwa katika sekta ya afya. Kulikuwa na changamoto kubwa siku za nyuma, kwa sasa tumeona jinsi ambavyo Serikali inafanya kazi. Iliweza kuleta shilingi milioni 500 katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita ambazo zilikwenda kwenye kuboresha Kituo cha Afya Nzela.

Nitumie tu fursa hii kuomba sasa, katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita ina majimbo mawili, Jimbo la Busanda kwa kweli hatujapata hiyo fedha, niombe kwa ajili ya kituo cha afya Katoro ni kituo ambacho kina watu wengi sana, kina msongamano mkubwa, hata wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri naomba utume watu waende pale wakajionee hali halisi. Ukienda kuangalia Hospitali ya Rufaa ya Geita watu wengi wanatoka Katoro, pale ambapo wodi ya wazazi inajaa inabidi wazazi hawa wapelekwe kwenye Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nichukue fursa hii kuomba sasa TAMISEMI kupitia Mheshimiwa Waziri, ikiwezekana tuma wataalam wako wakaangalie hali halisi, lakini kikubwa zaidi tunaomba fedha zaidi ili kuweza kukiboresha Kituo cha Afya Katoro ambacho kina msongamano mkubwa sana wa watu, hatimaye basi

waweze kupata huduma bora kama maeneo mengine. Vilevile ninashukuru kwa ajili ya gari la wagonjwa ambalo nilipatiwa kwa ajili ya Kituo cha Afya Katoro. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizi, niombe tena kwamba katika Jimbo la Busanda kuna tarafa mbili, kuna Tarafa ya Busanda ambayo haina gari la wagonjwa hata moja. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kuiomba Serikali katika Kituo cha Afya Bukoli pamoja na Gengekumi, niiombe Serikali basi iangalie, Kituo kinaitwa Kashishi na Igengekumi Serikali ione uwezekano wa kupeleka gari ya wagonjwa angalau hata gari moja kwa sasa kwa ajili ya Tarafa ya Busanda ili tuweze kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kanda ya Ziwa inaonesha inaongoza kwa vifo hivi vyta akina mama wajawazito wakati wa kujifungua. Ili tuweze kupunguza vifo hivi ninaomba sasa Serikali iweze kutuletea gari ya wagonjwa ili kupeleka huduma hizi kwa akina mama. Tunajua kwamba vijijini watu hawana uwezo, pale ambapo mama anashindwa kujifungua kwenye kituo cha afya au zahanati anakuwa hana uwezo wa kukodisha gari kwenda kwenye Hospitali ya Rufaa, lakin mkiongeza magari ya wagonjwa yatawezesha kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kwa sababu kutakuwa na uwezekano wa kusafirishwa kwenda katika Hospitali ya Rufaa ili waweze kupata huduma iliyo bora. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya afya tuna upungufu mkubwa sana wa watumishi. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita tu tuna upungufu wa watumishi zaidi ya 200. Niliuliza swali tarehe 30 Januari, ikaonesha kabisa kwamba upungufu uliyopo ni watumishi zaidi ya 240.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie fursa hii katika bajeti ya mwaka huu Halmashauri yetu ikileta maombi kwa ajili ya kibali cha ajira kwa watumishi, imeombia watumishi 121 niiombe Serikali basi iweze kutupatia hivyo vibali ili watu waajiriwe tuweze kupunguza adha na

matatizo na changamoto mbalimbali, hasa katika sekta hii ya afya ambayo ni ya muhimu zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua juhudzi za Serikali jinsi ambavyo wameongeza bajeti katika sekta hii ya afya, nina imani kubwa kwamba hizi changamoto Serikali itaendelea kuzifanyia kazi ili hatimae wananchi wetu waweze kunufaika na kuwa na afya bora. Haiwezekani kuwa na maendeleo kama afya haipo katika hali nzuri. Kwa hiyo, naiomba Serikali hasa watumishi katika sekta ya afya tuna upungufu mkubwa, iweze kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kuishukuru Serikali, hasa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwa jinsi ambavyo imeweza kupanga mpango wa kuweza kujenga hospitali ya wilaya katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita, jambo hili nalipongeza sana. Ilikuwa ni hitajji kubwa kutokana na kwamba, iliyokuwa hospitali ya wilaya ilibadilishwa matumizi ikawa Hospitali ya Rufaa ya Mkao. Kwa hiyo, niombe sasa hizo shilingi bilioni 1.5, fedha hizi zije mara moja ili ziweze kuanza kazi kuweza kujenga Hospitali ya Rufaa katika Wilaya ya Geita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika sekta ya afya tunatambua kwamba katika Wilaya yetu, kwanza nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mkuu wetu wa Mkao pamoja na Mkuu wa Wilaya kwa mkakati mkubwa ambao wamejipanga kuweza kutekeleza Sera ya Taifa ya Afya, kwamba kila kijiji kiwe na zahanati, kila Kata iwe na kituo cha afya, na tayari mpango huu umekwishaanza. Kwa sababu hii niiombe Ofisi ya Rais, TAMISEMI tujipange basi kuweza kuona kwamba utekelezaji huu unaungwa mkono kwa dhati, hasa kwa kuleta vifaa muhimu, lakini vilevile na watumishi pale ambapo zahanati zitakamilika pamoja na vituo vya afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nizungumzie sekta ya barabara. Tunatambua kwamba tumetunga sheria ya TARURA, TARURA kweli tunaona ipo tumeiazisha lakini bado haijaanza kufanyakazi yake vizuri, nitumie fursa hii hasa

kuiomba Serikali iweze kuiongezea uwezo *TARURA* ili iweze kufanya kazi zake vizuri. Tunaona jinsi ambavyo barabara nyingi za vijijini asilimia kubwa zaidi ya 70 ni watu wanaishi vijijini, barabara za vijijini hazipitiki. Ninaiomba Serikali iwekeze hasa kwenye barabara za vijijini, haiwezekani tunaweza kufikia uchumi wa katiba bila ya kuweza kufanikisha barabara vijijini.

Kwa hiyo, niombe Serikali kuhusu *TARURA* iongeze kasi zaidi na fedha ili tuone kwamba barabara za vijijini zinapitika wakati wote, hapo tunaweza kuwawezesha wananchi kuaanzisha viwanda wataweza kuuza mazao yao sehemu tofauti kwa sababu barabara zinapitika. Kwa hiyo, TAMISEMI iangalie sana *TARURA* ili hatimaye tuweze kuona mafanikio makubwa kutokana na kuwepo kwa barabara hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivi kwa sababu Jimbo langu la Busanda lipo vijijini ninaona changamoto iliyopo kubwa, barabara nyingi hazipiti. Kwa hiyo, niiombe TAMISEMI iwekeze kwenye barabara kwani ndiyo msingi wa maendeleo yetu hasa vijijini. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Lolesia Bukwimba.

MHE. LOLEIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu Bungeni tusikilizane. Mheshimiwa Omari Kigua atafuatiwa na Mheshimiwa Cosato Chumi.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi jioni ya leo niweze kuchangia hotuba hizi mbili za Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia nitakuwa mnyimi wa fadhila kama sitamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya. Kabla sijawa Mbunge

katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nilikuwa nafuatilia sana midahalo humu ndani, moja ya changamoto kubwa ilikuwa ni malalamiko kwamba Tanzania hii hatuna ndege, Tanzania hii hatuna *rail way* za kisasa, lakini Mheshimiwa Rais amethubuti kuhakikisha kwamba tunakuwa na *rail way* ya kisasa, amethubutu kuonesha kwamba tumenunua ndege kwa kweli lazima tumpongeze. Itakuwa ni jambo la kusikitisha sana kama hatasisima Mbunge katika Bunge hili bila kumsifia Mheshimiwa Rais. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo machache sasa nianze mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita zaidi kwa kuanza na *TARURA* (Mfuko wa Barabara Vijijiini). Mimi nipongeze maamuzi ya Serikali kuwa na *TARURA*, ni kweli kabisa kwamba *TARURA* imesaidia utengenezaji wa barabara zetu vijijiini, lakini zipo changamoto mbalimbali ambazo mimi kama Mbunge sina budi kuzungumzia, wamezungumza wenzangu hapa kwamba *TARURA* inachangamoto ya fedha na mimi niseme kwamba tuone namna ambavyo tunaweza tukakaribisha mfumo wa *TARURA*, tuweke chombo ambacho kinaweza kuwa kinasimamia utekelezaji wa majukumu ya *TARURA* ili kile chombo kinaweza kufanya tathmini ya majukumu ya *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi tuone namna ambavyo *TARURA* wanaweza kuongezewa watumishi, natoa mfano katika Jimbo la Kilindi ambalo lina kilometra za mraba takribani 845.2, eneo hili ni kubwa sana, lakini tunalo gari moja, tu utaona kwa kiasi gani kwamba dhamira ya kuwa na *TARURA* inaweza isifanikiwe katika Jimbo langu la Kilindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hii naiona ipo katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo tuangalie namna ambavyo tunaweza kuwaongezea *TARURA* vitendea kazi tuwaongezee *staff*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitofautiane kidogo na wazungumzaji wengine kwamba tuone chombo hiki kiende kwa Waheshimiwa Madiwani hili sikubaliani nalo, kwa sababu *TARURA* iko katika maeneo yetu ya Majimbo. Mheshimiwa Diwani anaweza kumwona Meneja wa *TARURA* akamweleza barabara yake, hata Mheshimiwa Mbunge anaweza akazungumza jambo hili. Kwa hiyo, sioni umuhimu wa kuipeleka chombo hichi katika chombo cha Madiwani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni zahanati. Ninamshukuru Ndugu yangu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo kwamba tumepata shillingi milioni 500 kwa ajili ya kituo chetu cha afya Songe, niseme wazi kabisa nilikuwa mionganoni mwa watu ambaao niliomba kuwa na Hospitali ya Wilaya, lakini kwa sababu nimepata shillingi milioni 500 na zimeweza kwa kiasi kikubwa tumejenga majengo naomba tuongezewe shillingi milioni 500 nyingine ili ikiwezekana tuweze kupandisha hadhi Kituo cha Songe iwe ni Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linakwenda sambamba na suala la watumishi. Watumishi imekuwa changamoto sana, tumeona juzi tu watumishi wengi wameondolewa. Ushauri wangu kwa Waziri wa TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Utumishi tuone namna ambavyo tunaweza tukawaajiri watumishi wa kada ya chini, huko ndiko kwenye watendaji wengi sana tuone namna gani zoezi hili ambalo limepita na lile la nyuma tuweze kuhakikisha kwamba mapengo haya ambayo yapo maeneo mengi yanafanyiwa kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, katika Jimbo langu la Wilaya ya Kilindi tunaupungu wa walimu 589, sekondari walimu 135, kada ya afya 320. Kwa hiyo, utaona uhitaji huu uko kila sehemu. Ninakuomba Mzee wangu Waziri wa Ofisi ya Rais, Utumishi waangalie namna gani wanaweza kuititia mahitaji haya katika Halmashauri zetu ili tuone kwamba huduma zile za wananchi zinakwenda vizuri zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo mchango wangu mwingine utaenda kwenye suala la utawala bora. Imejitokeza changamoto katika maeneo mbalimbali watumishi wengi wanakaimu, hili limekuwa ni tatizo kubwa sana. Mimi nina uzoefu kwa sababu nimefanya kazi Serikalini, zamani ilikuwa kwamba Katibu Mkuu akistaafu unajua kabisa ni nani anayefuata kuwa Katibu Mkuu, Mkurugenzi akistaafu unajua ni nani anaafuata kuwa Mkurugenzi. Hii *succession plan* sasa hivi katika Serikali haipo na hii ndiyo inasababisha kwamba unamteua mtu anakaimu unamfanya upekuzi kwa muda mrefu kwa sababu humfahamu. (*Makofii*)

Ninakuomba Katibu Mkuu Dkt. Ndumbaro wakae chini walitafakari hili, utaratibu wa *succession plan* urudi ili tuwe na uhakika kwamba Katibu Mkuu leo akistaafu tunajua nani anayefuata, badala ya kwenda kuchukua hapa na hapa ma-*gap* haya yanakuwa ni ya muda mrefu sana. Haya kwa kiasi fulani yana zorotesha utendaji wa Serikali kuanzia Serikali Kuu mpaka Halmashauri. Jambo hili ni muhimu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nirudi kwenye suala la huduma hizi za afya. Katika Jimbo langu la Wilaya ya Kilindi pamoja kwamba nimemsifia Mheshimiwa Waziri hapa kwamba amenipa shilingi milioni 500 kwa ajili ya Kituo cha Afya Songe, lakini viro vituo mbalimbali katika Jimbo langu la Kilindi ambalo jiografia yake ni ngumu sana, nimuombe Mheshimiwa Selemani Jafo ikiwezekana zikipatikana fedha unitengee fedha kwenye vituo vifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Jaila ambacho kina takribani watu 20,000, Kituo cha Afya Kwediboma kina takribani watu 50,000 na Kituo cha Afya cha Negero, wananchi wangu pamoja na Mbunge wao tumeshaweka majengo yameshakuwa ni makubwa sana, tunahitaji fedha za kumalizia, nitashukuru sana Mheshimiwa Waziri kama utapata fursa ya kuja kwenye Jimbo langu na kutembelea maeneo haya kwa sababu wananchi wa Wilaya ya Kilindi bado wana changamoto ya afya. Najua dhamira ya Serikali ni nzuri ya kuwasogezea huduma ya afya lakini

katika eneo langu la Wilaya ya Kilindi tulikuwa tunaomba sana sasa maeneo niliyoyataja yaweze kujengewa vituo vya afya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nipongeze japo kuwa halijaja suala hili dhamira ya Serikali ya kuwa na mamlaka kama chombo kama cha *TARURA* cha maji vijijini, hii itasaidia kwa kiasi kikubwa sana. Ni juzi tu nimeuliza swalii juu ya miradi ya maji katika Jimbo langu la Wilaya ya Kilindi, kuna mapungufu hapa ya usimamizi wa miradi ya maji. Naomba watu wa *TAMISEMI* na Wizara ya Maji wawe na Tume maalum wale na Kamati maalum ya kufuatilia miradi hii wasisubiri mpaka Wabunge tuje tuzungumze Bungeni hapa au *CAG* aandike ripoti. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa inapopelekwa katika maeneo yetu tuhakikishe kwamba inafuatiliwa, kwa sababu unapokuwa umeleta mradi halafu mradi ule haujakidhi viwango, mradi ule haojatoa matokeo yanayotarajiwa maana yake wanaoathirika ni wananchi wa maeneo husika na Serikali hairudishi tena pesa inachukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa Waziri wa *TAMISEMI* na Naibu Mawaziri wake wote wanafanya kazi kubwa sana, kwa sababu wanafanya ziara za mara kwa mara, jambo hili ni jema sana kwa sababu linasaidia Waheshimiwa Mawaziri kujua changamoto katika maeneo yetu na hii linafanywa na Mawaziri wengine pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kusema kwamba naonga mkono hoja na ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante tunaendelea na Mheshimiwa Cosato Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hizi muhimu. Awali ya yote ninapenda kusema mambo mawili nimemuona Mheshimiwa Mwigulu pale Simba tatu *Mbeya City* moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa niliseme katika kazi nyepesi duniani ni kazi ya kukosoa hata kama unatazama mpira ni rahisi sana kusema pale Okwi angefanya hivi au Chirwa angefanya hivi lakini ukiingia mambo yanakuwa ni tofauti kabisa. Kwa hiyo, *this is the easiest job in the world!* Hawa wenzetu wanapokosoa Waheshimiwa Mawaziri niwatie moyo tu kwa sababu wanafanya *easiest job in the world* wewe take easy tu chapa kazi kanyaga twende. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nami kama wenzangu ninapenda kuwashukuru Mawaziri na watendaji katika Wizara hizi, Mheshimiwa Selemani Jafo Waziri wa TAMISEMI, Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Gorge Kakunda na Mheshimiwa Josephat Kandege, Waziri wa Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa George Mkuchika. Pia hata Makatibu Wakuu wa Wizara hizi ukienda pale TAMISEMI kwa Mhandisi Mussa lyombe au kwa mama yangu Dkt. Zainab Chaula na kwa Dkt. Ndumbaro pale Utumishi bado sijapata nafasi ya kukutana na wale Manaibu wengine. Kiongozi yule anatoka kwenye Kiti anakuja huku anakusikiliza, mnajidiliana mnashauriana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la namana hiyo ndiyo uongozi ni jambo la kupongezwa unashida za wananchi wako wanakusikiliza mnashauriana *the way forward*. Kwa hiyo, ufanyaji wa kazi wa namna hii mimi niwapongeze. Hii ndiyo namna pekee ya kumuunga Mheshimiwa Rais mkono katika ndoto zake za kuendelea kuisogeza nchi yetu mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi niseme pia pongezi za jumla kwa Serikali kwa watu wa Mafinga, tunapenda kuishukuru sana Serikali katika masuala ya afya, maji na elimu kwa sababu usipokuwa mtu wa kushukuru maana yake ni kwamba wewe pia hustahili kuwepo kwa maoni yangu. Mpaka sasa tumepokea shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala, fedha hizi zitaongeza mzunguko katika Mji wa Mafinga. Mwenye

kusomba kokoto mwenye kusomba tofali, mama lishe, wote hawa wanatakuwa ni wanufaika wa fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali imetusaidia katika maji nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Maji tuna tanki pale la lita laki tano na sasa tumeanza ujenzi wa tanki lingine la lita milioni moja. Hizi ni hatua changamoto bado zipo, haziwezi kumalizika siku moja lakini ni vizuri kushukuru pale ambapo inastahili kushukuru. Kama haitoshi tuna mradi kule Maduma wa ujenzi wa tanki la lita 100,000 pia tuna mradi kule Bumilainga unaendelea, yote ni kusogea huduma karibu na wananchi, hata katika elimu tumepata takribani shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuboresha miundombinu kwenye shule ya sekondari Changarawe, shule ya msingi Maalum Makalala ambapo Mheshimiwa Jafo ukiwa Naibu Waziri baada ya kutembelea tu *immediately* tukapata shillingi millioni 100 tukajenga bweni na bado tena tumepata karibuni shilingi milioni 220 kuendelea kuboresha miundombinu katika shule ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama vile haitoshi katika afya tumepata shilingi milioni 500 nawashukuru sana Mawaziri, Mheshimiwa Waziri wa Afya tumepata *ambulance* shughuli zinaendelea, yaani ni kwamba kwa lugha nyingine pamoja na kuwa changamoto hazijaisha unaweza kusema Mafinga mambo ni moto. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye changamoto Mheshimiwa Waziri niwaombe, mlituomba tulete taarifa za miradi viporo kutokana na zile fedha za *LDG*, sisi tunasubiri pesa zile kwa ajili ya kukamilisha Kituo cha Afya cha Bumilainga, ukamilishaji wa zahanati tatu za Kitelewasi, Kisada na Ulole pamoja na nyumba za watumishi. Pia kukamilisha *hostel* ya wasichana ya Mnyigumba katika kata ya Lungembba na pia kukamilisha ukarabati wa shule ya msingi Kikombo jumla ni milioni 859 ambazo kama Serikali mliona kwamba tuainishe maeneo ambayo katika kuunga mkono juhudii za wananchi basi, ninyi mtatupa pesa tumalizie miradi viporo. Niombe Serikali kama ni Wizara ya Fedha kama ni TAMISEMI basi fedha hizi tuletewe ili tupate kukamilisha miradi

ile ambayo wananchi kwa nguvu zao walikuwa wa kwanza kuianzisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *TARURA*, tunashukuru kwamba Mafinga tumeputa fedha milioni 500 tumeboresha kituo cha afya cha Ihongole, lakini tunashida kubwa ya barabara unafikaje katika kituo cha Ihongole. Kati ya mahitaji ya Mafinga kwa ajili ya barabara kwa kweli kama siyo changamoto ya barabara kama nilivyosema, katika mambo mengine kwa jinsi tunavyokwenda mpaka kufika mwaka 2020 Mafinga mambo yatakuwa ni moto.

MBUNGE FULANI: Ni *fire!*

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *fire* kabisa. Shida kubwa iko katika barabara, kati ya mahitaji billioni 8.2 kwa mfano kwaka huu 2018 tumetengewa kutokana na ukomo wa bajeti shilingi milioni 830 hii ni kama asilimia kumi ya bajeti, kwa nini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana ninasema katika suala la *TARURA* ndugu zangu hata tukiwa na *TARURA* kumi, kama hatutabadilisha kanuni ya mgao wa fedha za Mfuko wa Barabara maana yake ni kwamba hatuwezi kupiga hatua yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati shughuli hizi zingine za maendeleo zinaenda ni muhimu sana kuhakikisha kwamba wananchi wanaweza kusafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine katika kuhakikisha kwamba mazao yanasaferishwa kwenda sokoni. Kwa mfano, Mafinga katika barabara tulizonazo *only asilimia 24* ndiyo zile tunaita *good and fair* kwamba zinapitika, lakini barabara nyingine kiasi cha takribani kilometra 288 ambayo ni asilimia 88 ya barabara ni za udongo. Kwa mfano, hii barabara ya kutoka Mashine ya Mpunga kwenda mpaka Kituo cha Afya Ihongole kwa kuwa ni ya udongo na ile wanaita *average daily traffic* ni 4,030 maana yake ni kwamba hata ukitengeneza kila wiki kwa sababu ina *traffic* kubwa itaharibika tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suluhisho na ushauri wetu Wabunge tutakapoleta *Finance Bill* hebu katika hizi fedha pamoja na kazi nzuri ambayo *TANROADS* wamekwishafanya tupeleke mgao kutoka asilimia 30 mpaka walau asilimia 50, kwa sababu *TARURA* wenye barabara zaidi ya kilometra laki moja wanapata asilimia 30, *TANROADS* wenye barabara takribani kilometra 30,000 wanapata asilimia 70 ya fedha. Hata tuwe na *TARURA* bado wananchi wa Mafinga, wa kutoka Changarawe kwenda kule Mtula ambako kuna *irrigation scheme* hawataweza kunufaika na ku-*feel*/matunda mema ya Serikali ya Mheshimiwa John Pombe Magufuli. (*Makofii*)

Kwa hiyo, suluhisho pekee, kwa sababu kazi yetu Wabunge ni kushauri, tushauri kwa pamoja ili kanuni ya mgao wa fedha za barabara iweze kubadilika ili *TARURA* isibakie kuwa *TARURA* jina bali iwe *TARURA* ambayo ina *resources* za kuweza kufanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia napenda kuipongeza Serikali, wenzetu wa Mufindi kwa jitihada zetu pamoja na Mheshimiwa Kigola, Mheshimiwa Dada Rose Tweve, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa sasa wanakwenda kupata shilingi 1.5 bilioni ili wawe na hospitali yao na hivyo kupunguza msongamano katika hospitali ya Mafinga. Hata hivyo, kwa kuwa hospitali hii haitajengwa *overnight* ndiyo maana nasisitiza tupate fedha zile za miradi viporo ili tukamilishe zile zahanati na Vituo vya Afya vya Bumilainga kusudi kupunguza msongamano kwenye Hospitali ya Mafinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja na Mungu aibariki Mafinga, abariki watu wa Mafinga na aibariki Tanzania kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Esther Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Pascal Haonga, Mheshimiwa Rehema Migilla na Mheshimiwa Zainab Mndolwa Amir.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kweli kwa kuweza kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kutoa *opinion* yangu kwa kile ambacho kinaendelea Bungeni, naona kama hatuitendei haki nafasi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanasimama, wanapongeza sana hili la darasa la saba walioajiriwa kabla ya 2004 kurudishwa. Kuna watendaji wengi na watendaji wengine kama hawa watendaji ambaao wamerudishwa hospitalini, madereva ambaao wameajiriwa mwaka 2004 mpaka sasa hivi ambaao kosa lao si tu kuwa darasa la saba kwa sababu waliowaajiri ni Serikali hii hii, imewaondoa kazini, haitaki kuwalipa mafao ya kuwaachisha kazi, halafu leo unasimama mtu anasema tunaipongeza Serikali sikivu, sikivu *what?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza wamefanya makosa hawa ambaao wameajiriwa mwaka 2004 kurudi nyuma *at the first place* hawakutakiwa kutoka kazini, wanatakiwa tuwawajibishe kwa sababu kwa kuwaondoa kazini kuna Watanzania ambaao wameathirika sana. Kuna Watanzania ambaao wamekufa kwenye sekta ya afya, kuna Watanzania wengi ambaao wameathirika halafu leo mnapiga makofi eti wamewarudisha watendaji kuanzia hapo kurudi nyuma, kwa kweli mimi nasikitika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iwajibike kuwalipa *gratuity* wale watendaji wote kwa maana waliokuwa katika hospitali na kwagine kote darasa la saba ambaao iliwaajiri wenyewe na imewaondoa kazini. Kama hawana fedha wanajificha kwenye vyeti *fake* na utendaji kuwaondoa kazini waseme kwa sababu kitu kingine, wameondoa hawa watendaji makazini wameshindwa kuwa-*replace* ambaao sasa wanasisa stahiki. Watu wanahangaika, mmewaondoa kwenye ajira hizi halafu mnashindwa kuwa-*replace* hapa inaonekana kabisa

kwamba Serikali haina fedha ya kuwalipa hawa watu na ni dhambi sana watu wanakufa kuondolewa kwa ghafla makazini na kutokurudishwa kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye utawala bora nilisema sitachangia kabisa, lakini kwa sababu mimi ni mwanamke na ni mwanamama na najua uchungu wa kuzaa na kuona kijana wangu anapotea kwa mazingira ya kutatanisha, watu wanauawa kwa mazingira ya kutatanisha, watu wanalemazwa lakini ukiongea watu hawasikii. Nikasema katika Biblia kuna *phrase* moja inasema; "chozi la mwanamke lina thamani mbele ya Mwenyezi Mungu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale akina mama wote, mama yake Ben Saanane, mama yake Mawazo, mama yake huyu Diwani wa Kigoma, mama wa Watanzania wote waliopotea, mama yake watoto wote waliolemazwa na Serikali hii ambayo haitaki kuchukua hatua; mama yake wa Diwani wetu aliyeuawa pale Hananasif katika uchaguzi wa Kinondoni anapolia chozi lake Mwenyezi Mungu atakwenda kuyalipa hapa hapa. Na mimi naendelea kuungana nao hawa wanawake kulia chozi kwa sababu na mimi ni mwanamke najua uchungu wa kuzaa, najua thamani ya mtoto anakufa bila hatia, naendelea kulia na wanawake hakika Mungu atakwenda kutenda. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kuchangia, kwa sababu dakika ni chache nichangie kwenye TAMISEMI, Jimbo langu la Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiisoma hii hotuba ya Waziri anaeneleza kabisa kwamba upungufu wa madarasa kwa maana ya vyumba vyta madarasa kwa mwaka Julai, 2017 mpaka Machi, 2018; kwanza nimpongeze, wanajitahidi pamoja na kwamba Serikali inashindwa kutambua kwamba TAMISEMI ilitakiwa kupewa fedha nyingi sana kwa sababu ndiyo inayobeba majukumu mengi. Kama ingeweza kutekelezewa vizuri basi maendeleo yangeonekana kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameeleza hapa kwamba yamejengwa madarasa 2,278 na hivi vyumba vimejengwa kwa asilimia 80 na Watanzania waliokuwa wanajichangisha. Upungufu ni 264,594, na vyumba tulivyonavyo sasa hivi ni 123,044. Miaka 57 ya Uhuru tume-manage kujenga madarasa 123,044 yamebaki 264,594 ukigawa kwa yale tu ambayo yamejengwa 2,278 inaonesha Chama cha Mapinduzi kitachukua miaka 116 kuweza kutatua matataizo ya vyumba vyta madarasa Tanzania. Ikizingatiwa wanakuwa na matamko mengi mengi, wananchi wanakuwa wanajitolea ikiwemo wa kwangu wa Jimbo la Tarime Mjini wamejitolea sana, wamejenga mpaka kwenye lenter Serikali...

MHE. ESTER A. MAHAWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

MHE. ESTHER N. MATIKO: ...wanaendelea wanakamilisha...

MHE. ESTER A. MAHAWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

T A A R I F A

MWENYEKITI: Taarifa

MHE. ESTER A. MAHAWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kumpa taarifa mchangiaji kwamba wakati huo wa Uhuru Tanzania walikuwa wachache sana na sasa tuko karibu milioni 54. Mimi nataka tu kuwaambia ikiwa tu wao tangu 1992 vyama vyta upinzani vimeingia ni miaka mingapi mbona wao hawana hata ofisi? (*Vicheko/Makofii*)

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa nasikitika sana halafu wajina wangu eti ana shule na ye ye ana-own. Hiyo taarifa yako inani-*support in actual sense*. Tangu uhuru mpaka leo mmejenga 123,000 bado vyumba 264,594 ukijua kabisa *population* ya Tanzania inaongezeka, mmeleta elimu bure, mnasajili wanafunzi wengi na *capacity* yenu ya kujenga madarasa ni ndogo sana halafu tunaongea

nini? Hivi nini ni kipaumbele chetu? Taifa ambalo haliwekezi kwenye elimu, mtafanya mengine yote lakini hatutaona uchumi ukijionesha. (*Makofî/Viegelegele/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea hapa hapa kwenye elimu ukija kwenye vyoo ni matatizo, na tunajua shule ambazo tunakuta hazina vyoo vya kutosha wanafungiwa wanafunzi wetu hawaendelei. Wananchi wanajitolea kwa asilimia kubwa ndiyo wanajenga hivi vyoo ambavyo wameweka hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna siku nilisema mwaka jana wakati nachangia ambapo mlisema mmeefanya *re-allocation* ya shilingi bilioni 39 kwenda Chato. Nikasema kwanini hata msiangalie kipaumbele mkazipeleka kwenye elimu, mkazipeleka na kwenye afya ili angalau kutatua hizi changamoto ambazo tunazona?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye elimu hapo hapo, walimu hawana nyumba za kuishi, na jana wakati wanajibu swalii hapa wakasema wako nyumba zao binafsi au wamepanga. Mnawapa hiyo hela ya kupanga? Iko nje ya mishahara yao? Mwalimu anapanga kwa mshahara mdogo ule ule mnaomlipa, anasafiri kutoka sehemu "A" kwenda "B" kwa mshahara ule ule halafu unategemea matokeo yawe mazuri. Lazima tuhakikishe tunaweka vichochezi vya kutoa elimu nzuri kabla hatujaanza kusema kwamba tunatoa elimu bure ambayo haina tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa Tarime muweze kunikarabatia sekondari ya Tarime ambayo ni kongwe, imefunguliwa mwaka 1973, na ni sekondari ambayo ni ya *high school*/tu na inachukua zaidi ya *combinations*saba. Mheshimiwa Waziri nimeshakwambia sana. Vilevile kulikuwa kuna gari pale *land cruiser* mmeliondoa tunaomba lirezeshwe wanafunzi wale wanateseka sana. Pia nilileta maombi kwa tarime muweze kutupandishia hadhi sekondari ya Mogabiri kwa mwaka huu wa fedha unaoisha lakini pia tuna sekondari ya Nyandoto ili iwe ya kidato cha tano na cha sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka sana, Waziri unatambua kabisa tatizo tulilonalo kwenye Hospitali ya Wilaya na Mheshimiwa Kandege ulikuja na Waziri Mkuu mliljonea uhalisia. Hatuwezi kuwa tunapata *basket fund* ya shilingi milioni 11 Hospitali ya Wilaya wakati mnapaleka shilingi milioni 42 katika Kituo cha Afya cha Nyalwana hii si haki kabisa na ukizungatia kwenye Halmashauri yangu sijapata kituo cha afya pamoja na kwamba nahudumia Serengeti na Rorya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni kwenye Mnada wa Magena. Ukiangalia kwenye hiki kitabu mapato ya Halmashauri yameshuka sana kutoka shilingi bilioni 1.1 kwa mwaka jana baada ya kuondoa mapato ya mabango na *property tax* kwa mwaka huu tumekusanya shilingi milioni 586 tu. Mkiturudishia Mnada wa Magena tutaweza kukusanya mapato mengi kwenye Halmashauri yetu. Hii *storyya* kusema kwamba Tarime sijui wizi wa ng'ombe kwanza mnatukebehi sana. Sasa hivi Tarime ni salama na ndiyo maana kuna Mkoa wa Kipolisi unaojitegemea wa Tarime-Rorya. Tunaomba kabisa ng'ombe wanatoka Serengeti haziendi Kirumi, ng'ombe wanaotoka Rorya hawaendi Kirumi wanapita moja kwa moja na wale ambao wanununuliwa kwenye Mnada wa Kirumi wanapitishwa Tarime kwa nini wasiibiwe? Tunahitaji Mnada wa Magena ufunguliwe ili uweze kutoa ajira kwa watanzania wa Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye halmashauri yangu wamekaimisha sana Wakuu wa Idara kitu ambacho *kina-affect* utendaji. Miaka inapita Wakuu wa Idara ndiyo wale wale naomba napo pia waweze kunibadilishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa walimu wa sayansi. Tunasema Tanzania ya viwanda, uhaba wa walimu wa sayansi ni mkubwa sana, wananchi wakawa wanajichangisha ili kuwalipa walimu waweze kufundisha Rais akatoa tamko msichangishe, ipitie kwa Mkurugenzi. Wananchi wameacha, Serikali sasa hivi hakuna maabara wala vifaa, walimu wa sayansi hamna. Tunaomba kama mmeshindwa, kwa mfano Tarime tuko tayari kuchangisha na

kuajiri walimu wa sayansi ili watoto wetu wasome vizuri. Tunaomba kabisa kama Serikali imeshindwa kutoa kipaumbele...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Najiuliza Mheshimiwa Matiko mbona nyumbani unakuwaga unaongea kwa utaratibu kabisa, pole pole na nini, kuna nini leo? Mheshimiwa Pascal Haonga.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni zamu yangu na mimi kuweza kuchangia kwenye Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na hoja ya kwanza ambayo ni walimu wa shule za sekondari kuhamishiwa shule za msingi bila kupewa haki zao kisheria.

Mjeshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye kitabu hiki cha hotuba ya Waziri wa TAMISEMI ukiangalia ukurasa wa 40 wameeleza pale kwamba walimu 8,834 walihamishwa kutoka shule za sekondari kupelekwa shule za msingi ili kupunguza tatizo la walimu shule za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza kabisa, kumtoa mwalimu kutoka shule ya sekondari kwenda shule ya msingi hii si sahihi hata kidogo. Kwa sababu huyu mwalimu amejifuza saikolojia ya kufundisha watoto wa sekondari wenye umri mkubwa kuliko wale wa shule ya msingi, leo unapomtoa sekondari kumpeleka shule ya msingi tunakwenda *ku-prove failure* na hauwezei kupata *efficiency* hata kidogo na matokeo yatakuwa ni mabaya kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku ni kukwepa majukumu, Serikali inafika mahali inakwepa majukumu, badala ya kuajiri inafika mahali inaanza kuhamisha walimu wa sekondari kupelekwa shule za msingi. Mheshimiwa Waziri, naomba nikuhakikishie kwamba huko sekondari mnakosema walimu

wanatosha, sekondari, walimu hawatoshi kwasababau unavyozidi kuongeza idadi huku shule za msingi hata kule sekondari idadi ya wanafunzi inakuwani kubwa sana. Kwa hiyo, mnachokifanya Mheshimiwa Waziri kabisa hamuwatendei Watanzania haki hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo lakini bado walimu hawa 8,834 wamehamishwa, lakini hawajalipwa fedha zao. Hawajalipwa *disturbance allowance, subsistence allowance*, wala *transport allowance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi walimu 117 waliohamishwa kutoka shule za sekondari kwenda shule za msingi wanadai zaidi ya shilingi milioni 300 hawajalipwa hadi leo. Serikali hii ambayo inasema ni Serikali ya wanyonge, wanyonge gani ambao hawajalipwa mpaka leo? Wanyonge ni akina nani kama leo walimu 117 wanadai shilingi milioni 300 na kitu hawajalipwa? Huyu anayejiita kiongozi wa wanyonge ni wanyonge wapi? Hii hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi juzi mmefuatilia maandamano yamefanyika kule Mbozi na walimu hawa 117, Rungwe walimu zaidi ya 80 wameandamana wanadai fedha hazijalipwa. Waziri wa TAMISEMI uko hapo, ukweli ni kwamba Waziri wa TAMISEMI katika hili mme-*prove failure* kabisa na mlishaizungumzia siku za nyuma wkamba watumishi wasihamishwe bila kulipwa lakini leo mmeshindwa kufayakazi hiyo ya kuwalipa hawa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niende kwenye suala lingine la ajira za watumishi. Leo Serikali inakwepa kuajiri watumishi, Awamu hii ya Tano haiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mfano mdogo tu, ukisoma ukurasa wa 40 wa hotuba hii ya Waziri wa TAMISEMI wanasema, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imefanikiwa kuajiri walimu wapya 2,767. Unapoajiri walimu 2,767 wakati kwenye ukurasa huo huo tumeambiwa kwamba upungufu wa walimu kwenye shule za msingi ni

walimu 97,517 unaajiri 2,767 tafsiri yake ni kwamba kama tutakuwa hatuzaliani unahitaji miaka 35 ili kuweza kumaliza tatizo la walimu shule za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Serikali ya Awamu ya Tano ukilinganisha na awamu nyininge ndiyo Serikali ambayo naona mimi *ime-prove failure* hamna kilichofanyika kabisa imeshindwa bora hata Serikali ya Jakaya Mrisho Kikwete tunaikumbuka kuna mambo alifanya mazuri, lakini hii ya wanyonge sidhani ni wanyonge gani anaozungumzia *huyu bwana*. **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mmeshindwa kuajiri...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Haonga naomba futa kauli ya neno huyo bwana futa.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kufuta, lakini nasema ujumbe hapa ni kwamba Awamu ya Tano haijaajiri, haitoi ajira.

Kwa hiyo, ukichukua hawa walimu, ukichukua miaka 35 tafsiri yake ni kwamba kama Watanzania hatuongezeki, kwa maana hatuzaliani kuanzia leo tunahitaji kuwa na miaka 35 mingine mbele. Ukijumlisha leo ni mwaka 2018 maana yake ni mwaka 2053 ndipo tatizo la walimu litakuwa limekwisha nchini. Kwa muda huo sidhani kama sisi tutakuwepo kwa sababu kutakuwa na chama kingine kinanachoongoza nchi hii. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni mishara kwa watumishi wa umma. Mishahara haiongezwi, Awamu hii ya Tano haijawahi kuongeza mshahara hata mara moja. Gharama za maisha zinapanda, hali ya uchumi inazidi kuwa mbaya, leo watumishi wanapokuwa wanajaza mikataba wanaanza kazi maana yake pale, pamoja na mikataba yao ni kwamba wanasaini kwamba watakuwa wanaongezewa mshahara *annual increment* kila mwaka, watakuwa wanaongezewa mishahara, wakipandishwa mishahara. Leo

hawapandishwi madaraja, hawaajaongezwa mishahara ndiyo awamu pekee ambayo haijawahi kuongeza mishahara, na ndiyo Serikali ambayo inajitila Serikali ya wanyonge, sijui wanyonge wapi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongeze jambo lingine, shilingi milioni 50 za kila kijiji. Usiku wa deni haukawii kuisha; na mimi nawakumbusha amezungumza Mheshimiwa Heche vizuri sana asubuhi. Usiku wa deni ni mwaka kesho kutwa 2020. Kwanza kuanzia mwakani Serikali za Mitaa tutakwenda kuwakumbusha Watanzania shilingi milioni 50 mlizowaahidi hadi leo hamjatoa na muda unazidi kuisha. Kwa hiyo ndugu yangu Mheshimiwa Jafo, Waziri wa TAMISEMI utatuambia hizi shilingi milioni 50 kwenye bajeti hii zipo au hazipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la ubaguzi wa Watanzania. Kuna watu wanaohojiwa uraia wao, viongozi wa dini maaskofu, Askofu Kakobe, Askofu mmoja anaitwa Severine Niwemugizi wa Kanisa la RC hawa watu pamoja na viongozi wengine mbalimbali, wanafunzi Abdul Nondo. Watu leo hii wameanza kubaguliwa uraia wao, wanahojiwa uraia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inafika mahali kama yule askofu kule Bukoba anasema kwamba kiongozi akatubu, tunataka Katiba mpya. Mtu anapotoa maoni yake ambayo amepewa uhuru wa maoni na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unakwenda kumhoji uraia, kwa nini kabla hajatoa maoni yake msingemhoji uraia? Kiongozi asiyekubali kukosolewa hawezi kuwa kiongozi, lindeni uhuru wa maoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumza ndugu yangu Zitto Zuberi Kabwe, mkitaka basi Mkoa wa Kigoma kama kuna uwezekano basi upelekeni Burundi. Kwa sababu leo inaonekana tatizo kubwa la kuhoji uraia wa watu mnahoji sana watu wa Kigoma. Abdul Nondo mwanafunzi wa chuo kikuu ni mtu wa Kigoma, Askofu Kakobe ni mtu wa Kigoma,

wako na wengine n mifano mingine. Leo kukaa mipakani imekuwa ni dhambi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na wewe mimi naamini kama unakaa karibu na mpakani kule si ajabu ukaja kutoa ushauri wako au maoni yako watakuja kukuhoji sijui uko jirani na nchi gani. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee. Wanasema wamba kama umezoea kula nyama ya binadamu huwezi kuacha, ndugu yangu Hussein Bashe amewahi kuhojiwa uraia wake eti kwa sababu kaingia kwenye kura za maoni na ndugu yangu huyu Waziri wa Maliasili amehojiwa akaambiwa si raia wa Tanzania.

Leo dhambi hiyo ya kuhoji watu haijaisha, kuwabugua watu kura za maoni zimekwisha leo Bashe amekuwa rala wa Tanzania ni kwa sababau kura za maoni zimekwisha na leo ni Mbunge mwenzetu kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kumbe hiyo tabia haikwisha imeendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ni mbaya sana na tunaomba tuikemee kwa pamoja sisi wote kwa sababu leo hii kwa kuwa mtu mwingine, kwa Kakobe leo imetokea kwa Bashe na kwa wengine imetokea kwa Nondo kesho na kesho kutwa ni dhamu yako, kwa kumalizia naomba nizungumze suala... (*Makofii*)

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Hamna muda wako umekwisha, ahsante sana. Tunaendelea, Mheshimiwa Rehema Migilla atafuatwa na Mheshimiwa Zainab Mndolwa.

MHE. REHEMA J. MIGILLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi jioni hii nichangie kuhusu Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Utumishi na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwapongeze Mawaziri wote Wizara hizi mbili, Mheshimiwa Jafo na timu yake Mheshimiwa Kakunda na Mheshimiwa Kandege, lakini vile vile Mheshimiwa Mkuchika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naanza kuchangia kama ifuatavyo na nianze na suala la elimu. Ni ukweli usiopingika kuwa elimu yetu kwa sasa imedolora na inashuka kiwango siku hadi siku. Hii inatokana na ukweli kwamba nchi yetu imeifanya elimu kama huduma na kuwaandaa watu kuwa ni wa kufaulu mitihani tu na si kwenye uwekezaji. Kama nchi haina kipaumbele kwenye elimu na inaifanya elimu kama huduma *obviously* hatuwezi kufika mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali yetu, kama kweli tunataka elimu yetu ikue naomba sana ijikite kwanza kuifanya elimu ni uwekezaji na badala ya huduma. Vilevile ili elimu hii iweze kuwa na tija kwa hawa vijana ni lazima basi hii mitaala ya elimu ifanyiwe *reformation*, kwa sababu sasa hivi ukiangalia inawaandaa tu wanafunzi kufaulu mitihani, lakini hakuna ujuzi wowote inayowapatia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kijana anamaliza darasa la saba, anamaliza *form four*, anamaliza *form six* mpaka Chuo Kikuu hana ujuzi wa aina yoyote, matokeo yake kila siku wanatembea na bahasha mitaani mpaka zinapauka. Naomba Serikali yetu kama kweli tunataka tujikite katika elimu basi haya ninayoyasema, mitaala ifanyiwe *reformation* na ijikite zaidi katika kuwapa wanafunzi *skills* ili wahitimu hawa wanapomaliza, kama ni kidato cha nne basi ajue anatoka na ujuzi gani badala ya kuwa anazurura mitaani. Leo hii vijana hata wa chuo kikuu badala ya kuwa ni *job creators* wamekuwa ni *job seekers*, naomba hili suala tuliangalie. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya ualimu na walimu. Kazi hii ya ualimu inaonekana kama ni kazi ya watu waliofeli, mimi ni mwalimu *by profession*, inaniuma sana jamii inaiona hii kazi ya ualimu kama ni kazi ya waliofeli. Hii inajidhihirisha

unapoangalia kwenye matokeo hata ya *form four, division one, division two* wanaenda *high school*, halafu *division three* hadi *fourth* dio wanaopelekwa ualimu. Kama tanataka kweli tuwekeze kwa nini hii *division one* na *division two* ndio wasipelekwe ualimu? Mpaka jamii inamuona mwalimu ni mtu mjinga mpaka inafikia anaulizwa yaani umekosa hata nafasi ya kwenda kwenye ualimu! Jamani ualimu ni kazi kama zilivyo kazi zingine wote tulimo humu tumeピta kwa mwalimu kwa nini huyu mwalimu leo hathaminiki? Naomba Serikali impe hadhi mwalimu kama inavyompa mtu mwengine. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwalimu wa Tanzania ana changamoto nyingi sana ambazo zinamkumba. Leo hii walimu wamekosa morali wa kufanya kazi na takwimu zinaonesha wanafanya kazi chini ya kiwango, yote hii inasababishwa na Serikali kwa kutowajali walimu. Walimu wana stahiki nyingi sana ambazo wanazidai lakini Serikali haitekelezi. Wana madeni ya *arrears*, wana madeni ya nauji, ya nini Serikali haitekelezi. Nataka njue leo hii Serikali inatumia vigezo gani pindi inapowalipa hawa wafanyakazi au walimu stahiki zao mbalimbali. Kwa mfano katika Jimbo la Tabora mjini kuna hizi shilingi bilioni mia mbili zilizotolewa na Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kuwalipa walimu, lakini ni walimu 18 tu ndio wamelipwa wakati kuna idadi kubwa ya walimu hawajalipwa. Sasa nataka TAMISEMI mtuambie ni vigezo gani ambavyo mnavitumia kuwalipa hawa walimu stahiki ili hali wana madeni mengi? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa kuanzisha elimu bure, elimu bure inaende sambasamba na kutoa posho kwa walimu wakuu wakuu wa shule na waratibu wa elimu kata. Hata hivyo ndugu walimu wana mishahara midogo sana. Tunaomba basi katika hii posho mnayowapa walimu sijui wakuu wa shule ma-*headmaster*na waratibu wa elimu kata basi na walimu na wenywewe wapewe hata kidogo, kwa sababu hawa wakuu wa shule mnaowapa pesa hawafanyi kazi peke yao wanafanya kazi na walimu wengine, nao tunaomba muwape hata kidogo kama motisha ya kuweza kufanya kazi vizuri na kwa ufanisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nizungumzie mchakato wa kuhamisha walimu wa sekondari wa *arts* na kuwapeleka *primary*. Mheshimiwa Haonga amesema ni ukweli usiopingika ni wazo zuri, lakini *approach* inayotumika sio nzuri. Walimu hawa walivyokuwa wanasma kwenye vyuo vyao walisomea masomo mawili, leo hii unawaambia wakafundishe kule watafundisha kitu gani? Mbaya zaidi hakuna hata *induction course* ambayo mmewaandalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali basi angalau iwave *induction course* hawa walimu ili waweze kwenda kufundisha kwenye mazingira yale. Tukumbuke kwamba walimu hawa wamekuwa *trained* kufundisha wanafunzi wenye kimo kikubwa, leo wakafundishe watoto wadogo wataweza? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado njia za ufundishaji watoto wa sekondari ni tofauti na watoto wa *primary*. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali yetu kama kweli tunadhamiria kuinua kiwango hiki cha elimu, japokuwa ni *approach*, nzuri basi hawa walimu wapatiwe *induction course* angalau ya mwezi hata mmoja kwenye *methodologies*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nizungumzie hii Tume Utumishi wa Walimu. Tume hii inafanya kazi kubwa sana na naiomba Serikali liiongezee pesa ili iweze kufanya kazi yake kwa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye kazi nyingine ambayo inafanywa na Wizara ya TAMISEMI. Kazi moja wapo ni kuhakikisha inatatua migogoro inayotokana na ardhi. Mkoaa wa Tabora hususani Manispaa ya Tabora walikumbwa na bomoa bomoa, watu hawa walijenga katika maeneo ambayo walipewa kisheria na bado Serikali yetu...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu.

MHE. REHEMA J. MIGILLA: ... tuweka hadi miundombini kule na bado walikuwa wanachukua hadi kodi

lakini leo hii hawa watu wanaambiwa wahame lile eneo ilhali walipimiwa na Serikali na wako pale kisheria lakini hatuoni dalili zozote za kupewa fidia au kutafutiwa eneo jingine. Naiomba sana Serikali iwanusuru watu hawa, tunaomba basi watu hawa wapatiwe eneo jingine au wapewe fidia waweze kuanza maisha mengine mapya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni katika uvezeshaji wa vikundi vya wanawake na vijana, ile asilimia 10 ya mapato ya ndani. Hizi asilimia zipo kisheria lakini halmashauri zimekuwa hazitengi pesa kwa ajili ya kuwapatia vijana, hali inayopelekea vijana sasa hivi wafanye kazi ambazo ni tofauti na ndoto zao. Tunajua kabisa kila mmoja ana kazi ya ndoto yake, lakini vijana wengi sasa hivi wanafanya kazi ya kuendesha boda boda, wanawake wengi wamekuwa *bar maid* ni kazi ambazo ziko nje ya ndoto zao. Kama Serikali itahimiza halmashauri kutenga asilimia 10 vijana hawa watanufaika na wataacha kuhangaika huko mitaani. Tunaiomba Serikali hizi halmashauri zisizipe mzigo mkubwa yaani mapato yarudi kule kwenye Serikali za mitaa badala ya kwenda Serikali Kuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine ni kuhusu utumishi. Tulipiga kelele sana kuhusu watumishi wa darasa la saba. Ni kweli kabisa watumishi hawa walijiriwa na Serikali na Serikali hii ndio tena ikawatoa kazini, lakini Serikali hii tena imewarudisha kazini, ni jambo zuri na wazo zuri, lakini suala langu ni hili, je, Wizara ina mpango gani au itawalipa kwa fungu lipi watu ambao hawajafanya kazi kwa muda mrefu sana? Pia kuna watu ambao tayari walishaajiriwa ku-cover hizi nafasi za watu walioko darasa la saba, je, hawa watu ambao sasa wameshaajiriwa kuziba zile nafasi za watu wa darasa la saba watatolewa kazini au vipi? Naomba majibu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Zainab Mndolwa atafuatiwa na Mheshimiwa Janeth Masaburi na Mheshimiwa Nkamia ajiandae.

MHE. ZAINAB M. AMIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nami napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema ya kuweza kuchangia katika ofisi ya TAMISEMI na ofisi ya Utumishi na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Wizara ya TAMISEMI kwa kazi nzuri inayofanya. Naipongeza kwa juhudini kubwa anazozifanya Mheshimiwa Jafo katika Wizara yake, hususani katika kazi zake zinazoonekana dhahiri katika kujenga vituo vya afya pia katika kujenga zahanati, na pia namshukuru sana kwa kupandisha Hospitali yetu ya Temeke kuwa Hospitali ya Rufaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiomba na kushauri Serikali; Hospitali ya Wilaya ya Temeke imepandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Rufaa lakini hospitali ile inachukua wagonjwa kutoka Wilaya za karibu hususani Mkuranga na Wilaya ya Kigamboni.

Nakuomba Mheshimiwa Waziri, najua kuna utaratibu unafanya kuboresha zahanati zilizokuwa Mkuranga pamoja na Kigamboni; naomba wakati unafanya utaratibu huo uitupie macho Hospitali ya Temeke. Hospitali hii wodi zake zile kweli ni chakavu na ni za siku nyingi. Nakuomba sana uipe kipaumbele, uiboresha, kwa sababu wananchi wa Mkuranga wakipata *transferti* lazima waende Tumbi na Tumbi ni mbali sana kutokana na jiografia yake kwa hiyo wanachotakiwa ni kuwaleta Temeke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Jafo unaandaa mazingira nakuomba sana Hospitali yetu ya Wilaya ya Temeke ambayo sasa hivi ndio itakuwa ni hospitali ya rufaa iboresha, majengo yake yawe ya hadhi ya rufaa. Kwa sababu eneo ni dogo nashauri Wizara angalau zile wodi namba moja, namba mbili, namba tatu majengo yake yawe ya ghorofa ili iweze kukidhi idadi ya wagonjwa. Pia si majengo tu kuna vifaa muhimu pia vinatakiwa hospitali vifaa kama *x-ray* mmejitahidi, lakini vifaa vingine ni vile vidogo vidogo lakini tunaona si vya muhimu. Katika wodi za wagonjwa lazima kuwe na vikabati vya kuhifadhi chakula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa ukifika Hospitali ya Temeke sasa hivi kuna matatizo, unapompelekea mgonjwa wako chakula unaweka chini chakula hakuna vikabati vya kutosha kwa hiyo naomba sana katika kuboresha hizo hospitali na vifaa vingine ambavyo mnaviona ni vidogo vinahudumia wananchi, vinahudumia wagonjwa wote ni muhimu sana katika hospitali zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili. Ni ukweli usiopongika kwamba Hospitali ya Muhimbili inachukua wagonjwa wengi kutoka mikoa mbalimbali Tanzania Bara na Visiwani. Serikali imejitahidi katika kujenga vyumba vya upasuaji na kuongeza wodi, lakini kuna changamoto moja inayoikabili hospitali ya muhimbili naona watu wengi hawaioni, lakini sisi wakazi wa mjini Dar es Salaam tunaionna. Si wagonjwa wote wanaoletwa katika Hospitali ya Muhimbili wana wenyeji katika Mkoa wa Dar es Salaam. Wanapopewa rufaa wakifika pale *emergence* na kukabidhi wagonjwa wao huwa wanaambiwa kwamba mgonjwa wako ameshapatiwa kitanda, kwa hiyo yeye aondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine hawana ndugu wala jamaa Dar es Salaam. Tunaiomba Wizara angalau itenje jengo maalum ambalo litasaidia wale wasindikizaji ambao wanakuja kuleta wagonjwa wao waweze kupata eneo la kijisitiri na kusubiri matokeo ya wagonjwa wao kama ni vipimo na kuwashudumia. Kuna huduma nyingine haziwezi kufanywa na daktari, haziwezi kufanywa na nesi. *Nurse* hawezi akamlisha mgonjwa, kufua nguo za mgonjwa na labda mgonjwa akiwa amejisaida, ni mtu wa karibu mno anatakiwa azifanye zile huduma.

Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Jafo, Hospitali ya Muhimbili ipatiwe eneo maalum ambalo litakalokuwa na wahudumu watakaoweza kukaa na kuwaona wagonjwa wao jinsi wanavyoendelea na vipimo na kuweza kuwasaidia katika mambo mbalimbali. Kama ikiwezekana wawe na hata *identity card* ya kuonesha kwamba huyu mgonjwa wake yuko Sewa Haji au yuko Kibasila. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili iweze kusaidia hata wale walini wetu wawapo katika maeneo ya ulinzi naomba sana hospitali zetu; nitolee mfano Hospitali ya Mwananyamala; naitolea mfano; ukipeleka mgonjwa hospitali ya Mwananyamala na Mwenyezi Mungu akamtanguliza mbele ya haki akitoka wodini, anapopelekwa chumba cha maiti ili kumtoa kila siku ni 20,000. Akikaa siku 10 ni shilingi 200,000, akifia nyumbani na kuletwa ndani kwenye *mortuary* ya hospitali unakuta anakuwa-*charged* shilingi 30,000. Sisemi utofauti wa malipo ninachosema yule ni Mtanzania halisi ambaye wakati wa uhai wake alikuwa analipa kodi na kodi hiyo ilikuwa inalipwa na Serikali inakusanya, iweje Mtanzania huyu amekufa na ametibowi na ndugu zake kwa gharama nydingi sana maiti mnaitoza malipo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaombeni kama inawekana, kwa ushauri wangu nawaomba mtoe yale malipo ya maiti. Nadhani pale mimi ninatolea mfano tu, kuna hospitali nydingi naona Waheshimiwa Wabunge sidhani kama mmefanya uchunguzi, ukiweka maiti yako hospitali si kama unaweka kwa sababu hutaki kumzika, huenda unasubiri ndugu na jamaa; kwa kweli gharama ni kubwa sana. Huyu maiti wa Tanzania ni Mtanzania alikuwa analipa kodi.

Naomba sana Mheshimiwa Jafo uliangalie kwa makini katika bajeti yako, muondoe haya malipo ya kumtoa maiti wetu katika hospitali hizi za Serikali, iwe huduma kama huduma nyagine. Kwa sababu inaonekana kama tumekosa sehemu nyagine ya kukusanya mapato, tutafute eneo lingine Serikali si kwenye maiti, tuwaonee huruma wafiwa na tumuonee huruma pia marehemu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia pia Hospitali ya Mkoa wa Morogoro. Hospitali ya Mkoa wa Morogoro chumba chake cha kuhifadhi maiti kipo nje ya uzio wa hospitali na kiko karibuni sana na shule ya sekondari ya Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilisoma pale miaka ya 1980, ni kero sana ile *mortuary*, iko karibu na madarasa

kiasi kwamba ndugu waliofiwa na ndugu yao wakati wanakuja kuchukua marehemu wao wanahisia mbalimbali wengine hulia, wengine huja pale labda kuaga kwa mapambio na mwalimu anapofundisha darasani hakuna usikivu. (*Makofi*)

Naombeni Mheshimiwa Jafo wakati unapanga bajeti yako uliangalie kwa jicho la huruma wanafunzi wa Morogoro Sekondari wanapata tabu kwa kuwepo chumba cha maiti karibu na madarasa. Naomba ulifanyie kazi kwa sababu hili ni tatizo kubwa ingawa Mheshimiwa Abdul-Azizi ataniunga mokono ni Mbunge wa Morogoro na anaona tatizo hili, yeye alisoma *Forest*, mimi nimesoma Morogoro miaka ya 1980 lakini tatizo ni kubwa sana. Hata wakati mnafanya mtihani mwalimu unakuta anaweka *stop watch* kwa sababu wangoje zile kelele zipungue, nawaombeni muhamishe ile *mortuary illipo*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine napenda kuchangia kwenye utawala bora, muda hautoshi mambo ni mengi. Kuna baadhi ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wanawaweza ndani kwa masaa 24 wananchi wetu bila sababu na wakati mwingine sababu zenyewe hazijulikani, anakuambia wewe kaa ndani. Sasa nataka Serikali injilishe, je, kama kuna sheria hii ni makosa gani ambayo Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya anatakiwa amuweke mtu ndani kwa masaa 24?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikibainikwa kwamba amemuweka kimakosa, je, Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya atachukuliwa hatua gani? Maana sasa hivi hatuelewi, hata sheria kila mtu anachukua mamlaka mikononi. (*Makofi*)

Nakuomba Mheshimiwa George Mkuchika unijibu swali hili, ni sheria gani inawaruhusu wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya kuwaweza ndani wananchi na baadae anawatoa? Je, ikibainika kwamba hana kosa lolote je, Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya atachukuliwa hatua gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ndugu tuliwarudisha juzi wa darasa la saba, wengine wamefariki, je, Serikali ina mpango gani kwa wale ndugu ambao jamaa zao wamefariki; na hapa juzi tumetangaza kwamba waterejeshwa, je, stahiki zao zitakuwaje? (*Makof*)

Kwa hiyo, naomba wakati wa kutoa maelezo tufahamishwe, kwamba stahiki za wela ambao wamepoteza maisha wengine kwa presha tu baada ya kusimamishwa, je, stahiki zao zitapatika vipi? Kwa sababu wameondoka mbele haki wameacha familia na juzi tunesema kwamba warudi makazini na hawapo duniani? Tunaomba Serikali itupe majibu kwa wale ambao wametangulia mbele ya haki na sheria imesema warudi kazini, walipwe mishahara yao tangu pale waliposimamishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mengi ya kuyazungumza lakini naomba sana walimu wengi wana matatizo, wengi wamezungumza, na sisi wote tumepita kwa walimu lakini sekta hii hatuipi uzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kuongeza mishahara nashauri walimu wawe wa kwanza, utaona, kwamba utakapowaongezea mishahara walimu wengi, hata kama mtu kapata *division one* atakuwa *interest* ya kusoma ualimu. Kama walimu wangkuwa wanalipwa mishahara kama tunayolipwa sisi, wengi na mimi pia ni mwalmu nisingkuwa hapa, lakini kutokana na ualimu kuonekana kama ni kazi dhalili watu wengine wanaacha ile kazi wanaondoka. Kwa hiyo, naomba sana tuwaboreshee walimu mishahara yao stahiki zao ili waweze kufanya kazi kwa weledi. Watakapofanya ya kazi kwa weledi wanafunzi wetu watafaulu vizuri kwa kiwango cha juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nashukuru sana, naomba haya yasiishie kwenye vitabu hivi tu, mmeandika mambo mazuri lakini yasiishie kwenye maandishi. Hii bajeti iliyopagwa itolewe kwa wakati ili muweze kufanya kazi zenu barabara, ahsanteni sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea Mheshimiwa Janeth Masaburi, Mheshimiwa Nkamia na Mheshimiwa Martha Umbulla wajandae.

MHE. JANETH M. MASABURI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ndiye aliyenipa zawadi ya uhai na ametujaalia sisi sote kujumuika hapa leo na kuweza kujadili mambo yaliyo mbele yetu kwa maslahi ya nchi yetu. Vilevile namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumjaalia afya njema Mheshimiwa Spika wetu kwa kumuvezesha kurudi salama. Tunamshukuru Mungu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais, Rais wa Zanzibar, Mawaziri wote na Naibu Mawaziri wote, Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Serikali bila kusahau Wakuu wa Mikoa ambao wote kwa pamoja wamefanya kazi njema ambayo matunda yameonekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Jaffo, Waziri wa TAMISEMI na Naibu Mawaziri wake kwa kazi nzuri wanayoitekeleza. Tumewaona mara kwa mara wakikimbia huku na huku, na mara nytingine wamepata ajali njiani, kwa kweli tunampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nichukue fura hii kumshukuru na kumpongeza Waziri husika wa TAMISEMI ambaye ni Rais wetu mpandwa, Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa kipindi hiki cha miaka miwili na nusu. Amefanya mambo mengi makubwa ambayo yamewashangaza Watanzania ambao wengi walikuwa wanabeza na wengi tukikumbuka walikuwa wanambeza sana Rais wetu wa Awamu ya Nne kwa kutokuchukua maamuzi mengine ingawa yeye pia ndiye aliyweweka mfumo mzuri, lakini pia yeye ndiye aliyetuchagulia Rais Magufuli. Yeye na wenzake walikuwa makini; akamchagua Mheshimiwa Magufuli ambaye leo amekuwa Rais wetu wa nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi yamefanyika katika nchi hii. Kwanza wananchi wengi katika nchi hii wamebadilika kifikra na kimtazamo. Kumekuwa na miradi mikubwa ambayo imetekelozwa kwa kiwango kikubwa sana na mingine pia inaendelea kutekelezwa chini ya uongozi wa Rais wetu. Pia kumekuwa na mabadiliko ya kiutendaji kwa watumishi wa Serikali na taasisi za umma. Nidhamu ya kazi kwa watumishi na huduma nzuri zinafanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitaje mambo machache tu ambayo yamefanyika kwa kipindi cha miaka miwili na nusu.

Moja, kumekuwa na nidhamu kazini kwa watumishi wa umma na uwajibikaji; pili, mapambano dhidi ya dawa za kulevyta na udhibiti wa uingizaji wa dawa za kulevyta. Mapambano dhidi ya ufisadi na uhujumu uchumi, udhibiti wa mapato ya Serikali na matumizi yake; mapato ya Serikali yameongezeka, kudhibiti rasilimali za taifa kama madini na kadhalika, ununuzi wa ndege sita na tatu zimeshawasili hapa nchini na wengi tumehudumiwa na wanaobenza na wao wanapanda hizo ndege.

Pia huduma ya maji imeboreshwa mijini na vijijini, sisi watu wa Dar es Salaam ni maajabu maana tulikuwa tunalalamika, lakini siku hizi changamoto sasa ni maji kupasuka huko mitaani, maji yanapatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna uhamasishaji wa ujenzi wa viwanda vya madawa nchini na viwanda vingine...

TAARIFA

MWENYEKITI: Taarifa!

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mchangiaji kwamba...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masaburi kaa tu.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe Taarifa mchangiaji kwamba labda Dar es Salaam anayozungumza ni nyingine lakini mimi ninayetoka Ukonga, Kata ya Msongola ambayo ina mitaa tisa ina maji kwenye mtaaa mmoja tu. Kata ya Chanika ambayo ina mitaa nane kuna maji mtaa mmoja, Kata ya Buyuni mitaa nane kuna maji kwenye nusu mtaa Kata ya Zingiziwa kuna maji mtaa mmoja...

MWENYEKITI: Mheshimiwa, unataka kuchangia?

MHE. MWITA M. WAITARA: ... kwa hiyo ina maana si kweli kwamba kuna maji yanapasua mabomba Dar es Salaam, labda nyumbani kwake ndiko mabomba yanapasua maji. (*Makof*)

MWENYEKITI: Haya, Mheshimiwa Masaburi.

MHE. JANETH M. MASABURI: Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei hiyo taarifa kwa sababu kwa asilimia kubwa maji yameboreshwa. Kuna maeneo ya Kimbiji na Chanyika ambayo yanategemea mradi unaotoka kule Kigamboni, lakini kwa asilimia 70 maji Dar es Salaam yanapatikana (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za afya zimeboreshwa, lakini kumbuka Roma hajijengwa kwa siku moja. Uhamasishaji wa ujenzi wa viwanda vyatanya dawa kama nilivyosema, mradi wa umeme wa Rufiji (*Stieglers Gorge*) unaendelea, ulinzi na usalama umeimarishwa nchini, mauaji ya Kibiti yamekomeshwa. Amekaribisha wafanyakazi kushirikiana na Serikali kuondoa vikwazo mbalimbali ili kuleta tija kwa Tanzania. (*Makof*)

TAARIFA

MWENYEKITI: Taarifa!

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nimpe taarifa msemaji anayeongea sasa hivi

kwamba Kanuni hazitutaki tuwe tunasoma, tunatakiwa tuwasilishe. Sasa ye ye muda wote amekuwa akisoma lakini pia anasoma taratibu sana. Kama ame amua kusoma asome kwa haraka ili wachangiaji wengine wapate nafasi. (*Makofi/ Kicheko*)

MWENYEKTI: Mheshimiwa Mwambe, hiyo si taarifa ulipaswa kusimama kwa utaratibu. Mheshimiwa endelea na kama unasoma usisome, wewe ni Mbunge mzoefu.

MHE. JANETH M. MASABURI: Mheshimiwa Mwenyekiti, inauma sana, muda mfupi mambo mengi yamefanyika. Hiyo sipoeki kwa sababu naangalia *data*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zimejengwa, madaraja, *flyover* mmeziona Dar es Salaam, mji unabadi lika unakuwa wa kisasa, mradi wa mabasi awamu ya pilii, tatu unaendelea; ujenzi wa kiwanja cha michezo Dodoma unazinduliwa na kadhalika Ni mengi, ngoja niishie hapo maana itauma sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote yaliyofanyika hapa nchini ambayo yanastahili pongezi, na dunia imeshangaa, mwenye macho haambiwi tazama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kumekuwa na changamoto kadhaa ambazo zinapaswa kutiliwa mkazo au kufanyiwa kazi. Katika nchi zilizoendelea kiuchumi duniani ikiwemo nchi ya Marekani, suala la ulinzi limetiliwa mkazo na limetiliwa kipaumbele kuliko sekta nyiningine kwa sababu jinsi uchumi unavyokua ndivyo uhalifu pia unavyokua. Kwa sababu hiyo hata nchi yetu ya Tanzania uchumi unakuwa lakini na mbinu mbalimbali za kihalifu nazo zinakua. Naiomba Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi iongeze bajeti ya kutosha kwa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ili ziweze kukidhi mahitaji ya vikosi vyetu au kwa vyombo vyetu vya usalama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto mbalimbali kama makazi ya askari, magari, mafuta na vifaa

mbalimbali. Mafunzo ya ndani na nje ya nchi, kwa hiyo naiomba Serikali yangu itilie maanani katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kidogo niongelee Jeshi la Zimamoto. Tunaposema uchumi wa viwanda ujue viwanda ni rafiki wa moto kwa hiyo tunaomba pia bajeti katika eneo hilo iongezwe bila kusahau Jeshi la Zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema elimu bure ujenzi wa shule mbalimbali, umeme vijijiini, ujenzi wa mradi wa umeme wa Rufiji (*Stiegler's Gorge*) na kadhalika, bila usalama haya yote hayawezu kutekelezwa. Kwa hiyo naiomba Serikali itilie maanani katika masuala ya ulinzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongelea habari ya hospitali na naomba nilipongeze Wizara ya Afya kwa kazi nzuri wanayoifanya, pamoja na kwamba pongezi ambazo nilishazitoa hapo nyuma. Katika Kitengo cha Moyo cha Jakaya Kikwete (JKC), Kitengo cha Mifupa (MO), Kitengo cha Dharura na Kitengo cha Akina Mama (Wodi ya Wazazi;) naomba fedha zipelekwe kwa wakati ili ziweze kukidhi na kuzuia maafa zaidi ambayo yanaweza kutokea katika maeneo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuwe na ukaguzi wa maeneo wakati wa kufanya usafi siku za Jumamosi kwa sababu siku hiyo akina mama wengi katika Mkoa wa Dar es Salaam ambao wanafanya biashara ya kuuza maandazi na vitafunwa, chapati na kadhalika, muda wao wa kufanya biashara ni asubuhi mpaka hapo saa tatu. Sasa kule muda huo unakuwa umepigwa marufuku, hakuna kufanya biashara mpaka saa nne, na ikifika saa nne muda wa kunywa kifungua kinywa utakuwa umeshakwisha, kwa hiyo akina mama hawa wanaathirika sana.

Naomba Serikali husika, najua kero hii itakuwa si Dar es Salaam tu, hata mikoa mingine, iangalie eneo hili ili kuinusuru hali ya akina mama ambao wamekopeshana hela ndogo ndogo kutoka kwenye VICOBA vyao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba Serikali iongeze vyuo vingi vya ufundii ili kuwaweka vijana wetu tayari kwa ajili ya kuajiriwa katika maeneo ya viwanda. Bila kuwatayarisha vijana kutakuwa na changamoto kubwa katika kupata sifa ya kuajiriwa katika viwanda. Baada ya kusema hayo, nawashukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. JANETH M. MASABURI: ... namalizia, nawashukuru sana...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana, ahsante sana...

MHE. JANETH N. MASABURI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nkamia, atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Umbulla na Mheshimiwa Hussein Bashe ajiandae.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru sana wewe bunafsi, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia leo kuwa na afya njema. Kwa namna ya kipekee tena niongeze kukushukuru sana Profesa Dkt. Mtemi Chenge kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru sana na nimpe pongezi za dhati kabisa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli, mwalimu wangu, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waziri Mkuu, Mawaziri wote na Makatibu Wakuu wote

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee kabisa uniruhusu nimpongeze sana ndugu yangu Jafo,

anafanya kazi nzuri sana. Mnyonge mnyongeni haki yake mpeni; nami naamini kwa kazi hii anayoifanya Jafo huwezi kujua huko mbele ya safari, kikubwa endelea kumuomba Mwenyezi Mungu, Mungu ndiye anayepanga kila kitu. Nikupongeze sana kaka yangu Kakunda na Naibu Mawaziri wote wawili, Katibu Mkuu Mzee wangu Mzee Iyombe, dada yangu Chaula na Nzunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze na suala la maji. Serikali kupitia TAMISEMI na hata Wizara ya Maji wanafanya kazi kubwa sana kwenye miradi mikubwa na miradi midogo, lakini msema ukweli ni mpenzi wa Mungu. Kama Mheshimiwa Rais ameweza kufanikiwa kupunguza ujisadi bado eneo la maji kuna ujisadi mkubwa sana kwenye miradi ya maji vijiji. Miradi mingi haikamiliki kwa wakati, miradi mingi fedha zinafujiwa, miradi mingi haiko kwenye kiwango matokeo yake Serikali inaingiza fedha nyingi lakini miradi hii baada ya muda mfupi inakufa. Niombi sana jambo hili mliangalie kwa umakini na ikiwezekana Serikali undeni tume maalum kuchunguza miradi mikubwa na midogo ya maji nchi nzima kwa sababu kuna *crisis* kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mdogo tu, kuna mradi mmoja wa maji uko kule kwenye kijiji kinachoitwa Lahoda, nilikwenda na Mheshimiwa Waziri Kakunda. Serikali imetoa shilingi milioni 551 lakini hata tone la maji hakuna, na Waziri kaenda pale aadanganywa kwamba baada ya mwezi mmoja tutarekebisha mradi huu, maji yataanza kutoka. Waziri Kakunda akaagiza apelekewe akiba ya fedha walimwambia kuna shilingi milioni 83, hakuna hata senti tano. Kesho wanamuona Mheshimiwa Rais hafai, kumbe ni kwa sababu ya watendaji wachache. Niiombe Serikali ichukue hatua juu ya jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kule Chemba tunavyozungumza hapa, Mondo, Daki, Hongai, Chandama; tumechimba maji muda mrefu lakini *two years now* hakuna kinachofanyika. Niiombe Serikali, inafanya kazi nzuri sana, lakini hebu hakiksheni huko chini tunakotoka sisi miradi mingi ni *useless*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilikuwa nataka nizungumzie kidogo elimu. Nadhani kuna mahali tume-mess up. Hivi mwalimu alikuwa anakwenda darasani anakwenda anasema *good morning folks, how are you?* Leo unampeleka akafundishe chei chei shangazi. Si kwamba walimu hawatoshi, kuna tatizo kwenye upangaji wa walimu. Shule za mijini, hapa Dodoma Mjini kuna *access* ya walimu 371, shule ya sekondari ya Mpendo ina walimu wanne. Sasa hivi tatizo ni kukosekana kwa walimu au tatizo ni mpango wa walimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe, hebu fanyeni tathmini kabla ya kufanya hilo zoezi. Mnatawanya walimu bila kujua; TAMISEMI, leo mzee lyombe uko hapa baba yangu, kwanza shikamoo.

Nikuombe, leo TAMISEMI mnapanga Mwallimu Juma Nkamia anaenda shule ya msingi Msaada. Akifika pale halmashauri anamkabidhi barua nimepangiwa shule ya msingi msaada, wapelekeni walimu acheni Halmashauri ndizo zipange waende wapi, lakini ninyi mtapanga wataenda kujazana mahali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hivi katika shule za mijini walimu wengi wamejaa wanatoka wapi? Wengi wasichana wazuri. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia, shule nyingi za mijini wasichana wengi, wazuri tu hivi, hivi hawa wanapangwa makusudi au wanakosea? Niwaombe tu, fanyeni utafiti muone. Hapa tuna vitu ambavyo hatuendi sawasawa na matokeo yake watu wanafikia hatua wanasema; "aah, unajua Serikali ya CCM haijafanya..." si kweli! Wapo watu ndani ya Serikali wanafanya makosa kinachotukanwa Chama cha Mapinduzi, chukueni hatua! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye elimu hiyo hiyo, ajira za walimu. Ajirini walimu wa kutosha, lakini mhakikishe wanapangwa kule kwenye matatizo kweli si unaajiriwa vimemo kibao, acheni hii kitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *issue* ya watumishi, mimi sielewi tu. Watumishi kwenye halmashauri wengi hawatoshi, lakini nchi hii hapa katikati hapa kuna kitu tumefanya makosa makubwa sana, tumeongeza maeneo mengi ya utawala wakati hatuna *resources*. Hivi unaweza kuniambia uligawaje Wilaya ya Siha na Wilaya ya Hai zikawa Wilaya mbili? *Population* ya pale ipoje? Hapa ni watu walitafutiwa vyeo. Tufike mahali tuangaie, kuna baadhi ya wilaya hazistahili kuwa Wilaya, vunja; Wilaya ina watu 70,000 ya nini? Ujisoma kwa sisi tuliosoma mambo ya *International Relations* kuna kipengele kinasema mtu anatafutiwa nafasi kwa sababu hana eneo lingine, anatafutiwa nafasi ili awe kiongozi mahali aje atafutiwe nafasi kubwa, *this is wrong*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali, zipo baadhi ya Wilaya vunja, kama wapo Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi, kazi ziko nyingi za kufanya, wapeni hata Wakuu wa Idara tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho TAMISEMI ninyi ndio mnashughulikia Mfuko wa Jimbo, unakuta baadhi ya maeneo Wabunge hawa ile fedha ya Mfuko wa Jimbo, fanyeni tathmini upya. Tangu sheria imetungwa mpaka leo kiasi kile kile, jimbo limeongezeka, Chemba sasa hivi tuna karibu watu laki tatu na ushee, ile ile, hatuwezi kwenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na niishukuru sana Serikali kwa kweli, leo mimi nikotoka hapa kwenda Chemba dakika 45. Nakushukuru sana Mheshimiwa Rais, ongezeni fedha kwenye *TARURA* barabara zetu zijengwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru Mheshimiwa Jafo nina vituo vya afya viwili, Hamai milioni 400, Kwa Mtoro milioni 500, naomba zile za Kwa Mtoro ziingie tutulie. Umenipa bilioni moja na milioni mia tano Hospitali ya Wilaya ya Chemba...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Nkamia. Tunaendelea, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Hussein Bashe na Mheshimiwa Deo Sanga wajiandae.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa hii. Naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye amenipa afya na kuweza kusimama mahali hapa leo kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kabla sijaanza kuchangia na kutoa mchango wangu katika Wizara hii na mimi niungane na wenzangu Wabunge wa Mkoa wa Manyara ambao wameshachangia kusema kweli, kutoa shukrani za dhati kwa mambo makubwa ambayo Mheshimiwa Rais wetu mpendwa katika ziara zake za hivi karibuni ametutendea katika mkoa wetu. Mheshimiwa Rais amesimamia kauli yake, yeye amesema hatabagua mpinzani kwa *basis* ya itikadi wala ya chama wala ya dini wala ya kabilâ. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mfano Jimbo la Simanjiro liko upinzani na ninategemea mdogo wangu Mheshimiwa James Ole-Miliya hapa atakaposimama amshukuru Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa maendeleo makubwa ambayo ameyafanya katika Jimbo lake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais tunamshukuru kwa mambo makubwa mengi lakini makubwa matatu naomba nichukue nafasi hii kumpongeza nayo; la kwanza; madini ya *Tanzanite* ambayo yalikuwa yananufaisha watu wengine na pengine hata nchi nyingine Mheshimiwa Rais ametuletea mfumo thabiti, mfumo rasmi kuhakikisha kwamba wanufaika wa kwanza wa madini haya watakuwa Watanzania na zaidi sana hata akina mama yeyoo wa Wilaya ya Simanjiro, hususan Mererani watanufaika na madini haya. Amesema atahakikisha kwamba ukuta uliojengwa hauwaathiri wale wanawake wanaochenjua madini haya, waliokuwa wanananufaika kidogo kidogo, bali

atawatengenezea mfumo rasmi waendelee kunufaika, tunamshukuru Mheshimiwa Rais wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Mheshimiwa Rais alipokuja Mererani tulimwambia tunakuomba baba yetu tenda miujiza kwa sababu shida ya maji katika Mji wa Mererani imedumu miaka nenda rudi. Aliwaangalia wale wanawake wa Mererani wanaoswaga punda toka asubuhi mpaka jioni wakisaka maji, akasema nimelichukua hilo. Baada ya muda mfupi ametuletea mradi mkubwa wa maji wa thamani ya shilingi milioni 780, sasa hivi baada ya muda mfupi shida ya maji itakuwa historia Mererani, tunamshukuru Mheshimiwa Rais wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hilo tu, tulimlilia, wanawake wa Mererani walimlilia, baba tunaomba msaada sisi tukipata *complication* ya kujifungua tunakimbizwa kwenda Kilimanjaro KCMC ama Selian kwa kutumia magari ya polisi, tunakuomba utusaidie gari la wagonjwa. Mheshimiwa Rais bila kigugumizi, bila kumung'unya maneno aliwajibu palepale nitawaletea *ambulance*. Juzi amekuja kufungua ukuta amekuja na *ambulance* yetu mkononi, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mungu ambariki. Ni dhahiri kwamba huyu ni Rais wa wanyonge. Tunamshukuru kwa moyo wa dhati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na haya yote si kwamba, Mkao wetu wa Manyara uko salama kwa masuala mengi. Wilaya ya Kiteto inasikitisha kwa suala la *ambulance* haina. Tunaomba Wizara iliangular hili kwa sababu, tangu nikiwa Kiteto gari la wagonjwa linakwenda kumchukua mgonjwa linaharibikia huko huko linatafutwa gari lingine. Tangu wakati huo hadi leo hakuna gari la *ambulance* Kiteto. Naomba hili Mheshimiwa Waziri alibewe na atusaidie katika nyanja hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa nizungumzie suala la uwezeshwaji wananchi kiuchumi. Kwanza kabisa naomba ni-declare *interest* kwamba mimi ni mtaalam wa *microfinance*. Nimefanya

suala la kutoa mikopo kwa wanawake na vijana kwa takribani miaka 20; kwa hiyo, ninaelewa ninachosema, lakini niipongeze Serikali kwa kututengea shilingi bilioni 61.6 kama asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri zetu kwa ajili ya wanawake na vijana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilikuwa naomba na nia yangu ya kuzungumzia eneo hili ni kuliboresha na kuhakikisha kwamba bilioni 61.6 zinaweka *impact*, si kwamba zitolewe tu kwa sababu sisi kama Wabunge kazi yetu kubwa ni kuhakikisha kusema kwamba hizi fedha zitoke, hizi fedha zitoke na bado ni kidogo, lakini hatuliangalii sana suala la kusema inaweka *impact* kiasi gani na wanufaika wanakuja kunufaika kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikundi 18,000 vilivytajwa katika kitabu cha Waziri je, ni vikundi vya watu wawili wawili, watu 10, watu 30, kwa sababu, hatuna uhakika wanufaika ni wananchi wangapi. Maana vikundi hivyo ni vikundi tu vya wanawake na hatujui kama ni vikundi vya wanawake pamoja na vijana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwekwe wazi, ili tuhakikishe kwamba, fedha hizi zinazotoka kwenye Halmashauri zetu zinaweka *impactsahihi* na zitanufaisha wanawake na vijana, na pia nadhani tuweze kujua kwamba katika wanawake na vijana, je, hawa vijana ni pamoja na vijana wa kike ama ni vijana wa kiume? Na umri wa hawa wanawake sasa unaishia wapi, ili wao wawe wanawake wanaonufaika? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ina wanawake wengi wakulima na wafugaji. Sasa hawa ni wale waliowekwa pembeni na mfumo rasmi wa ukopeshaji. Je, hii asilimia 10 fedha hizi shilingi bilioni 61 zinawanufaishaje wanawake wakulima na wafugaji, ili nao waweze kunufaika na asilimia hizi zinazotoka kwenye halmashauri yetu? Nadhani Mheshimiwa Waziri atakapo *wind up* atatueleza. Vilevile pengine si vibaya tukajua ni *criteria* gani inayotumika kuwapata hawa wanawake na vijana, kila mtu anaweza akakopa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hizi fedha kama ni mikopo ni lazima zifuatiliwe, katika bajeti ya ufuatiliaji, bajeti ya kuunda vikundi, bajeti ya kuweka *criteria* wanawake gani wakope, inajumuishwa katika hiyo bilioni 61 ama kuna bajeti ya pemberi ya kuhakikisha kwamba fedha hizi zinafuatiliwa vizuri? Na nani wanaofutilia, ni maendeleo ya jamii ndani ya Halmashauri ama kuna kundi la watu ambao wanaweza wakafanya kazi hii kwa ufanisi? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tungeweza kuweka wazi suala la urejeshaji. Kama hizi fedha zinarejeshwa kwenye halmashauri sijui ni kwa nini basi tuendelee kutenga asilimia 10 kila mwaka? Fedha zinazorejeshwa naamini kwamba, kama ni mfuko wa kuzunguka ina maana kwamba ni fedha zinarudi ili ziweze kukopeshwa. Kwa hiyo, nina hakika kwamba zinaweza zikapunguza hii asilimia inayotolewa kwa kila mwaka kwa Halmashauri zetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kwa kifupi sana pia suala la Makao Makuu ya Wilaya yetu ya Mbulu Vijijini; Wilaya ambayo ni halmashauri mpya ambayo tunaishukuru Serikali yetu kututengea na kutupa wilaya mpya. Hata hivyo tunaelewa kwamba suala la Makao Makuu ya Wilaya ni suala la kisheria, lakini kumekuwa na kigugumizi cha kuhakikisha wananchi wanagongana vichwa kwa sababu kila mtu anatamani Makao Makuu ya Wilaya yawe mahali fulani. Sisi wananchi hatujali wa Manyara, mimi binafsi ninayechangia, ili mradi TAMISEMI ituambie, kwamba Makao Makuu ya Wilaya ya Mbulu Vijijini yawe Dongobesh kwa sababu, kwa sensa ya mwaka 2012 ina idadi ya watu 239,637 wakati Haydom iko pembezoni sana na ina idadi ya watu 80,000. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa masuala haya ni ya kisheria, kama Serikali ina sababu ya kuridhisha, inataka kuweka Makao Makuu Haydom, ruksa. Ilimradi wananchi sasa wawe watulivu, taarifa hii itolewe rasmi na TAMISEMI ili wananchi wetu watulie na waendeleze shughuli zao za maendeleo badala ya kuwaza usiku kucha Makao Makuu yanaweza kuwa wapi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nimepanga kuzungumzia kwa nguvu haya. Naendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu kwa juhudini kubwa aliyotupa maendeleo katika Mkoa wetu wa Manyara, naomba Mwenyezi Mungu ampe maisha marefu na tunamuombea Mungu azidi kumbariki, asante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa, Mheshimiwa Hussein Bashe na Mheshimiwa Deo Sanga, wote mnaona muda wetu si rafiki.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naushukuru kwa kunipa fursa. Kwanza nitumie nafasi hii kumpungeza ndugu yangu Mheshimiwa Jafo na Naibu Mawaziri wote wawili wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanazofanya na kujituma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka nianze kwa jambo moja; jamii yoyote inayohitaji maendeleo msingi mkubwa wa maendeleo ni haki na viongozi kujua kwamba wana wajibu wa kulinda uhai na mali za kila raia. Nasema hivi kwa sababu kumekuwa na hii *culture ya impunity* na matukio madogo madogo yanayoendelea, na mimi kwa mtazamo wangu naamini kwamba *it is a high time* Serikali ikaja hadharani na kuteka *bold decision* juu ya haya mambo ambayo yamekuwa yakiendelea katika jamii yetu; kwa sababu yanaharibu taswira na heshima na jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niongee kuhusu TAMISEMI. Ukitazama taarifa ya Waziri *only 40 percent maximum of 50 percent* ya *Development Budget* ndiyo imekwenda kwenye Halmashauri zetu. Hata hivyo katika Halmashauri zetu mapato yetu ya ndani yanaathirika sana pale ambapo *Central Government* inashindwa kushusha fedha kwa wakati katika Halmashauri, na kule ndiko ambako kuna *burden* kubwa iliyopo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kisera tumeamua kuwa na *D by D*, naomba nitumie takwimu hizi kuwaonesha

Waheshimiwa Wabunge. Katika sekta ya elimu ukichukua *ratio* ya pato letu la taifa *vis-a-vis* kile ambacho tuna-*allocate* katika sekta; kati ya mwaka 2006 mpaka 2007/2008 *ratio* ilikuwa ni asilimia 20 ya pato letu la ndani ndiyo ilikuwa *allocated* kwenye sekta ya elimu. 2009 na 2010 ikawa asilimia 18. Imeendelea kushuka, mwaka 2017/2018 tumetenga *only 15 percent* ya pato letu la ndani kupeleka kwenye sekta ya elimu, sasa nini *implication* yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama matokeo ya kidato cha nne asilimia 60 ya wanafunzi wanaomaliza mtihani wa kidato cha nne wanafeli; na ni kwa nini? Kwa sababu kwa takwimu, na hizi ni takwimu za *BEST, satisfaction* ya walimu, *job satisfaction only 30 percent* ya walimu walioko katika shule zetu za msingi na sekondari ndio wako *satisfied* na kazi wanayoifanya, maana yeke tunaandaa janga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini fedha za elimu tunazozipeleka TAMISEMI, asilimia 96 ya fedha hizi zinatumika kwenye *administrative only*, haziendi kwenye *development* ya *education*, kwa maana ya kujenga *infrastructure* na kuangalia stahiki za watoa elimu, hili ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna umuhimu mkubwa sana Serikalini wa kufanya *replanning*, nini *focus* yetu? Tunataka kujenga uchumi wa viwanda. Ili tujenge uchumi wa viwanda ni mambo mawili tu, moja ni uwepo wa rasilimali kwa maana ya *raw material*, lakini uwepo wa rasilimali watu. Kama elimu yetu matokeo yake ni haya ni matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwape mfano wa *TARURA*; mwaka jana tumetenga shilingi bilioni 246, mwaka huu tunatenga shilingi bilioni 272. Ukitazama mipango yetu ya maendeleo ni *urban centric*, yote inatazama Dar es Salaam, Mbeya, fedha zinaenda Jiji la Mwanza na vitu vya namna hiyo, lakini kule ambako kuna wazalishaji wa rasilimali, kwa maana ya wakulima, barabara zao tumeziweka chini ya *TARURA*, hatuzipi fedha ama tunachoki-*allocate* ni kidogo, tuna matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kuhusu suala la *TARURA*; Waheshimiwa Wabunge wamesema tuangalie hela ya mafuta *30 percent* kwa *ratio* ya *70 percent*, ninaomba Wizara ya Fedha angalieni kutumia chanzo cha *Gaming Board*, chanzo hiki kiwe *dedicated* kisheria, kiende moja kwa moja kuongeza Mfuko wa *TARURA*. Pamoja na *ratio* mnayoitumia sasa hivi tumieni *Gaming Board* kuna fedha, watu wana-*bet*. Tumeamua kuruhusu watu wacheze kamari, basi tumle huyu nguruwe vizuri aliyenenenepa ili matokeo ya kule yaje basi kwenye barabara, hili ni eneo lingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 52 anasema; ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi Tanzania unategemea kwa kiasi kikubwa sekta ya kilimo. Sekta hii ni mhimili wa uchumi wa viwanda na kuchangia kuifikisha Tanzania kwenye uchumi wa kati. Ili tuweze kufikila lengo hili ni lazima tuwekeze kwenye sekta ya kilimo, tutoe fedha za pembejeo, tujenge barabara za kutoa mazao kwa wakulima vijijini kuleta kwenye barabara kubwa zilizojengwa na *TANROADS*, bila kufanya hivi hatuvezi kutatua hili tatizo la kuondoa umaskini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nioombe Serikali. Leo kule kwenye Halmashauri, na mimi nasema hii kwa nia njema, kule kwenye Halmashauri Serikali kwa maana ya Rais amekuja na *vision* kubwa kupambana na rushwa, kujenga miundombinu, kuhakikisha kwamba wananchi masikini wanapata haki, lakini ukitazama kinachoendelea katika Halmashauri zetu, ni kero kubwa kwa wafanyabiashara wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mkulima kabeba mpunga wake kutoka Katavi kwenye gari la tani 10 kaamua kufunga yale magunia kilo mia-mia badala ya kilo 90, lakini uzito ni tani 10, akifika njiani anapigwa faini. Msafirishaji wa ng'ombe kutoka Nzega kuleta Dar es Salaam, amekatiwa ushuru, ana leseni, ana kila kitu, akifika njiani kasimamishwa kapigwa *fine*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongoza Halmashauri na nchi kwa faini, hatuwezi kuwasaidia hawa watu maskini. Ningemuomba Mheshimiwa Waziri Jafo wakati anakuja kufanya *winding up* hapa atuambie *definition*, kuna mgogoro mkubwa unaendelea kwenye *Local Government*. Tulipitisha hapa Waziri wa Fedha alileta Mabadiliko ya Sheria ya Fedha mwaka jana, wenye hoteli ambao wanalipa VAT je, wanatakiwa walipe *service levy*? Je, wanatakiwa walipe *hotel levy*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu sasa hivi kinachoendelea analipa VAT, anapelekewa *service levy* anapelekewa *hotel levy*, asipolipa anafungiwa. *This is a very bad thing*, na mimi nataka niseme Waheshimiwa Wabunge wa chama change, kwamba tunaweza tukajenga *standard gauge*, tunaweza tukanunua ndege, tunaweza tukajenga barabara, kama kero zinazohusu maisha ya watu ya kila siku hatutakuwa wakali kuitaka Serikali ichukue hatua mapema, sisi ndio tutakaoenda kunyooshewa vidole. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kule kwenye Halmashauri kila mtu ni mbabe. Mtu ana kabisahara ka-shilingi 500,000 anapigwa *fine* ya shilingi 2,000,000, *It is very unfair.* (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo ambalo nakuomba kabisa ndugu yangu Mheshimiwa Waziri Jafo toka *strong statement*. Hii tabia ya Wakurugenzi wetu kwenda kufungia watu makufuli, kwenda na polisi kuburuza, unaletewa sasa hivi *demand note*, *in a next one hour* umepigiwa kufuli. *Demand note* inasema nini, hujalipa *service levy*... (*Makof!*)

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sanga utanisamehe sana, lakini niliseme hili kwa ujumla kwa sababu ya maombi ya Miongozo asubuhi na majibu yake na taarifa, matokeo yake ndiyo haya. Sasa uwiano wetu wa vyama mnaufahamu. Kwa siku nzima tunaweza kuchangia Wabunge 32 tu. Sasa kwa uwiano wa uwakilishi wa vyama vinavyowakilishwa humu Bungeni mnajua tunavyofanya, Chama cha Mapinduzi 22, CHADEMA sita na CUF wanne. Sasa kwa vile tuna ACT na NCCR Mageuzi kwa haki huwa tunawaingiza kama mlivyoona leo.

Sasa ili uweze kuu-*manage* muda huu vizuri lazima uvute upande wa walio wengi, uanzo nao wanane, halafu ubebe wawili, maana mizunguko ni mitatu. Ubebe wawili huku halafu unaweza kubeba mmoja ukianzia huku, lakini itafika *round* ya pili unabeba saba, saba, wawili, wawili, unamaliza sita na huku utakuja imekaa vizuri, lakini inakuwa shida kweli, haki mnayo, lakini pia mimi nasema baadhi ya taarifa hizo zinatulia muda tu.

Nimeona niliseme hilo, lakini kutenda haki mimi nitawakabidhi katibu nao watawakabidhi viongozi wa Kambi. Sitaki Waheshimiwa Wabunge ambaorodha ilikuwepo kesho majina yao yasioneokane. Mimi nadhani tutende haki ili haya majina ambayo hayakupata nafasi leo kwa sababu mbalimbali yaanze kesho halafu ndipo wengine waingie hivyo, tutakuwa tunawatendea haki wenzetu vizuri. (*Makofii*)

Mwisho niliombwa Mwongozo na Mheshimiwa, leo katika Kikao cha Nane cha Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge, muda wa mchana kabla ya kuahirisha Bunge nilipokea maombi ya Mwongozo kutoka kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kuhusu uvunjaji wa Katiba. Suala hilo lilitokeza wakati wa mijadala ya Wabunge wakati wa kuchangia hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2018/2019 inayoendelea Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mhagama (Mb), alifafanua katika maombi ya Mwongozo wake kuhusu kuibuka kwa mijadala inayohusu masuala ya imani, viongozi wa dini na nyaraka mbalimbali za Kitume ambazo zimekuwa zikitolewa na viongozi wa dini. Mheshimiwa Mhagama (Mb), aliomba Kiti kitoe Mwongozo kwa maneno yafuatayo, alitumia, nanukuu; "Kama ni sahihi mijadala inayoendelea ndani ya Bunge kuhusisha shughuli za imani za kiimani za imani tofauti." Mwisho wa kunukuu.

Katika kujenga hoja yake Mheshimiwa Mhagama (Mb), alitumia lbara ya 19 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Waheshimiwa Wabunge, niliwaeleza kuwa kabla ya kutoa majibu ya Mwongozo huo nilihitaji kupitia Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) ili niweze kubaini ni michango ipi ya Wabunge iligusa masuala ya imani za dini, viongozi wa dini na nyaraka mbalimbali za kitume. Baada ya kupitia Taarifa Rasmi za Bunge nimeridhika kuwa katika michango ya baadhi ya Wabunge kuna maeneo yaliyogusa masuala ya dini na imani mbalimbali. Kwa mfano mchango wa Mheshimiwa John Heche (Mb) ambaye wakati anatoa mchango wake alieleza kuwa Serikali iliyahi kuwatukana viongozi wa dini, Maaskofu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunafahamu kuwa mbele yetu kuna Bajeti ya Serikali, ni wajibu wetu kutoa michango yetu ya mawazo kuhusiana na bajeti hiyo na kisha kuipitisha kama tutaona inafaa.

Waheshimiwa Wabunge, michango inayogusa imani ya dini tulizonazo, madhehebu, makundi mbalimbali ya kidini na dini mbalimbali tulizonazo haina nafasi katika michango tunayotoa kwani isipofanyika kwa umakini inaweza kupandikiza chuki kati ya Serikali na viongozi wa dini, madhehebu mbalimbali mionganoni mwetu na hata kati ya mtu mmoja, kati ya mtu na mtu, jambo ambalo linaweza kutuletea mgawanyiko katika Taifa letu.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mimi binafsi na Kiti hiki hakitakubali Bunge hili kutumika kama uwanja wa kupandikiza chuki za kiimani za dini katika taifa. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika lbara ya 19(2) inaeleza bayana kuwa; "Kazi ya kutangaza dini, kufanya ibada na kueneza dini itakuwa ni huru na jambo la hiari la mtu binafsi, na shughuli za uendeshaji wa jumuiya za dini zitakuwa nje ya shughuli za mamlaka ya nchi." Mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa kikatiba shughuli za uendeshaji wa dini ni nje ya shughuli za mamlaka ya nchi, hapa Bungeni hilo pia si jukumu letu. Endapo Bunge hili litaendekeza kujadili shughuli za kidini au kiimani, jambo linalopaswa kutekelezwa na viongozi wa dini na waumini wao tena katika maeneo maalum, itakuwa tunakiuka Katiba.

Waheshimiwa Wabunge, kwa maelezo hayo Mwongozo wangu wa Kiti ni kuwa, mijadala yote hapa Bungeni ijiepushe kujihusisha na masuala yanayohusu imani za dini, ibada, nyaraka za kitume, viongozi wa dini, pamoja na makundi mbalimbali ya kidini. Mijadala hiyo inaweza kufanyika tu endapo itakuwa inaingilia Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge. Hivyo, naelekeza maneno yote yanayotaja viongozi wa dini yaliyotolewa na Mheshimiwa John Heche (Mb) yafutwe katika Taarifa Rasmi za Bunge. (*Makof*)

Mwongozo huu nimeutoa leo tarehe 12 Aprili, 2018 mbele ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi, tarehe 13 Aprili, 2018.

*(Saa 01:45 Usiku Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 13 Aprili, 2018 Saa Tatu Asubuhi)*